# HADITHI KAMA CHOMBO CHA MAUDHUI KATIKA FASIHI: UCHANGANUZI WA RIWAYA ZA MKANGI, G.K. *MAFUTA* (1984) NA *WALENISI* (1995)

**NA**

**ANAYE JOSPHAT VONYOLI**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU KENYATTA**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili (M.A) katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.**

**AGOSTI 2004**

Anaye, Josphat
*Hadithi kama chombo cha maudhui katika*
05/277414

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine.

ANAYE, JOSPHAT VONYOLI

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu.

BWANA MUGAMBI, P.J.M.

NA

BWANA MUTEGI, M.J.N.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa marehemu baba yangu Ayubu Anaye na marehemu Profesa George Katama Mkangi.

Natabaruku kazi hii pia kwa mke wangu Florence, mamangu Makungu na watoto wetu Kemoli, Amuyunzu, Anaye, Migare, Egunza na Ziro kwa kunipa moyo wa kuendelea na masomo nikiwa katika umri huu wangu.

## YALIYOMO

Mada ........................................................................ i

Ungamo ........................................................................ ii

Tabaruku ........................................................................ iii

Yaliyomo ........................................................................ iv

Shukrani ........................................................................ vii

Ikisiri ........................................................................ ix

Istilahi........................................................................ x

Vifupisho ........................................................................ xiv

## SURA YA 1

1.0 Utangulizi ........................................................... 1

1.1 Swala la Utafiti ........................................................ 2

1.2 Malengo ya tasnifu ................................................. 3

1.3 Sababu za kuchagua mada ...................................... 4

1.4 Misingi ya nadharia ................................................ 5

1.4.1 Mihimili ya nadharia ............................................ 9

1.5 Yaliyoandikwa kuhusu swala la utafiti .................... 12

1.6 Upeo wa utafiti ...................................................... 14

1.7 Njia ya utafiti .......................................................... 14

1.8 Kuchanganua data .................................................. 15

1.9 Mpangilio wa sura za utafiti .................................. 16

**SURA YA 2**


2.0.0 VIPERA VYA HADITHI NA UMUHIMU WA HADITHI

KATIKA FASIHI SIMULIZI ........................................... 18

2.0.1 Utangulizi ......................... ....................................... 18

2.0.2 Vipera vya hadithi ...................................................... 20

2.0.3 Ufafanuzi wa Utanzu wa hadithi .................................. 20

2.0.4 Hadithi za kihistoria .................................................. 25

2.0.5 Umuhimu wa hadithi ................................................ 27

2.0.6 Hitimisho ................................................................ 33


**SURA YA 3**


3.0.0 Utangulizi ............................................................ 36

3.1.0 Riwaya ya *Mafuta* .................................................. 38

3.1.1 Hadithi ya Mwenye Mkunazi .................................... 38

3.1.2 Hadithi ya Mama Fofi ............................................ 44

3.1.3 Hadithi ya Matope ................................................. 49

3.1.4 Hadithi ya Ti ....................................................... 56

3.1.5 Hadithi ya Mbeyu ................................................. 61

3.1.6 Hadithi ya Gweni ................................................. 65

3.1.7 Hadithi ya Jasho .................................................. 69

3.1.8 Hadithi ya Mtue ................................................... 71

3.1.9 Hitimisho ........................................................... 81

**SURA YA 4**

4.0 Riwaya ya *Walenisi* .................................................. 87

4.1. Utangulizi .................................................. 87

4.1.1 Hadithi ya Mapacha .................................................. 94

4.1.2 Hadithi ya Maskini Jeuri .................................................. 103

4.1.3 Hadithi ya Wachuna .................................................. 109

4.1.4 Hadithi ya Mabavu .................................................. 121

4.1.5 Hadithi ya Moto .................................................. 125

4.1.6 Hadithi ya Mchawi .................................................. 132

4.1.7 Hadithi Kuu .................................................. 136

4.1.8 Hitimisho .................................................. 151

4.1.9 Mtindo wa Mwandishi.................................................. 155

4.2.0 Utangulizi.................................................. 155

4.2.1 Mtindo wa Usimulizi .................................................. 156

**SURA YA 5**

5.0.0 Hitimisho .................................................. 171

5.1.1 Utangulizi.................................................. 171

5.1.2 Maathiriano ya Fasihi Andishi na Fasihi Simulizi ...... 175

5.1.3 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi .................................................. 181

5.1.4 Kiambatanisho A .................................................. 184

Kiambatanisho B .................................................. 185

Marejeleo.................................................. 191

**SHUKURANI**

Ningependa kutoa shukrani zangu kwa Maulana kwa kunipa afya nzuri, uwezo na ari ya kuendeleza masomo yangu.

Ninatoa shukrani zangu kwa Mwalimu P. Mugambi na Mwalimu M. Mukobwa ambao walikuwa wasimamizi wangu kwa kunipa mwongozo na mwelekeo ulioniwezesha kuimaliza kazi hii. Nawashukuru pia wahadhiri wangu wote katika Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kunipatia miangaza, kuniongezea maarifa na kunitia moyo masomoni. Ningependa kutoa shukurani zangu kwa Mwalimu Hannah Gathenji aliyenifundisha somo la Isimu, Daktari Richard Wafula wa Idara ya Kiswahili na Mwalimu George Mwiruki kwa usaidizi wao wa kipekee.

Natoa Shukurani zangu kwa Bi. Anne Kimotho na Mary Khaemba kwa ustahimilivu na kujitolea kwao na kuipiga chapa tasnifu hii.

Ningependa pia kushukuru wenzangu tuliosoma nao Bi. Jacinta Magaju na Bi. Marion Nyanchama. Tuliweza kujadiliana nao katika kisomo hiki kigumu, waliweza kunitia moyo. Ningependa pia kutoa shukurani zangu kwa wafuatao kutoka shirika la Uchapishaji la East African Educational Publishers Ltd., Bwana Henry Chakava, Mwenyekiti, Bwana Barack Muluka, Maneja Mkurugenzi na Bi. Lilian Dhahabu Meneja Mhariri, kwa usaidizi wao wa kipekee ambao uliniwezesha kuendelea na masomo yangu. Mungu awashehenezee baraka zake. Pia

ningependa kumshukuru Bwana Jimmi Makotsi wa Acacia Publishers Ltd. kwa usaidizi wake na kunipa moyo.

Shukurani zangu za mwisho ziwaendee Bwana Egara Kabaji na Bi. Susan Lukano aliyekuwa mwalimu Mkuu wa Chamakanga Girls High School na Abungu Tao wote kwa kunitia moyo ili niende kusoma.

Mwisho ningependa kuwashukuru marafiki zangu popote walipo kwa kunitia shime.

**IKISIRI**

Utafiti huu unachanganua hadithi kama chombo cha kutolea maudhui katika riwaya za George Katama Mkangi za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Kwa kutumia nadharia ya uhalisia wa uyakinifu wa kijamaa iliyoasisiwa mwaka wa 1934, miaka michache baada ya mapinduzi ya Urusi ya mwaka wa 1917, tumechunguza jinsi Katama Mkangi ametumia urithi wa fasihi simulizi wa jamii yake kutusawiria uhalisi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Utafiti huu umechanganua hadithi tofauti katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi* na kubainisha maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yaliyojikita katika hadithi hizo. Utafiti huu umeonyesha pia jinsi hadithi za kijadi zimetumiwa kama nyenzo ya kutolea maudhui ya kisasa.

Kazi hii ina sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi unaojadili suala la utafiti, sababu za kuchagua mada hii, mbinu za utafiti, mapito ya kazi muhimu na misingi ya nadharia. Tungependa kusisitiza kuwa uzito wa utafiti huu umewekwa juu ya hadithi kama chombo cha kutolea maudhui. Hadithi hizi za jadi zimefungamanishwa na uhalisia wa maisha ya jamii kisiasa, kiuchumi na kijamii. Sura ya pili imejadili tanzu za hadithi na umuhimu wake katika riwaya hizi mbili. Sura ya tatu na nne zimechanganua hadithi zinazopatikana katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* na mtindo wa kutolea hadithi katika riwaya hizi mbili.

Sura ya Mwisho ni hitimisho ambamo tumebainisha uhusiano na athari baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi na kutoa mapendekezo ya haja ya utafiti zaidi juu ya mitindo anayotumia Mkangi katika riwaya zake.

## ISTILAHI ZILIZOTUMIKA KATIKA UTAFITI HUU NA VIFUPISHO

Katika utafiti huu, istilahi zifuatazo zimetumika kwa kuzingatia maana kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Hadithi: | Tungo za masimulizi kwa kutumia lugha ya nathari kwa mpango wa mtiririko na vitushi kutoa kisa au maudhui. |
| 2. | Hadithi katika hadithi: | Masimulizi yanayotoa maudhui miongoni mwa hadithi kuu. Ni matumizi ya hadithi fupifupi katika hadithi kuu. |
| 3. | Data changishi: | Maelezo kutoka kwa marejeleo ya vitabu, watu, magazeti na majarida. |
| 4. | Utafiti wa Kimsingi: | Utafiti wa awali kutoka nyanjani au kutokana na walioona na kushiriki katika matukio. |
| 5. | Sanaa: | Ufundi wa hali ya juu wa kuwasilisha jambo kupitia kwa maandishi, mazungumzo, uchoraji, ufinyanzi, ufumaji miongoni mwa njia nyingine. |
| 6. | Tanzu: | Kitengo kinachohusu fasihi simulizi au fasihi andishi. |
| 7. | Vipera: | Tanzu ndogo zilizojikita katika tanzu kubwa (Tazama: vipera vya hadithi). |
| 8. | Kushonwa mdomo: | Kuzuia kwa vyovyote mtu/watu wasiweze kusema. |

9. Mwakenya: Kundi la kisiri lililochukizwa na mienendo ya watawala nchini Kenya kati ya mwaka wa 1980 na 1995. Pia kulikuwepo na chapisho kwa jina hilo. Kundi hili lilikuwa kundi haramu na kupigwa marufuku na serikali. Waliopatikana kuwa wafuasi wa kundi hili au watuhumiwa wa kundi hili walifungwa.

10. Pambana: Hili pia lilikuwa kundi la kisiri la kudai haki na pia lilitaka kuondoa utawala uliokuwepo. Pia kulikuwa na chapisho la siri kwa jina hilo. Kundi hili lilijitokeza baina ya miaka ya 1983 na 1995 lilipigwa marufuku na serikali ya Kenya.

11. Gladiata: Jumba la maonyesho katika enzi za kale za Warumi.

12. Kuvunja ngasu: Kusema ukweli wa mambo.

13. Nzora: Katika lugha ya kimijikenda (Kigiryama) ni 'kisu', au kitu ambacho hakifai au kisu kisicho faida, namna ya kisu butu kisichoweza kukata.

14. Ukarabati wa Mioyo: Msingi wa Kisayansi wa kuzinduana katika uyakinifu wa kijamaa ulioasisiwa na Stalin 1934.

15. Uchanganuzi wa yaliyomo: Kuchambua mambo yaliyo katika maandishi au makala.

16. Mbinu ya ustahilivu: Hii ni mbinu ya utafiti ambayo huwa haitumii tarakimu sana. Mara nyingi utafiti wa aina hii hutumia maelezo tu.

17. Nokolani: Hili ni neno lililotumiwa kwa maana ya zahanati/hospitali.

18. Trimi: Chombo cha kusafiria ambacho huenda kwa kasi sana.

19. Jehanamu: Duniani alikotoka Dzombo kumefananishwa na Jehanamu kulingana na matendo mabaya ya huko.

20. 'Posho': Kipimo cha unga kilichotolewa na wakoloni kwa wafanya kazi wao kama chakula ili watumie kwa muda wa juma moja. Kipimo hiki kilijumuisha unga, maharagwe na chumvi.

21. Ufyanduzi: Serikali.

22. Msuko: Ploti au maelezo kuhusu maudhui.

23. Tuni: Matumizi ya sauti ili kuonyesha hisia za mtu. Hasa anapokasirika.

24. Misendu: Hutokana na neno la kabila la Wakimbundu kutoka Afrika ya Kati. Huwa linatoa dhana ya 'Hadithi za Kihistoria.' Neno hili limetumiwa na Ruth Finnegan (1970).

25. Tanye: Neno ambalo hutokana na kabila la Wadogori wa Afrika Magharibi lichukualo dhana ya visasili. Misendu na Tanye yametumiwa na Ruth Finnegan (1970:364).

26. Kufunga nyama: Kufumba fumbo. Kufumbua fumbo kulihitajika wakati fumbo limefumbwa. Hali ya kufumba ndiyo iliyoitwa 'kufunga nyama'. Fumbo hili lilihitajika kufumbuliwa na wengine.

27. Tendohisia: Tendo linalojitokeza bila hiari kwa mfano kupiga chafya au kicheko.

28. Mkataba wa Berlin: (Berlin Conference 1884) Huu ulikuwa mkutano uliofanyika nchini Ujerumani mwaka wa 1884-5 kujadili jinsi nchi za Ulaya zingeweza kugawana bara la Afrika bila matatizo au vita vyovyote miongoni mwao.

**VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| TUKI: | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. |
| USIU: | United States International University. Chuo hiki kina mojawapo ya mabehewa yake hapa jijini Nairobi. Hapa ndipo Profesa George Katama Mkangi alikuwa akifanya kazi. Mahojiano na mtafiti yalifanyika katika ofisi yake chuoni tarehe 6-8-03. |
| NARC: | National Rainbow Coalition. Muungano wa vyama vilivyounda serikali inayotawala nchini Kenya baada ya uchaguzi wa mwaka 2002. |
| KAPE: | Kenya African Primary Examination |
| CEE: | Common Entrance Examination |



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

# SURA YA 1

## 1.0 Utangulizi

George Katama Mkangi ni mwanaelimu jamii aliyeandika riwaya za *Ukiwa* (1975), *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Utafiti huu umechunguza riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Katika riwaya hizi ametumia mbinu ya utanzu wa fasihi simulizi hasa hadithi kutoa maudhui yake. Mkangi ametumia "hadithi katika hadithi" kama mbinu ya kuwasilisha ujumbe wake. Maudhui ya ujumbe wake yamejikita katika hadithi hizo. Kwa kufanya hivi ameonyesha matumizi ya fasihi simulizi kutolea maudhui. Hisia zake zimesawirika vizuri katika hadithi anazotoa zinazofurahisha na kuelimisha. Mbonde, akinukuliwa na Sengo, (1988:12) anasema:

> Faishi simulizi ni mali Bia,
> Yahuisha, Yadumisha,
> Yastaajabisha, yaburudisha,
> Yazoeza, yahekimisha, yaelimisha.

Maneno haya yanatoa muhtasari wa dhima ya fasihi simulizi. Kwa mfano kusema ni mali ya bia ina maana kuwa tanzu za fasihi simulizi kama methali, semi, nyimbo, vitendawili, hadithi na kadhalika ni mali ya jamii. Fasihi simulizi yahuisha kweli kabisa. Uhai wa jamii ya kijadi ulitegemea amali za fasihi simulizi. Baadhi ya wanasanaa wanatumia mashairi, nyimbo au hadithi. Mkangi amehiari kutumia hadithi kwa sababu muhimu, kama alivyosema Abdilatif Abdalla (1973:23) katika

shairi lake *KUNO KUNENA*, Ubeti wa pili:

> Kana na huku kunena, kunenwa hakutakiwi,
> Kuna wanakuona, kunena kwamba si kuwi,
> Kunena wakikuona, kukuita hawakawi
> Kunena kani kwanuka, nikukome kukunena?

Abdilatif alisema mambo haya baada ya kuwekwa kizuizini kotokana na yale aliyokuwa amesema katika makala ya "Kenya Twendapi?" Hapa anaeleza kuwa kunena hakutakiwi na ikiwa watakuona basi watakuita na kukutenga na jamii. Maneno ya mdomo yanatoa hisia zaidi kuliko maandishi. Hadithi za Mkangi ni jazanda kuashiria mambo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, na udhalimu katika jamii yake. Hili lilifanya mambo yasijulikane waziwazi.

Wakati ambapo Mkangi alikuwa anaandika riwaya zake, waandishi kama Oyugi Okong'o, Al-Amin Mazrui na wengine walikuwa wametiwa kizuizini kuhusiana na maandishi yaliyokuwa yakitoa shutuma dhidi ya serikali. Al-Amin Mazrui aliandika tamthilia ya *Kilio cha haki* (1981). Wakati huo kulikuwa na dhuluma serikalini dhidi ya wanaharakati waliokuwa wakitetea haki katika nyanja mbalimbali za maisha. Katika riwaya ya *Mafuta* (1984), Mtue aliwekwa kizuizini kwa kuonyesha huruma hivyo kwamba kujinasibisha na Matope. Kazi zilizoonyesha uozo wa jamii hadharani zilipigwa vita. Mkangi alibuni hadithi zake ili ziweze kuchukuana na mazingira na wakati.

## 1.1 Swala la Utafiti

Waandishi wengi wametumia masimulizi kutolea maudhui yao. Utafiti huu utachunguza jinsi Mkangi alivyotumia 'hadithi katika hadithi' kama nyenzo au jazanda kutolea maudhui yake.

Kuna waandishi wengine ambao wametumia hadithi katika kumulika maswala ya kijamii. Kwa mfano George Orwell, *Shamba la Wanyama* (1975), Shabaan Robert katika kazi zake *Kusadikika* (1951), *Kufikirika* (1961), *Siku ya Watenzi wote* (1968) na *Adili na Nduguze* (1951), J.S. Mbiti (1966), *Akamba Stories*, Ngugi wa Thiong'o katika *Petals of Blood* (1977) na *Matigari* (1987). Katika jamii nyingi za Kiafrika hadithi zilikuwa na umuhimu wa kuasa, kuonya, kutumbuiza na kuelimisha. Katika *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995), Mkangi anatumia hadithi kama nyenzo kumulika malengo yake. Utafiti huu umechunguza jinsi Mkangi alivyotumia utanzu wa hadithi kama chombo cha kuangazia zaidi na kurutubisha maudhui yake. Utafiti huu umezingatia hadithi kama utanzu wa fasihi simulizi na jinsi mwandishi alivyoitumua kuelimisha na kutoa hisia za ndani. Utafiti huu umeongozwa na maswala haya:

(i) Kwa nini mwandishi alihiari kutumia hadithi ambao ni utanzu wa fasihi simulizi katika kazi zake za *Mafuta* na *Walenisi*?

(ii) Ni mambo gani muhimu yaliyojikita katika hadithi hizi?

(iii) Hadithi hizi ziliafiki mtazamo wa mwandishi kwa njia gani?

(iv) Hadithi katika hadithi zilikuwa na umuhimu gani katika riwaya hizi?

## 1.2 Malengo ya Tasnifu

Utafiti huu umeainisha hadithi mbalimbali na kuchanganua maudhui yaliyojikita katika kila hadithi zilizotumika katika *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995) kwa:

(i) Kuonyesha jinsi hadithi zilivyotumiwa kimtindo kusawiri maudhui ya mwandishi.

(ii) Kuchunguza jinsi hadithi hizi zilivyofinyangwa ili kuonyesha itikadi maalum iliyomchochea kuziweka hadithi hizi katika riwaya zake.

(iii) Kuchunguza jukumu la mwanasanaa wa fasihi kwa jamii yake, na kujadili umuhimu wa hadithi kama utanzu wa fasihi simulizi katika riwaya hizi mbili.

(iv) Kutaka kuziba pengo la dhana za jadi kama hadithi ambazo hazishughulikiwi katika utunzi wa riwaya.

## 1.3 Sababu za Kuchagua

Utafiti huu ulisababishwa na mshawasha wa matukio ya jamii ya mwandishi. Haya matukio ni:

(i) Riwaya za Mkangi *Mafuta* na *Walenisi* husomwa na wanajamii wa kila tabaka. Pia hufunzwa vyuoni na shuleni na kutahiniwa na Baraza la Mitihani, Kenya. Kwa hivyo vinapaswa kuhakikiwa ili kurutubisha wasomaji na mawazo yaliyo katika hadithi zilizo katika vitabu hivi.

(ii) Kutaka kuchangia taaluma ya uhakiki, hasa kazi za Mkangi ambazo hazijafanyiwa uhakiki wa kutosha.

(iii) Matumizi ya hadithi kama chombo cha kutolea maudhui katika riwaya hayajazingatiwa sana katika riwaya ya Kiswahili.

(iv) Riwaya hizi zinaibua nyenzo na mbinu mwafaka ya kisanii zilizotumiwa kufufua na kuhifadhi utamaduni wa jadi wenye manufaa kwa jamii ya kisasa.

(v) Hadithi zilizo katika riwaya hizi zinaburudisha na kuelimisha licha ya kutumiwa kijazanda kuficha maudhui.

(vi) Riwaya zote mbili ni masimulizi ya hadithi katika hadithi zilizosimulia juu ya maudhui yanayolingana.

(vii) Kwa maoni yetu hakuna mtu mwingine aliyeshughulikia maudhui na mtindo katika muktadha wa hadithi za riwaya hizi.

## 1.4 Misingi ya Nadharia

Katika kutazama kazi za Mkangi *Mafuta* na *Walenisi*, utafiti huu umetumia nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Nadharia hii inazingatia kiwango cha ubunifu na uhalisia wa maisha. Kufuatana na uhalisia wa kijamaa, sanaa haina budi kuonyesha misingi yake katika historia. Kimani Njogu (1997) katika utangulizi wake akimunukuu Engels katika Bisztray (1978:17) anasema kuwa "uhalisia kwa maoni yangu, humaanisha licha ya ukweli wa maelezo, ukweli katika usawiri wa wahusika halisi, katika hali halisi."

Kwa mujibu huu, dhana ya uhalisia katika fasihi ina vipengele vitatu ambavyo ni masimulizi yenye uhalisia katika muktadha wa jamii inayozungumziwa, kipengele cha pili ni kuwa na wahusika halisia wanaopatikana katika hali halisi. Mazingira ya wahusika hawa yana uhalisia. Wao ni wahusika wa miraba minne. Tatu, hali ya masimulizi imefungamana na matukio ya kihistoria. Masimulizi ya hadithi katika hadithi yaliyoelezwa katika *Mafuta* na *Walenisi* ni sawa na misingi ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Senkoro (1987: 66-7) katika kazi yake anasema:

> Uhalisia wa kijamaa huhakikisha kuwa uwezo wa kila mtu hujengwa, huimarishwa na Kukidhiwa kwa kusudi kubwa la kuyashinda kabisa mazingira ya mtu huyu kwa manufaa ya jamii nzima. Ni tapo lenye kumjenga mtu mwenye furaha na amani, ni tapo la watu wanaobadilisha na kujenga upya ulimwengu.

Maelezo haya ya Senkoro yanatoa uhalisia wa mambo jinsi yalivyo katika hadithi za *Mafuta* na *Walenisi*. Kwa mfano hadithi ya Ti, Matope na Mapacha ni miongoni mwa zingine. Hatima ya hadithi za Mkangi katika riwaya hizi ni kuleta mabadiliko katika jamii.

Mtazamo huu wa jamii una mawanda mapana ambayo huweka wazi kazi ya fasihi kwa jumla. Pia huzingatia matukio ya kihistoria na kuyafungamanisha na wakati maalumu na hisia za mwandishi ambazo hutokana na athari ya kijamaa. Nadharia hii hujikita katika fasili ya uhalisia ambako tunatazama uhalisia wa mambo katika jumuiya fulani ya wanadamu.

Uhalisia wa kijamaa huzingatia kwa undani historia ya jamii na mivutano yake. Sifa kubwa ya uhalisia wa kijamaa ni kutetea masilahi ya wafanya kazi na kuwapa matumaini ya siku za usoni.

Gorky katika kazi yake S*ocialist Realism* akinukuliwa na Arvon 1973:85 anasema kuwa, "uhalisia wa kijamaa ni uhalisia wa wanadamu wanaobadilisha na kuujenga upya ulimwengu."

Katika maelezo haya anasisitiza umbuji una lengo la kuendeleza ukuaji wa vipawa muhimu ili kuhakikisha ushindi dhidi ya mazingira makali na kupambana na udhalimu wa aina yoyote. Mkangi aliweza kutumia hadithi za Mapacha, Mabavu, Matope na Ti miongoni mwa zingine kuonyesha mazingira makali na suluhu. Kwa upande mwingine, Gorky anaendelea kusema:

> ... jukumu la mwandishi ni kuona kuwa kazi zake za kiuandishi zinaenda sambamba na shughuli zote za kijamaa. Kwa kufanya hivo husaidia juhudi za wanajamii kupambana na ugandamizwaji wa kilimwengu. *(tafsiri yetu)*

Gorky anaona kuwa jamii ya wanadamu lazima ijaribu kupapatika katika juhudi zake ili iweze kuishi kama jamii moja yenye fanaka. Kwa sababu hali ya watu ina msingi yake katika historia, basi mwanafasihi hana budi kuzingatia historia ya jamii anayoizungumzia na kuonyesha mivutano ya kitabaka kama sehemu ya maisha. Mkangi aliweza kuonyesha hii mikinzano na mivutano katika matabaka yanayodhihirika kupitia kwa hadithi zilizo katika *Mafuta* na *Walenisi*. Pia alionyesha hali ya kizinduana kupitia kwa hadithi hizi.

Katika kuhitimisha utangulizi huu kuhusu uhalisia wa kijamaa, Plekhanov katika *Marxist Esthetics* (1973:12)"anasema "sanaa ni kioo cha hali halisi ya maisha katika jamii ... kazi yoyote ya sanaa ni kielelezo cha wakati huo".

Katika maelezo haya Plekhanov anatuonyesha kuwa kazi ya sanaa inajikita katika mahusiano ya wanajamii. Lenin (1905) akinukuliwa na Arvon, (1973:14) anasema:

> Fasihi hutekeleza jukumu la kijamaa, huwa ni kielelezo cha mapinduzi kwa kuamsha hisia, kukuza na kuhamasisha hisia za uhalisia wa kijamaa. *(tafsiri yetu)*

Maelezo haya ya Plekhanov na Lenin yanatoa muhtasari wa maudhui yaliyojikita katika hadithi za riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Kimani Njogu (1988:45) anasema hivi kuhusu uhalisia wa kijamaa:

> Fasihi yakinifu basi inachukuliwa kama kielelezo cha hali halisi ya jamii na haijitengi na maswala ya kijamaa. Licha ya kuzichangamsha nafsi za hadhira yake, fasihi yakinifu hujadili uhusiano wa watu katika shughuli zao za maisha kama vile siasa, uchumi, utamaduni na dini. Saikolojia itokanayo na maisha yao haina budi pia kueleweka. Mwanadamu huishi katika mazingira ya kiasili ... hayo humwathiri mwanadamu naye pia huyaathiri. Taathira hizo mara nyingi hujitokeza katika fasihi yenye uhalisia.

Kwa mujibu wa maelezo ya Kimani Njogu (1997) baadhi ya wataalamu walioishughulikia hoja hii ya nadharia ya uhalisia ni kama Basquez, (1973), Bisztray (1978), Ngugi wa Thiong'o (1981a, 1981b ) na wengineo.

Mbunda Msokile (1993:109) anasema kuwa uhalisia wa kijamaa ulianza rasmi wakati wa kipindi maalumu cha historia hasa baada ya mapinduzi ya kijamaa ya Urusi ya 1917. Arvon, (1973:84) anasema Gorky katika kazi zake *The Mother* (1906) na *The Enemies* (1906) ziliweka misingi madhubuti ya kwanza ya fasihi halisia. Unyama na mapambano baina ya matabaka yalionekana dhahiri shahiri. Arvon anaendelea kusema kuwa dhana ya Uhalisia wa Kijamaa iliibuliwa na Stalin katika mazungumzo yao na Gorky pamoja na Alexei Tolstoy mwaka wa 1932 katika mkutano wa waandishi. Hapo Stalin aliweka mihimili madhubuti ya kuongoza sanaa. Jambo ambalo utafiti huu umeliita 'wakarabati wa mioyo'. Hili ndilo lililokuwa chanzo cha kupatia uhalisia wa kijamaa, shabaha au fasili ya kisayansi. Katika kazi hizi *The Mother* na *The enemies* anaonyesha uhalisia wa kijamaa ambako mapambano baina ya matabaka yalikuwa yamefikia kilele. Katika misingi ya Uhalisia wa Kijamaa waandishi wanatazama nguvu za jana, leo, kesho na kazi hizo zinaweka nguvu za taifa. Kazi za Mkangi, *Mafuta* na *Walenisi* zinatazama jamii katika uhalisia huu kwa kutumia masimulizi ya 'hadithi katika hadithi' anazosimulia.

### 1.4.1 Mihimili ya Nadharia

Nadharia hii ina mihimili ifuatayo:

Owen, (1967:20) anasema kuwa, "... mapinduzi ya kuzinduana ndiyo msingi wa nadharia hii." Hapa ni kusema kwamba uhalisia wa kijamaa hujikita katika mapinduzi na kuamshana kwa sababu huipa fasihi jukumu la kuandaa jamii ili kujikomboa na kuanzisha jamii yenye usawa.

Pili, historia ya mwanadamu imeonyesha kuwepo kwa harakati na mapambano ya kitabaka. Harakati hizi zinaonyeshwa katika hadithi za Mafuta na Walenisi. Kuna mgao wa majukumu au kazi, na huo ndio huwa msingi wa kuundwa kwa matabaka katika jamii yaani tabaka la wafanyakazi, watawala na wazururaji. Haya matabaka yamedhihirishwa katika kazi za Mkangi kupitia kwa hadithi alizotoa. Kilele cha maendeleo haya huzua ubepari. Mali humilikiwa na kundi dogo la watu. Mali hii hupatikana kutokana na kujirundikia mali kwa kuhini na kunyonnya umma, hasa wafanyakazi.

Tatu, nadharia hii inasisitiza mapambano katika jamii. Hili hudhihirika katika matabaka yaliyoko katika jamii. Kama anavyosema Gorky (1973:85) anasema, "Jukumu la mwandishi ni kuona kwamba kazi zake za kiuandishi zinaenda sambamba na shughuli zote za jamii". Mwandishi hawezi kujitenga na matukio ya jamii yake kwa sababu ana majukumu katika jamii hiyo. Mwandishi katika kusawiri matukio ya kijamii huongozwa na itikadi na imani yake kuhusu jamii anayoizungumzia. Nadharia hii pia inaonyesha kuwa kazi ya kisanaa ni zao la jamii ambapo msanii hufasiri kazi

ya sanaa kutoka kwa lugha ya kisanaa hadi ile ya elimu-jamii ambayo humshirikisha na jamii yake kisaikolojia. Ngugi wa Thiong'o (1981:81) anasema,

> Jinsi mwandishi anavyochora uhalisia wa maisha huathiriwa na falsafa yake ya kimsingi kuhusu maumbile na mbinu yake ya kupeleleza maumbile na jamii hiyo. (tafsiri yetu)

Hapa Ngugi anasisitiza uhusiano baina ya uhalisia wa maisha na falsafa ya msanii. Hali kadhalika nadharia hii husisitiza kuwa fasihi ni amali ya jamii. Msanii ni mmojawapo wa wanajamii ambao wanahitajika kujenga na kuibadilisha jamii kupitia kwa sanaa. Nadharia hii pia huonyesha kuwa fasihi ni kielelezo cha jamii kama alivyosema Plekhanov (Tazama: Arvon 1973:12). Fasihi inafaa kumsaidia mwanadamu kujikomboa kutoka katika hali duni na ndipo Stalin katika Arvon, 1973:83) anaiita dhima hii ukarabati wa mioyo.

Nne, nadharia hii pia inatueleza kinagaubaga kuwa historia na siasa haviwezi kutenganishwa na fasihi. Fasihi nayo haiwezi kutenganishwa na masuala ya kiuchumi, kijamaa na kisiasa. Nadharia hii inashikilia kuwa chimbuko la fasihi ni harakati za maendeleo ya binadamu kihistoria. Fasihi hushughulikia jamii katika mikondo tofauti kwa jumla na pia huhusu mtu mmoja. Mambo yanayohusu jamii yanaweza kuwa mambo ya wakati uliopita, uliopo au maisha na mazingira ya kawaida. Kama tulivyoeleza hapo juu binadamu ndiye kiumbe wa pekee anayeweza kubuni na kufurahia fasihi. Kipawa cha kubuni na kuelezea hisia ndicho kinachompa binadamu mawazo ya aina tofauti. Binadamu pia amepewa kipawa cha lugha na

inafaa atumie lugha hii kuhamasisha jamii yake. Chambilecho Mbughuni (1978:12);

> Binadamu ni kiumbe chenye mamlaka ambacho kwa wema wa jamii hakistahili kukaa nyuma na kuona mambo yakichukua mwelekeo wa kiholelaholela, lazima aonyeshe nguvu na juhudi zake katika kukabiliana na uovu na kuung'oa ... binadamu ana uwezo fulani wa kusema juu ya hatima yake, anaweza kuhiari uzuri au ubaya, haki au dhuluma, na katika kufanya hivyo huwa anashiriki katika umbuji wa historia. *(tafsiri yetu)*

Tano, katika ujenzi na juhudi hizi zote hatima yake itakuwa kuleta mabadiliko katika jamii. Hili nalo pia limejitokeza kuwa mhimili wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Hapa tunaona sanaa ya uandishi lazima ihamasishe na kuzindua umma ili kuchochea mabadiliko, kama masimulizi ya hadithi katika hadithi za *Walenisi* na *Mafuta* zinavyoonyesha. Kwa mfano, hadithi ya mapacha au moto katika *Walenisi* au hadithi ya mkunazi na hadithi ya *Ti* katika *Mafuta.*

Hali kadhalika uhalisia wa kijamaa kwa maoni ya Arvon (1973:87), huacha umma na matumaini. Mtazamo wa nadharia hii hupinga ubepari na ubwanyenye na unajenga ujamaa na kumkomboa mfanyakazi ambaye anadhalilishwa na mfumo mbaya. Kwa mfano hadithi ya Mkunazi, hadithi ya Dzombo na hadithi ya Wachuna ni miongoni mwa zingine. Kazi za kisanaa zinazojikita katika nadharia hii ziwasilisha ukweli katika uhalisia wake kama alivyosema Kimani Njogu (1997) katika utangulizi wake.

Kwa muhtasari, uhalisia wa kijamaa huhitaji kudhihirishwa kwa mambo katika uhalisia wake. Pili kazi hii imejikita katika uhalisia wa kijamaa. Maudhui yaliyo katika hadithi zetu yamejikita katika misingi ya nadharia hii.

## 1.5 Yaliyoandikwa Kuhusu Swala la Utafiti

Baadhi ya maulama ambao maandishi yao yamejikita katika uhalisia wa kijamaa ni kama Al-min Mazrui, katika uhakiki aliotoa katika juzuu la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), juzuu 51/1 na 51/2 (1984) alihakiki kitabu cha Mohamed, S.A. (1980) *Dunia Mti Mkavu.* Hapa alionyesha matabaka tofauti yakiwakilishwa na ndugu wanne wanaoonyesha mfumo wa kijamaa na kiuchumi. Pia anatueleza kuwa tabaka la wafanyakazi linahitaji uongozi bora katika kukabiliana na unyanyaswaji na mazingira makali. Uhakiki wake unahusiana na masimulizi. Pia tamthilia yake, *Kilio cha Haki* (1981). Ngugi wa Thiong'o (1981) anaeleza jinsi ya kukabiliana na unyanyasaji wa dhuluma na istiimari. Katika maelezo yake pia anaonyesha jinsi ukoloni mamboleo umejikita. Cantalupo (1995) alihariri *Petals of Blood* (1977), na *Matigari* (1987) na kuonyesha jinsi Ngugi wa Thiong'o anavyozungumzia juu ya udhalilishaji wa wafanyakazi. Kathleen Greenfield katika Cantalupo, C. (1995:38) anatumia hadithi ya talanta kuonyesha jinsi waliopewa vipawa tofauti walivyovitumia ili kunyanyasa jamii. Hadithi hii ina msingi wake katika hadithi iliyotolewa na Yesu Kristo (Luka 19:11-26) kuhusu ugawaji wa vipawa katika Agano Jipya. Mwandishi anasema,

> Mfanyakazi aliyepewa shilingi laki moja alifukia zake chini kwa sababu pesa haziwezi kuongezeka bila kunyonya jasho la wafanyakazi.

Utafiti huu umechanganua na kuchunguza jinsi Mkangi alivyotumia 'hadithi katika hadithi' kutoa maudhui yake.

Wamitila katika Jarida la *Kiswahili Juzuu 61* (1998:83) ameonyesha jinsi kazi ya Mkangi, *Walenisi* (1995) imejikita katika mtiririko wa hadithi. Msanii huyu hakujadili

maudhui. Utafiti huu umeangalia maudhui haya. Katika *Mafuta* (1984) Mkangi alitumia hadithi kutoa maudhui yake. Maudhui katika riwaya zote yanafungamana na uhalisia wa kijamaa katika jamii ya msanii. Maxim Gorky (1906) alizungumzia juu ya dhuluma kupitia kwa kazi yake *The Mother* na *The Enemies*. Katika kazi zake *The Song of the Falcoln* na *Song of the Stormy Patrel* zinaonyesha wafanyakazi wakipinga mfumo wa ubepari. Riwaya hizi zinaeleza dhuluma na unyonyaji kupitia kwa masimulizi ya kawaida. Tofauti hapa ni kwamba Mkangi alieleza dhuluma kupitia kwa 'hadithi katika hadithi'. Hili ndilo jambo ambalo utafiti huu umejaribu kufuatilia katika riwaya hizi mbili. Kazi za waandishi wengine kama Mohamed Suleiman Mohamed *Nyota ya Rehema* (1976) Shafi Adam Shafi *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (1978), na *Kuli* (1979), Saidi Ahmed Mohamed *Asali chungu* (1980), *Utengano* (1980), *Sikate Tamaa* (1980) na *Kina cha Maisha* (1984:30) "Shairi la Haki yangu Tadai". Haya ni baadhi ya maandishi yanayojaribu kutoa mchango kuhusu ujenzi wa jamii mpya kupitia kwa masimulizi ya kawaida.

Mbughuni (1978) katika *TUKI Swahili Vol. 48/2 Septemba* anaonyesha jinsi masimulizi ya hadithi yanavyotumiwa katika kutoa maudhui. Anatoa mifano katika kazi za Shabaan Robert, *Kusadikika* (1951), *Kufikirika* (1961), *Siku ya Watenzi Wote* (1968) na *Adili na Nduguze* (1951). Hizi ni kazi za fasihi andishi zilizojengeka katika fasihi simulizi. Uhakiki wa Mbughuni unatoa motisha ya kutazama mwandishi mwingine ambaye ni Katama Mkangi kwa sababu hakuna msanii aliyezichambua hadithi katika misingi ya uhalisia wa kijamaa jinsi utafiti huu unavyodhihirisha kupitia kwa maandishi ya Mkangi.

## 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu umezingatia riwaya mbili tu za Mkangi, *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995), kusawiri na kuhakiki maudhui ya riwaya hizi mbili ambazo zinazungumza juu ya ugandamizwaji. Riwaya ya *Ukiwa* (1975) haikuchunguzwa kwa sababu maudhui yake yanahusiana na mapenzi. Jambo la pili ni kuwa njia ya masimulizi iliyotumiwa ni tofauti kabisa. Jambo la tatu na la mwisho ni kuwa uandishi wa *Ukiwa* ulitokea wakati mwandishi alikuwa anaendelea kukomaa na kubobea katika sanaa hii.

Kupitia kwa riwaya hizi, *Mafuta* na *Walenisi* utafiti huu umechanganua jinsi hadithi alizotoa mwandishi zimeweza kutoa maudhui. Pia kuchunguza umuhimu wa hadithi kama nyenzo ya kutolea maudhui.

Utafiti umechanganua mitindo ya 'hadithi katika hadithi' peke yake. Utafiti huu pia umechanganua maudhui yanayojitokeza katika hadithi hizo pekee.

Mtafiti aliwahoji wahakiki watatu tu ambao wametumia riwaya hizi katika mihadhara yao.

Nadharia ya uhalisia wa kijamaa ndiyo iliyotumiwa katika kuchanganua na kuhakiki hadithi hizi ili kupata maudhui. Ploti ya msanii huyu inaweza kuchukua nchi yake au nchi nyingine yoyote ya Kiafrika inayogandamizwa na Ukoloni mamboleo.

## 1.7 Njia ya Utafiti

Kwanza, utafiti huu umefanyika maktabani kwa kusoma riwaya mbili za Mkangi, *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995).

Pili, utafiti umechunguza jinsi mazingira ya mwandishi yameathiri kazi zake kwa kuzingatia nadharia hii ya uhalisia wa kijamaa. Ili kuyakinifu kazi yake, utafiti umechunguza maandishi ya wasanii kama Ngugi wa Thiong'o, Soyinka, Frantz

Fanon, Shabaan Robert, Al-Amin Mazrui, Mbughuni na Walter Rodney miongoni mwa wengine wanaojaribu kusawiri ukweli wa kijamaa kisiasa na kiuchumi katika jamii zao. Maandishi haya yamesaidia kuhakiki hadithi za mwandishi.

Tatu, mapitio ya vitabu, makala na machapisho ya majarida mengine yamesaidia katika kuhakiki maudhui. Jambo hili limegusia majilio ya wageni hasa katika karne ya kumi na tisa. Utafiti umefungamanisha mihimili ya nadharia hii na jinsi inavyoingiliana na maudhui katika riwaya hizi mbili ili kutambua ukweli unaojikita katika hadithi hizi. Fungamano hili limekuwa kigezo muhimu cha kusawiri hadithi hizi na maudhui yanayojikita ndani.

Nne, utafiti umechunguza makala yanayorejelea fasihi simulizi. Maandishi haya ya fasihi simulizi yamezingatia jinsi hadithi za kufurahisha zinavyoweza kutumiwa kama jazanda au nyenzo ili kutoa maudhui katika muktadha wa uhalisia wa kijamaa.

Kwa muhtasari utafiti huu umejikita maktabani na pia kuwahoji wasomi wahakiki watatu ili kuweka swala hili la utafiti wazi.

### 1.7.1 Kuchanganua Data

(i) Mahojiano baina ya wahakiki watatu waliohakiki maandishi ya riwaya za Kiswahili na mtafiti ili kupata maoni yao kuhusu riwaya hizi.

(ii) Data ya upili changishi iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutathmini mambo yaliyo muhimu kutokana na usomaji wa vitabu, majarida na magazeti.

(iii) Data iliyochanganuliwa imewasilishwa kupitia kwa maandishi ya nadharia yanayorejelea kazi zinazochanganuliwa.

(iv) Uchanganuzi wa yaliyomo (content analysis) umefanyika ili kutoa muundo unaofaa kwa utafiti huu. Mbinu ya ustahilifu (qualitative analysis) na ya kihistoria ndizo zimetumika.

### 1.7.2 Mpangilio wa sura za utafiti

1. Sura ya kwanza

    1.0 Utangulizi

    1.1 Swala la utafiti

    1.2 Lengo la tasnifu

    1.3 Sababu ya kuchagua mada

    1.4 Misingi ya nadharia

    1.4.1 Mihimili ya nadharia

    1.5 Yaliyoandikwa kuhusu swala la utafiti

    1.6 Upeo wa utafiti

    1.7 Njia za utafiti

    1.7.1 Uchanganuzi wa Data

2. Tanzu za fasihi simulizi na umuhimu wake katika riwaya hizi.

3. Mtindo wa Usimulizi katika Riwaya ya *Mafuta*.

    3.0 Uchanganuzi wa maudhui kwa kuainisha hadithi za *Mafuta*.

    3.1 Hitimisho

4. Mtindo wa Usimulizi katika Riwaya ya *Walenisi*

    4.0 Uchanganuzi wa maudhui kwa kuainisha hadithi za *Walenisi*.

    4.1 Mtindo wa usimulizi katika riwaya zote mbili.

5. Maathiriano ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

5.0 Mapendekezo

5.1 Hitimisho

5.2 Kiambatanisho A

5.3 Kiambatanisho B

## SURA YA 2

## 2.0 VIPERA VYA HADITHI NA UMUHIMU WA HADITHI KATIKA FASIHI SIMULIZI

### 2.01 Utangulizi

Hadithi ni mojawapo wa tanzu ya fasihi simulizi. Ili kutoa picha halisi ya hadithi, kwanza tumeangalia tanzu za fasihi simulizi kisha tumetilia mkazo vitanzu au vipera tofauti vya hadithi. Katika sura hii tumejadili hadithi kama chombo cha kutolea maudhui. Fasihi simulizi imekuwepo tangu jadi katika jamii zetu. Fasihi hii imesahaulika baada ya wageni kuleta maandishi. Hali kadhalika jamii zinaendelea kubadilika, nayo fasihi pia inabadilika. Kamera. D.W. katika Makala ya semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili, *Fasihi III* (2003:39) anasema;

> Urithi wetu wa jadi kwa hakika ni kisima chenye rutuba ya kutosheleza haja zetu zote za utunzi.

Fasihi simulizi ni mojawapo wa vipengele vya urithi huu. Urithi huu umeweza kupitishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya mdomo. Tanzu za fasihi simulizi ni ngano au hadithi, nyimbo au mashairi, methali na vitendawili. Haya ni kwa mujibu wa Al-Amin na Syambo (1992:12) na Wamitila (2003:254) wakisema kuna simulizi au hadithi, maigizo, ushairi, semi au tanzu bunifu. Makundi haya makubwa yana vijikundi vingine vidogo au vipera. Kutokana na urithi huu wa jadi unaweza kutoa hadithi zinazoweza kutumika katika ujenzi wa jamii mpya. Uritihi huu tumeweza kuupitisha kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya mdomo. Julius Nyerere akisisitiza umuhimu wa hadithi kama urithi wa jamii katika Kamaru D.W. (2003:40) anasema;

> Jifunzeni kwa wazee wenu na babu zenu hadithi, mashairi, na historia ya watu wetu maana mambo mengi sana hayo hayajaandikwa vitabuni na kama hamkuyajua basi yatapotea. Hadithi hizi ni sehemu ya urithi wetu. Ni lazima mzijue na kuwafundisha wengine pia wazijue, zisijesahaulika baada ya kizazi hata kizazi.

Maneno ya Nyerere yanasisitiza juu ya urithi wetu wa jadi. Urithi huu unapitishwa kutoka kizazi hadi kingine kwa njia ya mdomo kama anavyosema Matteru katika *Fasihi III* (2003:260);

> Fasihi simulizi ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo katika kuumbwa, kuwasilishwa na kusambazwa kwa wasikilizaji na watumiaji wake... ni aina ya sanaa itumiayo maneno katika mpangilio na maumbo mbalimbali kutoa dhana ama mawazo fulani.

Katika dondoo hili tunaona kuwa fasihi hii hutumia mdomo. Yaani inakusudiwa kufikia hadhira kwa njia ya mdomo (maneno) na pia masikio kwa kutoa dhana fulani. Maoni haya pia yametolewa na Al-Amin na Syambo (1992), na Wamitila (2003b).

Fasihi simulizi inaweza kugawanywa katika vitengo vinne muhimu. Hivi ni: hadithi, maigizo, ushairi na semi. Utafiti huu umezingatia hadithi kama kitengo mojawapo katika fasihi simulizi. Mtazamo uliochukuliwa ni kutazama hadithi kama chombo cha kutolea maudhui kama inavyodhihirika katika kazi za Mkangi, *Mafuta* na *Walenisi*. Kwa hivyo utafiti huu haukuchunguza tanzu zingine za fasihi simulizi.

## 2.1.2 VIPERA VYA HADITHI

Utanzu wa hadithi umesheheni vipera viwili vikubwa ambavyo ni:

(a) Hadithi za kubuni

Hadithi za kubuni huhusisha ngano, hadithi, mbazi, istiara, na soga. Katika kipera cha ngano, tuna vipera vingine kama hekaya, hurafa na ngano za mazimwi.

(b) Hadithi za kihistoria (*Misendu*)

Hizi huhusisha shajara, migani, tarihi na kumbukumbu. Utafiti huu umejikita katika aina hizi mbili za hadithi katika kutazama hadithi kama chombo cha kutolea maudhui. Mkangi katika riwaya zake *Mafuta* na *Walenisi* ametumia hadithi hizi kama nyenzo ya kutolea maudhui yake. Hadithi hizi zote hutolewa kwa njia ya masimulizi. Kiambatanisho (A) kinaonyesha utanzu wa hadithi na vipera vyake. (Tazama Kiambatanisho A) Vipera hivi ambavyo vimejikita katika utanzu wa hadithi vitakuwa vikijitokeza hapa na pale ili kutoa maudhui aliyokusudia mwandishi katika kazi yake.

## 2.1.3 UFAFANUZI WA UTANZU WA HADITHI

Hadithi ni mojawapo wa vipera vya fasihi simulizi vinavyotumia lugha ya mfululizo. Kipera hiki kilizuka baada ya nyimbo au ushairi. Mara nyingi hadithi husimuliwa jioni. Huu ni wakati ambako jamii huwa inapumzika baada ya kazi ya siku kutwa. Kuzuka kwa utanzu huu kunaonyesha jamii ilikuwa sasa imetulia na hii ndiyo iliyokuwa njia ya pekee ambayo ingetumiwa kuelezea dhana tofauti,

desturi, na amali mbalimbali za jamii kwa njia ya kinathari. Hadithi hizi zilikuwa mali bia, yaani zilikuwa mali ya jamii. Maelezo ya hadithi yametolewa na Senkoro (1982:75) anaposema;

> Hadithi fupi mara nyingi hujengeka juu ya tukio moja tu au sana sana matukio mawili, pia humzungukia mhusika mkuu mmoja na hujihusisha na mkondo mmoja wa kihisi, na kama ikiwa ni mikondo mingi aghalabu yote huelekezwa katika mmoja mkuu. Riwaya ina wingi wa yote hayo yaliyotajwa.

Katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi* kuna matukio ya hadithi tofauti yaliyojikita katika hadithi moja kuu. Hadithi hizi zina ujumla wa muungano wa matukio mbalimbali yajengayo tukio moja muhimu ambalo huelezwa kwa muda mfupi. Katika muda huo maudhui yaliyokusudiwa huwa yameshaelezwa. Mkangi ametumia hadithi tofauti katika msuko wake ili kutoa maudhui aliyodhamiria. Hadithi za Mkangi zimetumika kama nyenzo ya kutoa maudhui ya kisasa kama alivyosema Okpewho (1983:155) kuhusu mazungumzo ya jadi lakini anaeleza mambo ya kisasa. Pili, hadithi hizi zinatoa taharuki ili kumtia msomaji mshawasha na hamu ya kuendelea kusoma. Kwa upande mwingine Mbunda Msokile (1992:23) anaeleza kuwa:

> Hadithi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha ya nathari. Hadithi inaweza kuwa masimulizi ya kweli au ya kubuni. Sanaa ya hadithi ni kazi ya mtu yenye mwigo wa kiyakinifu ambao umefungamana na wakati, mazingira na mfumo wa jamii.... Hadithi kama kazi ya sanaa husawiri maisha ya jamii. Kwa msingi huu wa kusawiri, hadithi lazima ieleze tukio, mahali na hatimaye mbinu za kulieleza tukio hilo.

Maelezo ya Mbunda yanasadifu kueleza hadithi zinazopatikana katika *Mafuta* na *Walenisi*. Riwaya hizi zimetoa uyakinifu ambao umefungamana na wakati, mazingira na mfumo. Hadithi zilizo katika riwaya hizi zimesawiri maisha ya jamii katika kipindi cha wakati fulani. Matukio haya yanatokea katika nchi nyingi za bara la Afrika. Hadithi hizo vilevile zilikusudiwa kubeba maudhui tofauti. Matumizi ya tamathali za semi hutofautisha hadithi na mazungumzo ya kawaida na kuifanya hadithi kuwa sanaa inayoonyesha uhalisia wa maisha katika jamii ya mwandishi. Kazi za Mkangi zimechukuwa mwelekeo huu zikizingatia uhalisia wa kijamaa kwa kusawiri jamii anayoiandikia.

Hadithi huwa na kitangulizi cha kuteka hadhira. Mtambaji hukitumia kuihusisha hadhira yake. Kitangulizi kinaweza kuwa;

Mtambaji: Paukwa
Hadhira: Pakawa
Mtambaji: Paukwa
Hadhira: Pakawa

Mtambaji: Hapo zamani zake palikuwa na..."

AU

Mtambaji anatamba kwa kuanza;
Kaondokea chanjagaa
Kajenga nyumba kakaa
Mwanangu mwanasiti
Vijino kama chikichi
Nakujengea nyumba
Na vilango vya kupitia.

Hapo zama za zama za kale....
Wakati mwingine mtambaji huanza kwa;



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Mtambaji: Hadithi, hadithi,
Hadhira: Hadithi njoo!
Mtambaji: Hadithi, hadithi,
Hadhura: hadithi njoo!

Baada ya haya ndipo yeye huanza kusimulia hadithi yake. Kwa kusema "Hapo jadi palikuwa---".

Kitangulizi kinatumika katika hadithi kwa sababu kadha:

(a) Huwa ni njia ya kuteka na kuichangamsha hadhira yake.

(b) Huwa ni kama ishara ya utangulizi wa hadithi kama wasemavyo, "mwanzo wa ngoma ni lele". Hili ndilo lele katika 'ngoma' hii.

(c) Hiki kilikuwa kigezo cha kuweka mpaka baina ya ulimwengu wa hadithi na ulimwengu halisia.

(d) Kitangulizi hiki kilitumiwa ili kushirikisha hadhira katika hadithi na kuongeza uhai katika hadithi.

Hadithi zilikuwa na utangulizi, mwili na hitimisho kama anavyoonyesha Senkoro (1982:77). Jamii tofauti zilikuwa na utangulizi na hitimisho tofauti. Hitimisho iliashiria kumalizika kwa hadithi. Ikiwa kulikuwepo na jambo lingine basi, hapakuwa na budi lielezwe. Ikiwa kulikuwepo na mapumziko basi ilikuwa mbinu ya kuwapumzisha wasikilizaji ili kuwawezesha kutafakari juu ya maudhui yaliyotolewa. Mapumziko katika utambaji yaliweza kuitia hadhira taharuki. Katika riwaya ya *Walenisi* Mkangi ametoa hadithi zake moja kwa moja kwa sababu hizi zilikuwa hadithi alizozipata kupitia kwa utafiti katika maktaba ya Walenisi, kwa mfano hadithi ya "Moto", "Mapacha", "Mabavu, "Uchawi" na hadithi ya Wachuna. Pili hakuwa na hadhira isipokuwa familia ya wenyeji wake. Katika riwaya ya

*Mafuta* Mkangi ameonyesha mianzo tofauti lakini mianzo hii imechukuana na desturi za utambaji wa hadithi kwa mfano hadithi ya Gweni. Hadithi hii inaanza hivi;

> "Pia, Gweni akawa anaongea, hadithi hii inanikumbusha sana Mfalme aliyekwenda uchi.
> 'Ni ipi hiyo?" Mtoto mdogo mmoja akauliza kwa hamu.
> "Niwaambieni? Akawauliza.
> "Tuambieeee---" Wakajibu kwa hamu
> "Haya basi, hadithi yenyewe inasema hivi---"
> Na hapa kila mtu akawa masikio wazi".
> (*ukurasa 70)*

Kitangulizi cha hadithi hii kinalingana na vitangulizi ambavyo vimeelezwa hapo awali kama msingi wa kuanza hadithi ingawa mandhari yamebadilishwa. Hitimisho pia ziliweza kuchukua mtindo huu wa hadithi ingawa maneno ni tofauti.

Kuhusu wahusika katika hadithi, Wamitila (2003:40b) anaeleza;

> "Ngano ni hadithi za kimapokezi ambazo hutumia wahusika wa aina mbalimbali (wanyama, miti au watu) kusimulia kisa fulani chenye mafunzo. Neno ngano hutumiwa katika jamii zetu kwa maana pana kiasi kwamba aina nyingine ya simulizi za hadithi---zinaweza kujumuishwa kwenye kundi pana la ngano".

Vipera vya hadithi za kubuni ni hadithi za mazimwi, hadithi za kishujaa, hadithi za kiayari au hekaya, hurafa au hadithi zenye wahusika wanyama. Kwa mfano hadithi ya "Chui na Nyani" katika riwaya ya *Mafuta na* hadithi ya "popo" katika riwaya ya *Walenisi* na hadithi za kimafumbo (ambazo huchukua istiara, mbazi, na mchapo), vichimba kazi na soga. Riwaya za Mkangi zinachukua hadithi za kimafumbo na kwa kiasi kidogo hurafa. Tazama mifano iliyotolewa.

### 2.1.4 HADITHI ZA KIHISTORIA

Hiki ni kipera kingine cha hadithi ambacho huchukua masimulizi ya kihistoria. Vipera vya utanzu wa kihistoria ni tarihi, migani au visakale, visasili, kumbukumbu na shajara.

Tarihi hueleza matukio ya kihistoria yanayoweza kuwa ya kweli lakini yamefinyangwa kisanaa kwa kuongezea ubunifu ndani. Kwa mfano tamthilia ya Ebrahim Hussein *Kinjekitile* inadhihirisha jambo hili. Hadithi ya Wachuna, Moto na Wachawi ni matukio ya historia kwa sababu umilikaji wa mali ulizua mfumo wa kikabaila ambao pia ulizua ubwanyenye. Baada ya rasilimali kuwa nyingi basi ilibidi njia itafutwe, njia ilipatikana katika bara la Afrika. Nchi za Ulaya zilipokuja katika bara la Afrika ili kupata mahali pa kuweza kuuza bidhaa zao. Nchi hizi za Ulaya ziliweza kung'ang'ania sehemu mbalimbali katika bara Afrika. Kuondoa uhasama huu ilibidi bara Afrika ligawanye kupitia kwa mkataba wa Berlin, (Berlin Conference, 1884).

Magani au visakale ni matendo ya mashujaa. Hadithi hizi huchanganya chuku na matendo ya mashujaa katika historia. Kusudi la hadithi kama hizi ni kueleza visa na mikasa ya watu (mashuja) ambao pengine walikuwepo katika historia ya jamii. Watambaji huweza kusimulia hadithi za namna hii kwa njia tofauti ili kuonyesha shani ya shujaa huyo anayehusika. Hadithi hizi zinaeleweka kwa

muktadha wa Ushirikina wa watu, kwa mfano hadithi ya Lwanda Magere, au hadithi ya Fumo Liyongo.

Pia kuna pia visasili (au Tanye) ambavyo hueleza chanzo au asili ya mambo au matukio fulani yanayoweza kuwa ya kihistoria. Kwa mfano asili ya mauti au asili ya makabila fulani ya wabantu. Pia hueleza mitazamo ya mambo fulani katika jamii kwa mfano wasifu wa kimaumbile ambao mhusika anachukua; Hadithi ya Mfalme aliyeenda uchi katika riwaya ya *Mafuta*, na hadithi za "Moto", "Mchawi" na hadithi ya "Mabavu" ni visasili vinavyopatikana katika riwaya ya *Walenisi*. Kadiri jamii inavyopanuka ndivyo visasili vinapoibuka ili kujibu maswali ya, kwa namna gani, au kwa nini. Katika hadithi za kihistoria tuna kumbukumbu, ambazo huweza kusheheni tawasifu na wasifu. Hadithi ya Mama Fofi na hadithi ya Matope katika riwaya ya *Mafuta* zimejikita katika kipera hiki cha kumbukumbu. Hadithi ya "Maskini Jeuri" na tawasifu ya "Dzombo" katika riwaya ya *Walenisi* ni mifano mingine. Tawasifu ya Dzombo inatoa maelezo kuhusu Dzombo. Kwa upande mwingine tuna shajara. Hii huwa ni hifadhi ya matukio yanayotokea kila siku. Hifadhi hii ya matukio ndiyo hujenga historia ya jamii. Katika riwaya ya Walenisi, utafiti uliofanywa na Dzombo katika Maktaba Kuu ya *Walenisi* ni mfano wa shajara. Utafiti huu uliibua hadithi ya "Wachuna", "Mapacha", "Moto", "Uchawi" na "Mabavu".

Kwa muhtasari hadithi hizi ndizo zimeunda msingi wa suala letu la utafiti. Hadithi hizi zilibuniwa na Mkangi ili ziwe nyenzo ya kutolea maudhui yake.

### 2.1.5 UMUHIMU WA HADITHI

Sehemu hii imechunguza umuhimu wa hadithi kwa muktadha wa riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Kabla ya kuangalia umuhimu wa hadithi kwa kuzingatia riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi*, ni bora tuangalie maoni ya wasomi wa fasihi kuhusu umuhimu wa fasihi simulizi. Wamitila (2003:20 b) anasema;

> ... tunaweza kugawa wajibu wa fasihi simulizi kwenye majukumu yanayohusiana na burudani, elimu, ujitambuaji na ujijuaji, hali ya kuwa sehemu ya jamii na ukuzaji wa stadi za lugha.

Kwa mujibu wa Wamitila fasihi huburudisha huelimisha, hueleza chanzo cha mambo, hukuza lugha na huwa mali ya jamii.

Senkoro (1982:70-71) anasema;

> Lengo kuu la ngano ni kuadibu, kuielekeza jamii katika mstari unaokubaliana na amali zake. Ngano basi huadibu, huonya na hufunza. Hujaribu kujenga utubora, na wakati huo huo ngano – viini hujibu maswali ya "kwa nini" na 'Kwa namna gani?" katika kueleza mambo yaliyotokea. Pia historia ya jamii ilielezwa kwa kupitia katika ngano. Wakati huohuo, kwa sababu mojawapo ya kazi kuu za fasihi na sanaa kwa jumla ni kuburudisha na kuliwaza watu, ngano hali kadhalika zilitumiwa kutimiza lengo hilo--- zingine zimeandikwa kabisa kwa wa kutumia maelezo ya mtazamo mpya unayoshughulikia na kuyachambua mambo ya jamii yake.

> Mifano twaiona katika kazi za Ebrahimu Hussein za *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi.* Hadithi hizi zimetoa mwelekeo mpya ambao huenda leo hii ndio unaohitajiwa: Welekeo wa kuzipa tanzu mbalimbali sifa za fani asilia kubeba maudhui mapya yanayohusu masuala mbalimbali ya jamii za leo.

Utafiti huu umejadili umuhimu wa fasihi simulizi kwa mujibu wa maelezo haya ya wasomi kwa kuzingatia riwaya za *Mafuta* na *Walenisi.*

Jambo la kwanza ni kuwa hadithi za usimulizi zinazopatikana katika riwaya ya *Walenisi* zinajaribu kutumia ulinganuzi ili kueleza wema na ubaya. Katama Mkangi anatutolea sifa za Wachuna dhidi ya zile za *Walenisi,* na hadithi ya Mapacha, Chihenyo dhidi ya Madza. Kwa maelezo haya, hadithi hizi zimetumiwa kama chombo cha kuonyesha wema na uovu katika jamii. Jamii ya Dzombo imejaa uovu na ile ya *Walenisi* imejaa wema. Wamitila (2003-127) anasema; "--- Dzombo ni ishara ya vita dhidi ya uovu, anawakilisha wema. Kimsingi basi kinachohusika hapa basi ni vita dhidi ya wema na uovu". Kupitia kwa hadithi ya Mapacha yenye wahusika Medza na chihenyo na hadithi ya Walenisi na Wachuna, Mkangi ameonyesha kuwa hadithi zinaweza kutoa maudhui kwa njia ya ulinganuzi.

Jambo la pili ni kuwa hadithi zinakusudia kuburudisha hasa baada ya kazi ngumu ya kutwa. Hadithi hizi zilitambwa wakati wa jioni baada ya chajio. Hadithi zilizo katika riwaya ya *Mafuta,* hasa hadithi ya Gweni, Mbeyu, Jasho na Ti zilikusudiwa

kuburudisha. Hadithi hizi zilitambwa hadi watambaji na wasikilizaji wakasahau kuwa usiku wa manane ulikuwa umefika. Hadithi hizi, pia kwa kuzingatia maneno ya Senkoro yaliyotangulizwa hapo juu katika dondoo, zimechukua mwelekeo mpya. Licha ya kuwa chombo cha kuburudisha, zimetoa mwelekeo mpya unaozipa umbo jipya ambalo linatumia sifa na fani asilia kubeba maudhui mapya yanayohusu masuala ya jamii ya kisasa. Hadithi hizi zimekuwa nyenzo ya kutolea maudhui ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Mtindo huu mpya hautoi taharuki miongoni mwa vibaraka na wadhalimu wengine. Hadithi za Mkangi katika *Mafuta* zimezingatia fani hii mpya. Hadithi ya Mapacha katika riwaya ya *Walenisi* imezingatia mtindo huu pia.

Hadithi hizi kadiri zinavyokuwa vyombo vya kuburudisha, zinaibua hisia za ndani. Kwa mfano hadithi ya "Matope" katika riwaya ya *Mafuta* na hadithi ya "Mapacha" katika riwaya ya *Walenisi.* Katika kutilia mambo haya mkazo Gibbe na Mvungi (1987:8) wanasema;

> Fasihi simulizi ya siku hizi huwaelimisha watu kuhusu masuala ya kilimo, siasa, uchumi, uhusiano wa jamii, mapambano dhidi ya Walowezi--- inaelimisha kuhusu masuala ya kijadi, kitaifa na kimataifa--- masuala ya kitaifa ni kama vile sera kuhusu siasa--- Masuala ya kimataifa ni kupiga vita ukandamizaji unaoendeshwa na wageni.

Mawazo yaliyodondolewa hapo juu yanaonyeshwa kupitia kwa hadithi ya "Jasho" na hadithi ya "Mwenye Mkunazi" jinsi kuna mapambano dhidi ya ukandamizaji na sera mbaya ya siasa. Mapambano dhidi ya walowezi ndiyo yaliyoleta mabadiliko.

Hadithi hii pia inaonyesha kuwa shida za unyonyaji zinasababishwa na nini, ni akina nani ambao wanahusika na wako wapi. Haya ni masuala ya kisiasa na kiuchumi yanayotolewa na hadithi hizi. Siasa za vyama vingi hapa Kenya zimekuwa mapambano.

Jambo lingine ambalo Wamitila (2003:201) na Senkoro (1982:70-71) wametaja ni uhifadhi wa historia ya jamii. Hadithi ya Wachuna na kuzaliwa kwa *Walenisi* ni matukio ya kihistoria ambayo Dzombo aliweza kuyapata katika Maktaba Kuu ya Walenisi. Hadithi ya 'Moto', 'Mchawi' na 'Mabavu' ni hadithi zilizojikita katika matukio ya kihistoria hasa nyenzo za uzalishaji na chanzo cha ukabaila. Mtindo huu wa ukabaila ndio uliozua ubepari hadi ikabidi kulipuka kwa istiimari za wageni. Kutogawa kwa rasilimali kwa njia bora kulisababisha bidhaa kujaa bila kuwa na soko. Ikabidi wazitafutie soko katika nchi zingine. Historia ya wachuna ilionyesha jinsi walivyoigawa nchi ya *Walenisi* (ambayo ni taswira ya nchi zilizotawaliwa na wageni, miongoni likiwa bara la Afrika) imeelezwa kupitia kwa hadithi zilizotolewa. Hadithi ya "Mama Fofi" imejikita katika mambo ya ubepari na ubwanyenye. Katika kufanya biashara ya kuuza mbawa za kumbikumbi waliwapatia wafanyakazi pesa kidogo kama ujira ili wao waweze kupata faida kubwa. Al-Amin Mazrui (1981) katika kazi yake amelizungumzia suala hili. Huu ni unyonyaji na udhalilishaji wa wafanya kazi. Hadithi ya 'Mfalme aliyeenda uchi' katika riwaya ya *Mafuta* ni kisasili kinachoonya dhidi ya uongozi mbaya.

Hali kadhalika fasihi simulizi hukuza na kuendeleza lugha ya jamii husika. Kiwango hiki cha lugha huchukua methali, nahau, semi, jazanda, istiara, taswira, mafumbo, vitendawili na hadithi, matumizi ya majazi, kejeli, kinaya na tanakali za sauti. Matumizi haya yote ya lugha yanapatikana katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi,* kwa mfano methali hii, "Aliyeumwa na nyoka hata ung'ong'o humshtua", inapatikana katika riwaya ya *Walenisi* (ukurasa 60), na "Usimwone nyuki akitafuta asali pekee ukadhani yu peke yake", inapatikana katika riwaya ya *Mafuta* (ukurasa 80).

Hizi ni baadhi ya methali kutoka katika riwaya zote mbili. Wasomaji wa riwaya hizi wataweza kujumuika kwa kukuza msamiati na lugha yao kupitia kwa mbinu hizo za lugha.

Kutokana na maelezo ya Senkoro tuliyoyanukuu tumeona kuwa fasihi simulizi huadibu. Katama Mkangi ametumia mbinu ya ulinganuzi baina ya Wachuna na Walenisi, baina ya Medza na Chihenyo ili kuonyesha na kufundisha juu ya wema na uovu katika jamii. Ameonyesha kuwa baadhi ya wafanya kazi wa umma huwa hawazingatii kazi zao kupitia kwa hadithi ya "Mapacha". Katama Mkangi anatuhimiza kutenda wema na kuwajibika kulingana na mahitaji na maendeleo ya wakati uliopo na ujao. Hadithi zilizotambwa katika riwaya ya *Mafuta* wakati Ti alipokuwa ameenda kumwona Msati kuhusu kutiwa kizuizini kwa Mtue zimeonyesha namna hadithi zimeweza kutumiwa kama chombo cha kuleta

ushirikiano baina ya wanajamii. Wazo hili linaenda sambamba na maelezo kuwa hadithi za fasihi simulizi ni mali bia. Jambo kuu linalojitokeza hapa ni ushirikiano ambao misingi yake imejikita katika ujamaa. Chajio kilipoletwa walishirikiana (akina Ti, Msati, na Zuka miongoni mwa wengine) kula.

Hadithi ya "Maskini Jeuri" na "Matingasi" katika riwaya ya *Walenisi* ni kumbukumbu ya maisha. Wazo tunalojaribu kueleza hapa ni kuwa kumbukumbu huweza kuhifadhiwa kama hadithi. (Tazama vipera vya hadithi). Kwa upande mwingine, hadithi ya "Mama Fofi" katika riwaya ya *Mafuta* ni tawasifu. Hii inatoa historia na juhudi zake kabla hajanajisiwa na maji. Hali kadhalika maelezo ya Dzombo na sifa zake zinazopatikana katika riwaya ya *Walenisi* pia ni tawasifu. Hivi tawasifu inaweza kuhifadhiwa kupitia kwa hadithi.

Nyimbo zilizotumika katika riwaya zote zina umuhimu wake kama chombo cha kuburudisha. Mara nyingine nyimbo zilitumiwa kutilia uzito tukio lililotokea. Kwa mfano kuwasili kwa Dzombo katika vituo kadhaa alipokuwa ameenda kwa safari ya utu. Mara nyingine ni dalili ya ukaribisho mwema. Nyimbo za vijana wa Marika tofauti zilikuwa nyimbo za kuwasuta Wachuna na kuonyesha sifa zao mbaya. Pia nyimbo zinaweza kutumiwa ili kuleta uhai katika sherehe. Gibbe na Mvungi (1987:9) wanasema;

> Fasihi simulizi hutumika ili kuadhimisha matukio maalum. Nyimbo za fasihi simulizi hutumika kusherehekea jambo, kuitukuza au kuisifu siku ambayo ni muhimu.

Lakini, tungependa kuongeza kuwa wakati mwingine nyimbo hutumika kusuta na kukashifu.Mifano ya namna hii inapatikana katika riwaya ya *Walenisi*. Nyimbo mara nyingi hubeba hisia za malalamiko ya mtu mwenye simanzi au yule ambaye hakutosheka na jinsi mambo yalivyoenda. Katika riwaya ya *Walenisi* (ukurasa 96-97) vijana wanaimba wimbo wa siasa ili kuwatia moyo washirikiane katika miradi ya maendeleo kwa manufaa ya jamii nzima ya *Walenisi* bila kurudi nyuma. Nyimbo kama hizi zilikuwa hapa nchini Kenya tulipopata uhuru. Lakini zimemezwa na ufisadi na hazisikiki tena.

### 2.1.6 <u>Hitimisho</u>

Maelezo ambayo tumetoa yameonyesha kuwa hadithi au masimulizi ya fasihi simulizi yana majukumu muhimu katika jamii kwa sababu kama wasemavyo Obiechina (1967), na Mulokozi (2003:12), jamii nyingi za Waafrika bado hazijajua kusoma, hivi kwamba wataendelea kutumia fasihi simulizi kuliko fasihi andishi. Pili Obiechina anaeleza kuwa jamii nyingi za Waafrika zinaishi mashambani au vijijini ambako fasihi simulizi inatumika zaidi. Walio mijini wana mizizi yao huko vijijini kwa hivyo hawatajitenga na mawasiliano ya fasihi simulizi. Wanaporejea kule vijijini huwa miongoni mwa wanakijiji hivi kwamba wanatumia mazingira ya fasihi simulizi. Katika jamii nyingi za bara hili la Afrika wenyeji hawajajua kusoma na kuandika, bado wanategemea masimulizi. Jambo linalomfanya Matteru

(2003:33) katika makala yake yaliyo katika *Fasihi simulizi na uandishi wa Kiswahili katika Fasihi III kusema*;

> ... binadamu hawezi kupoteza hadhi ya usimulizi. Hili ni jambo la kuaminika. Hata kama maandishi yatatumika, hayawezi kusema kila kitu na kuenda sambamba na mabadiliko ya wakati kwa kasi ile ile. Tena hata watu wakihamia mjini wote, bado hali ya kuhitaji kutumia mdomo katika mawasiliano ya ana kwa ana itakuwepo. Na kwa vile usanii ni sehemu ya binadamu, usanii utakaotumia mdomo utaendelea kuwepo katika jamii hizo hata kama ni kwa sura tofauti na ile ya awali".

Wazo la Matteru linasisitiza tu umuhimu wa fasihi simulizi. Kitu kinachohitajika ni kutumia fasihi simulizi kifani ili kutoa maudhui ya kisasa. Kazi za Katama Mkangi (1984) na (1995), Shabaan Robert (1946) na (1951), na kazi ya Ebrahim Hussein (1976) ni mifano mwafaka kuonyesha matumizi ya fasihi simulizi katika 'nguo mpya'.

Mulokozi (2003:10) anasema kuwa, wakati wa kudai uhuru katika Tanganyika na Kenya, fasihi simulizi ilichukua nafasi muhimu. Wimbo wa vita wa Kinyamwezi wa karne ya kumi na tisa, "Oh-ho Chuma Chabela Mutwe" ukawa wimbo wa TANU, au '(KANU) yajenga nchi'.

Kama tulivyosema hapo awali nyimbo ni chombo muhimu cha kusisimua watu. Ushairi wa Margaret Dickinson (1972) kuhusu mapambano ya Angola, Mozambique na Guinea ni fasihi simulizi. Matumizi ya nyimbo katika vita vya Mau

Mau yalichangia katika mapambano dhidi ya walowezi na udhalimu wao. Nyimbo hizi ziliwatia mashujaa mshawasha na kusisimua ari za mapambano dhidi ya wadhalimu.

Wazo lingine kuhusu umuhimu wa fasihi simulizi ni kuwa inaweza kutumiwa kuleta maendeleo na mapinduzi. Hadithi katika kazi za Katama Mkangi zinachochea maendeleo na mapinduzi kwa sababu zinaburudisha pamoja na kutoa mafunzo. Pia fasihi simulizi imekuza na kudumisha fasihi andishi kwa sababu maudhui, lugha na fani tuzipatazo katika maandishi yana asili yake katika fasihi simulizi. Kazi za Katama Mkangi zimetumia fasihi simulizi kuweka uhai uandishi.

Kwa kufunga jamvi kuhusu umuhimu wa fasihi simulizi tunamnukuu Kamera (2003:41) katika makala yake katika *makala ya semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili III Fasihi* akimnukuu Mbonde kwa kusema;

> "Fasihi ni mali ya bia.
> Yahuisha, yadumisha;
> Yastaajabisha, yaburudisha;
> Yazoeza, yahekimisha, yaelimisha".

Malezo haya yanatoa muhtasari wa sifa za fasihi simulizi kwa mujibu wa vipengele vyake.

# SURA YA 3

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii utafiti huu umezichambua na kuziainisha hadithi zilizo katika *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995) kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Hadithi hizi zinakusudiwa kutoa maudhui fulani. Riwaya zote mbili zinahusiana kwa kiasi kikubwa na masuala ya kisiasa kama anavyosema Wamitila (2003:7),

> Riwaya zote mbili zinachunguza jinsi mfumo wa kisiasa unaodhibitiwa na tabaka la watu wachache unavyoweza kuathiri maisha ya waliotawaliwa kijamii, kiuchumi, kisiasa na hata kisaikolojia. Hizi ni riwaya ambazo zinaonyesha uovu uliopo katika tawala ambazo hazitilii maanani maslahi ya wengi ila zinaendeshwa na kigaro au kikundi cha wachache waliotawaliwa na unyama, ukatili na udhalimu mkubwa ... Hizi ni riwaya zinazoonyesha dhuluma, mateso na ukandamizaji kwa kina na jinsi jamii inavyopaswa kufanya juhudi za kuhakikisha kuwa udhalimu huo umeondoshwa katika jamii ili maisha yao yawe bora. Riwaya zote mbili ni riwaya za ukombozi, ni kielelezo cha jinsi jamii inavyoweza kujinasua kutoka kwa mfumo unaowakandamiza na kuwadhalilisha wengi.

Maelezo haya ya Wamitila yanatoa muhtasari wa ploti ya 'hadithi katika hadithi' zinazopatikana katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Pili, ingawa baadhi ya hadithi hizi ni visasili zimejikita katika uhalisia wa kijamii. Hadithi hizi zinazomulika masuala ya kijamaa, hadithi za kuzindua jamii kwa kuonyesha dhuluma walizotendewa wanajamii. Kwa hivyo zisichukuliwe tu kama hadithi zilizotambwa hapo kale ili kujumuisha na kupoteza wakati baada ya kazi ya mchana kutwa. Hadithi hizi zinazungumzia masuala ya utawala, udhalimu, umilikaji wa nyenzo za uzalishaji na kutogawanywa kwa mali ya asili kwa njia

iliyo sawa. Hadithi hizi zinatoa harakati za mapinduzi kwa kuonyesha migongano iliyopo baina ya matabaka yanayokinzana. Kusudi la hadithi hizi ni kufunza, kuzindua na kutoa suluhisho kwa matatizo ya kijamii, kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa mwanadamu anahitajika kuishi kwa furaha bila vikwazo vya aina yoyote na kupata mahitaji yake kama asemavyo Senkoro (1987:66);

> ... Kuumba mtu aliyekamilika kabisa, mtu anayepata mahitaji yake yote ya lazima ya kimwili na kiroho. Mtu asiyenyonya wala asiyenyonywa na mwingine.

Kwa misingi hii ya uhalisia wa kijamaa, mwandishi anasimulia 'hadithi katika hadithi' kama nyenzo ya kuelezea na kutetea maudhui yake ya uhalisia wa kijamaa. Kupitia kwa hadithi hizi Mkangi alitetea kuwepo kwa mabadiliko katika serikali na utawala, ambao ungeunga mkono wakulima au tabaka la wachochole dhidi ya ubepari, umwinyi na ubwanyenye kwa kuwainua kwa hali na mali. Kwa mfano tabaka la wazururaji lingepewa kitu cha kufanya, kama kazi. Hili tabaka lingeshirikishwa katika uzalishaji mali. Aliona kuwa hili linaweza kufanyika tu ikiwa adui atatambuliwa, na wanaodhalilishwa na kudhulumiwa au kuteswa waungane pamoja ili kung'oa uovu. Ikiwa juhudi hizi hazitafanyika kwa njia inayofaa, hasa kwa kukosa viongozi wa kuongoza mapinduzi haya basi maafa yatatokea. Wadhalimu watapata nafasi ya kuondoa wapinzani wao. Katika riwaya ya *Mafuta,* Mtue na Matope walikuwa mfano. Hawa ni wahusika waliotengwa na kuzuiliwa kwa sababu walichochea mabadiliko. Mtue alimwonea Matope huruma, ambaye alishtakiwa kwa kosa la kumwosha mteule kwa maji. Katika serikali nyingi tofauti za Kiafrika washtumiwa wengi waliwekwa kizuizini au

kuuawa. Mkangi alionelea kuwa hakutakuwa na hadhi na usawa kwa kizazi cha mwanadamu ikiwa uchumi na nyenzo za uzalishaji mali zitamilikiwa na watu wachache. Haijalishi kama hawa wachache ni wageni au wenyeji. Jambo muhimu ni kuwa na mgawano sawa wa rasilimali za nchi. Haya ameyaonyesha kupitia kwa hadithi za *Walenisi* na *Mafuta*.

## 3.1.0 <u>RIWAYA YA MAFUTA</u>

Hadithi kadha zimetumiwa katika riwaya hii. Riwaya hii ina hadithi zifuatazo.

(i) Hadithi ya mwenye mkunazi.

(ii) Hadithi ya Mama Fofi.

(iii) Hadithi ya Matope.

(iv) Hadithi ya Mbeyu.

(v) Hadithi ya Gweni.

(vi) Hadithi ya Jasho.

(vii) Hadithi ya Ti.

(viii) Hadithi ya Mtue.

### 3.1.1 Hadithi ya Mwenye Mkunazi

Hii ndiyo hadithi iliyochochea hadithi zingine katika riwaya ya *Mafuta*. Hadithi yenyewe yahusu mtu mmoja aliyemiliki mkunazi. Hadithi hii ilitoa mfano wa baadhi ya mapebari katika jamii waliomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Zuka, Jali na Kazamoyo ni vijana ambao hawakuwa na lolote wala chochote. Waliweza



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kucheza kamari kwa kutumia vizibo vya soda. Hawa vijana wangeparaga mkunazi wakati mwenyewe alipokuwa akikoroma na kutunda kunazi ili aliyekuwa na deni angeweza kulipa kwa kutumia kunazi. Ikiwa mdaiwa alikuwa na deni kubwa basi ingembidi amrushie Mdai kiashi kingi cha kunazi. Walipokuwa wanacheza ile kamari, vijana hawa walikuwa wanatoa ulinzi kwa kunazi zilizowekwa hapo chini ya mkunazi kwa mafungu. Wakati huo mwenyewe alikuwa analala. Lakini wakati mwingine wangeliweza kuchukua kunazi zilizotundwa na kuzila halafu wangeparaga mti wakati mwenyewe anakoroma na wangezirudisha. Mwenye mkunazi alikuwa bepari aliyeweza kuwalipa wafanyi kazi wake (hawa vijana) kwa kuwapa kunazi. Ujira aliowapatia ndio huo. Aliwadhalilisha na kuudumisha ubinadamu wao kwa manufaa yake. Yeye kama mwajiri aliwanyonya na kujitajirisha.

Hata hivyo Jali, Kazamoyo na Zuka walikuwa wakiiba kunazi zake. Hivyo ingeonekana kwamba hangeweza kuziuza lakini mafungu bado yapo. Vijana walikuwa wanakula kunazi na kurejesha wakati wanapouparaga mkunazi. Bahili mwenye mkunazi alishangazwa kwa nini kunazi zake hazinunuliwi, ilhali watu wanakula kunazi. Siku moja bahili huyu alihiari kufanya mtengo wa kuwanasa wanaoiba kunazi zake. Alijifanya analala na kukoroma, kumbe alitaka kujua yaliyokuwa yakitendeka wakati alipokuwa akilala. Hapo ndipo Jali alipoinama na kuokota kunazi moja huko akijidai alitaka kuonja. Lakini akijua wakati atakapoparaga mti atarudisha pale zingine. Punde tu alipokuwa tayari kuitia

mdomoni, ndipo mwenye kunazi alichuchumia kwa ghafla na kumnasa mkono. Alipomshika mkono alisema "Leo mwizi nimekushika". Jali alijitetea lakini mwenye mkunazi na kunazi alikuwa amehiari kumwangamiza. Alizidi kusema;

> Huu sio wizi basi! Wewe u mwizi, u mwizi, u mwizi!!! Mwenye kunazi akawa anasisitiza kwa kupaaza sauti. Watu kusikia mwizi wakaanza kusogelea pale mkunazini.
> (*ukurasa 4*)

Jali aliweza kujinusuru kwa kuchopoka vya ajabu kama swara! Jali alifukuzwa na umati wa wasio na la kufanya, malofa au wazururuaji. Umati huu ulimwandama na hukumu ya kifo ikiwa mwao machoni. Msimulizi anasema,

> Malofa hawa, hawakuwa na la mwanzo wala la mwisho maishani mwao. Kwa kutojua wezi halisi ni akina nani, na kukosa lengo halisi mwao maishani, chochote kile kilichotokea cha kuwafanya wao kuwa na la kufanya – kama vile kufukuza aliyedhaniwa kuwa ni mwizi – kuliwa furahisha sana. Maskini hawakufahamu methali ya weka mwizi ushike mwizi! ...
> (*ukurasa 5*)

Hili ni kundi la wazururaji wasiokuwa na kitu. Kundi hili linaweza kuunga yeyote mkono kwa sababu halina cha kufanya. Katika hadithi ya mkunazi tunapata maudhui yafuatayo:

Hali ya ubepari sio ya wageni peke yao. Lakini kuna wenyeji waliojikita katika ngazi za utawala wanaomiliki mashamba makubwa au nyenzo za uzalishaji mali ambao wanawanyanyasa wafanya kazi na wachochole. Nguvu za wafanya kazi zinanyonywa. Al-Amin Mazrui (1981), ameonyesha kuwa mabepari huwalipa wafanya kazi wao mishahara duni, kuna mazingira mabaya ya kufanya kazi na

masaa mengi ya kufanya kazi. Mabepari wanaona faida peke yake. Ebrahim Hussein (1973) ameonyesha jinsi ubepari ulivyojikita baada ya mkoloni kuondoka. Huu ndio ukoloni mamboleo. Kupitia kwa mbinu hizi jamii huwa inadhalilishwa na watawala ambao wanajilimbikizia mali. Pili, yule mwenye mkunazi alitaka kuhamisha harakati dhidi yake na kupeleka kwingine kwa kuonyesha kuwa Jali alikuwa mwizi. Kwa kufanya hivyo juhudi za malofa na wachochole kumwuliza kwa nini yeye pekee ndiye anayemiliki mkunazi na wengine hawana zingedidimia. Hawa malofa hawangemwibia tena na pia hata akipoteza mafungu machache atakuwa amejihami vilivyo dhidi ya malofa hawa. Msimulizi anasema,

> Hali mayowe ya 'mwizi huyoo' yalikuwa yangali yakimjia, yule mwenye mkunazi alisimama pale shinani na tabasamu usoni akijua kuwa vita vya wakosa kunazi havikuelekezwa kwake. Kwamba mafungu yake ya kunazi yalikuwa hayako tena baada ya umati kuondoka, havikumuudhi sana akijua kuwa hiyo ilikuwa gharama ndogo kulipa ili kuzuia malofa kufichua njama hii... alicheka kindanindani. (*ukurasa 5*)

Hadithi ya mkunazi inatuacha na swala moja kuu, mbona mkunazi unamilikiwa na mtu mmoja na wengine wengi hawana chochote. Pili, kule kusinzia kwa mwenye mkunazi na kuacha vijana wanaocheza kamari kwa kutumia vizibo vya soda badala ya pesa kumlindia kunazi zake kunaonyesha ubepari kwa upande mmoja na ufukara kwa upande mwingine. Tabaka la wazururaji halina chochote wala lolote. Hili ni tabaka la malofa. Tabaka hili linaweza kuunga yeyote mkono kwa sababu halina msimamo au kitu ambacho linafanya. Tabaka hili la wazururaji linaona kuwa limetengwa katika masilahi ya kijamii, kiuchumi na

kisiasa. Tabaka hili liko radhi kufanya lolote ili lisionekane ndilo linalokandamizwa.

Kusudi la mwandishi ni kutaka kujenga watu wenye furaha na amani. Watu wenye nia ya kuubadilisha ulimwengu kwa kuondoa matabaka na kuujenga upya ulimwengu ili uwe pahali pazuri pa mwanadamu kuishi. Hadithi hii ya mkunazi inashutumu upebari. Zuka anasema,

> Ni kwa kivipi ni yeye tu ndiye mwenye mkunazi?' ... Inakuwaje ni yeye tu aruhusiye zitundwe, azipangaye mafungu, ayapaye bei ...? Ni yeye ... kila kitu ni yeye ! Twendeni basi tukamwulize haya maswali kabla ya kumsomea ... Njiani walijikuta hawako peke yao...
> (*ukurasa 92*)

Jambo linajitokeza hapa ni harakati dhidi ya ubepari na unyonyaji. Pili kuna mgawanyiko wa jamii katika matabaka. Tabaka la juu linalowakilishwa na mwenye mkunazi, na tabaka la chini. Tabaka la chini lina matabaka mawili, hawa ni malofa na tabaka la wachochole ambao wanacheza kamari kwa kutumia vizibo vya soda badala ya kutumia pesa. Pia kuna tabaka la wasomi, hawa ndiwo waliosoma maandishi yaliyoachwa nyuma na Jali, mwanamume ambaye anatufunulia sura ya jamii hii kupitia kwa maandishi yake. Mkunazi hapa unawakilisha njia za kiuchumi. Mwenye mkunazi anawakilisha ubwanyenye na ubepari kwa upande mmoja kwa sababu yeye hulala tu na kuchuma kutoka kwa mkunazi. Umilikaji wa njia za uzalishaji mali umesababisha ukosefu wa kazi, wizi, uzuuraji na kudunishwa kwa maisha. Mabepari wanaabudu pesa kupitia kwa njia

ya unyonyaji. Tabaka la wazururaji ni tabaka hatari. Al-Amin Mazrui katika *Kiswahili* juzuu 51/1 & 52/2 (1984) anasema,

> ... tabaka hili ni hatari lililojaa fujo na hung'amua fursa inayojitokeza, na kwa jinsi fulani wafuasi wake wanaweza kuwa wahalifu na hutumiwa kwa jinsi ya mambo ilivyo (status quo) kupinga maslahi ya wafanyakazi na wachochole wanaogandamizwa. ...
> (*ukurasa 203*)

Wagandamizaji hapa ni mabepari. Tabaka la malofa linapewa chochote kwa mfano pesa, ili kuunga mkono tabaka la wagandamizaji. Hapa nchini Kenya tabaka hili huwa mara nyingi linatumiwa na wanasiasa wanaowania viti vya ubunge kushurutisha na kutisha wapigaji kura. Wakati mwingine wanakodishwa kwenda kufanya fujo mahali fulani ambapo bepari anataka ili huyo bepari anufaike. Katika misingi ya uhalisia wa kijamaa Zuka na Kazamoyo wanahitaji usawazishaji na ugawaji sawa wa mali ya asili na kupinga ukiritimba. Hili ndilo linalofanya kuulizwa kwa maswali waliyoulizwa. Katika kutaka haya yafanyike wameweza kuungwa mkono na wengine waliokuwa wananyanyaswa na kudhalilishwa. Pili, jambo la uongozi linajitokeza hapa. Lazima tuwe na uongozi madhubuti; wale wanaoweza kuongoza harakati hizi. Kwa mujibu wa hadithi ya mkunazi, viongozi wa harakati ni wasomi kama methali inavyosema, "mtambua ndwele ndiye mtibu ndwele". Kazamoyo na Zuka ndio walioweza kusoma makaratasi ya hadithi yaliyoachwa nyuma na Jali. Mwenye mkunazi hakujua kusoma na hakuona faida ya makaratasi yaliyoachwa. Hadithi hii inawakilisha uovu unaotendewa kina yakhe na mwenye mkunazi. Mwenye mkunazi anawakilisha wote walio na mali. Akina Mama Shibe, Dubwana, Dubwasha,

Bwagu na Bwaguzi ni vielelezo vya unyonyaji ukandamizaji na udhalimu uliojikita katika jamii. Juhudi za wanaotaka kujikomboa huzimwa, kwa mfano Mama Fofi na Mtue.

### 3.1.2 Hadithi ya Mama Fofi

**(Ubwanyenye na Upebari)**

Hapa ni mahakamani ambako Mama Fofi analalamika jinsi alivyonyimwa uteule tonge likiwa mdomoni. Kunyimwa uteule tonge likiwa mdomoni inadhihirisha ubwanyenye na ubepari uliokita mizizi katika nchi nyingi za Kiafrika na kuzua matabaka. Ubwanyenye na ubepari huu ulitokana na kunyonywa na kudhalilishwa kwa wafanya kazi. Mabadiliko katika jamii yaliyoletwa na wanaharakati kama Ti, Mtue, Matope na wengine yaliweza kuukomesha (Ubwanyenye na ubepari) upesi baada ya wanajamii kugundua kuwa walikuwa wakinyonywa na kundi la wachache. Wakati njama zake zilizimwa kwa upesi ndipo Mama Fofi alihiari kuleta mashtaka yake mbele ya mahakama ili mahakama imsaidie kuendeleza kudhalilisha wafanya kazi. Wakati uo huo mahakama zilikuwa zimepoteza hadhi ya kudumisha Haki, na kuwa chombo cha ukandamizaji. Juhudi za Mama Fofi za kutumia wengine kama ngazi ili afikie kilele cha ufanisi kwa kuwanyonya wachochole zilizimwa. Hapo ndipo anasema

> "... Na sasa yaonekana, hata hiyo kudura
> yake sitaweza kuitekeleza kwani maji
> yameninajisi ... Niende wapi? ...
> (*ukurasa 32*)

Kwa mujibu wa msimulizi, kitanda kiliwakilisha mbinu za ujanja zilizotumiwa na wakandamizaji ili kujidumisha katika ngazi za utawala. Kuwa mteule ni utabaka. Huko ndiko kukilalia kitanda. Msimulizi anaeleza kuwa, kukilalia kitanda ni uongo ambao umekuwa ukweli kwa sababu hakuna yeyote ambaye angelitaka kueleza upumbavu wake. Huu uongo ndio ulidumisha maslahi ya watawala. Msimulizi kwa kutumia mhusika Mtue anaeleza,

> "... Na sasa tembea mpaka ufike chini ya kivuli cha kitanda." ... lala kifudifudi, ... sasa lala kichalichali ... fanya kinyume cha ulivyofanya sasa hivi ... na sasa tembea mpaka ufike ule mpaka ulio mbele yako ... Geuka na urudi. Alipitia tena chini ya kitanda lakini juu ya kivuli chake na alikuwa yuko karibu kuingia ndani waliposema, "Hebu simama ... Sasa tupa macho juu. Kufanya hivyo akaona maandishi yakisema: "KITANDA UMEKILALIA, NA KARIBU UTEULENI." Lakini sikukilalia! Ni mavumbi ya kivuli chake. Hapo ni kweli. Lakini tuambie ni mteule gani angetaka kukubali upumbavu wake ...? Na ni kwa sababu hii, aondokapo huenda akitangaza kwamba sasa yeye ni mteule kwa kuwa amekilalia! Na usisahau kitendo hiki ni nia ya wengi ... Ukweli ni kwamba amefanywa mpumbavu, hapo hatakubali na ataficha. Kwa hivyo ataeneza uongo. Na huo ndio ambao mpaka wa leo ndio umekuwa ukweli, ... Na pia usisahau ni uwongo huu ndio udumishao masilahi yao!"
>
> (*ukurasa 84-85*)

Uongo huu ndio unaotumiwa na viongozi walafi, wakatili na wenye kukandamiza jamii ili waweze kujistiri zaidi katika utawala. Walio katika hadhi za utawala wangetumia kila njia ili kudumisha mamlaka yao juu ya watawaliwa. Mafuta na kitanda vinawasilisha falsafa ya uongo iliyotumiwa kuendeleza dhuluma. Mama Fofi alieleza jinsi bwana yake alizaliwa katika mazingira ya ufukara. Anasema,

> Maisha siyo yake tu – lakini hata kwa jamii yake yote, toka jadi yao, walikuwa watu hohehahe. Ukame huu ulionekana ukienea jamii nzima na kurithika kama ufalme!
> (*ukurasa 26*)

Wazo hili la mama Fofi ni jinsi walivyoishi katika ulitima. Juhudi za Sifa mumewe Fofi ziliambulia patupu. Sifa alitaka kuepuka ile hali ya kuzaliwa katika tabaka la chini na kufia katika tabaka hilo. Hata jamii nzima ilikuwa katika ulitima ulioriithishwa kutoka familia moja hadi nyingine. Hawakuwa na jinsi wangeliweza kujitoa katika ulitima huu. Mama Fofi na mumewe walifanya jitihada katika kazi yao. Mwandishi anaonyesha matabaka kwa kusema,

> ... wako wale waliobahatika na kupewa vichuguu ambamo mchwa wenyewe walizaliana. Wao ilikuwa ni kulalia nundu tu basi. Pia kulikuwa na wale ambao walipewa kandarasi ya kukamata kumbikumbi na baada ya kuondolewa mbawa zao. Hawa chao kilikuwa kidari. Nyama za mbavu zikawa zetu. Sisi tulipewa kandarasi ya kuzoa mbawa na kuziuza.
> (*ukurasa 30-31*)

Kazi hii ilikuwa ngumu kwani mzoaji alihitajika kupigana na kudhibiti maumbile na mazingira ili apate chochote. Katika kufanya kazi hii walipambana na vikwazo kama ndege, upepo unaopeperusha mbawa hizi na kuzitawanya kila pahali. Mvua na matope viliweza kuzorotesha kazi hii. Wazo hapa ni kuwa mwanadamu lazima apambane na mazingira magumu ili aweze kuyathibiti. Lakini huwa ni vigumu wakati ambapo wanadamu wengine huwa vikwamizo. Kwa mfano wanapomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Ngara 1985:17 akimnukuu Gorky anasema,

> ... Uhalisia wa kijamaa unashikilia kuwa maisha ni matendo, amali na ubunifu ambao madhumuni yake si

> kuwa kizuizi kwa maendeleo na bidii za mwanadamu za kumletea ushindi dhidi ya nguvu za asili ... furaha ya mwadamu kuishi katika dunia hii ni kutaka kuitengeneza kuwa mahali pazuri ambapo binadamu anaweza kuishi akiwa kama jamii moja.
>
> (*tafsiri yetu*)

Uhalisia wa kijamaa umedhamiria na kuangaza mbele kwa ujenzi wa jamii yenye furaha na mafanikio. Mama Fofi alileta mashtaka yake kwa sababu bidii zao zilitumbukia nyongo. Mwandishi anaonyesha juhudi zao na uhasama wa mahakama. Katika kueleza hadithi yake anaonyesha mabadiliko katika jamii kutoka kwa ubwanyenye hadi kwa ubepari. Mama Fofi alitaka kuingia katika hali hii (ubepari), kwani wao waliweza kupata faida nyingi kutoka kwa kazi yao. Karl Marx akinukuliwa na Huberman (1968:85) anasema;

> Mabepari hawaoni kitu kingine ila faida. Katika kutaka kutekeleza shabaha hii wao huwalipa wafanyakazi pesa kidogo ... wakati huo mabepari hutaka kujilimbikizia mtaji.

Kwa maoni ya mwandishi Mama Fofi na bwanake Sifa walikuwa mabepari baada ya kuishi katika ulitima. Licha ya kuanza biashara ya kuuza kumbikumbi wenyewe, kulikuwa na matatizo kutoka kwa ndege na kumbikumbi wenyewe kupotea. Bidii yake ilifanya ajinunulie kichuguu chake mwenyewe. Kifo cha Sifa kilisababishwa na mashindano ya kibiashara baina ya mabepari. Kezilahabi (1974:1) katika shairi lake *Jinamizi* anasema,

> ... Samaki ambaye, kupata hewa,
> Aliinua kichwa chake juu ya maji
> Utawala wa Chuma ulimtoboa fuvu
> La kichwa na kutupwa mtubwini.
> Halafu nilifikiria Afrika
> Na siasa kwa ujumla.

Lakini mara mamba kwa maelfu
Mtumbwi waliukimbilia kwa fujo,
Mtumbwi kupasuka wakatatuliwa
Vipande vipande
Halafu samaki wote waliinua
Vichwa vyao juu ya maji
Na pamoja wakaimba wimbo wa Uhuru.

Maelezo haya ya Kezilahabi yanatuonyesha kuwa kifo cha bwana Safi kilisababishwa na mashindano. Punde katika hatima ya riwaya hii tutaona wanajamii wakiimba wimbo wa maji kuonyesha ushindi wao dhidi ya dhuluma. Mama Fofi analilia haki itendeke ili aweze kupata haki yake. Lakini ukweli ni kuwa haikuwa haki bali alikuwa amenyonya wafanya kazi waliomsaidia katika kazi yake. Pili faida iliyopatikana ilikuwa mali yake binafsi. Jambo hili la kutaka haki kwa kula jasho la wengine ndilo mwandishi anapinga kupitia kwa hadithi hii. Huu uongo wa maji kuwa mafuta na kitanda kukilalia ulikuwa umefika kikomo, kama wasemavyo wambao wamba, 'unaweza kuwadanganya watu lakini sio wakati wote.' Mama Fofi hakupata lolote kutoka kwa mahakama. Wakati kulitokea mshindo wa "Maji Tu!" Maji Tu!" ndipo Mama Fofi alijua kuwa ukweli ukijidhihirisha uongo hujitenga.

Hadithi hii inatuonyesha dhuluma na unyonyaji wa walio wachache. Malalamishi yalipuuzwa kwa sababu wateule wachache wanataka kudumisha unyanyasaji na utabaka wao. Kwa upande mwingine Mama Fofi naye alikuwa akiendeleza ubwanyenye na ubepari. Baraza la mahakama liko kudumisha unyonyaji na uongo wa watawala.

### 3.1.3 Hadithi ya Matope

**(Dhuluma na Ukatili)**

Matope ni raia mmoja aliyeishi katika kidimbwi cha matope. Ametumiwa kuonyesha uhasama ulio katika mahakama. Pili, alituhumiwa kuwaosha wateule kwa maji. Hii ni kama njama ya kuwaondoa kisirisiri walio katika uteule. Hili hukashifiwa na tawala za mabavu. Matope alihiari kunyamaza mahakamani kwa sababu alijua kuwa haki huwa hazitendeki hapo. Hali ya Matope ilikuwa mbaya. Msimulizi anasema,

> Kuingia kwake kulileta mshtuko mahakamani. Bila yeye kujua, alikuwa amewafanya wengi waliokuwepo kushikwa na ndwele tofautitofauti. Kulikuwa na wale ambao kule kumwona tu, walianza kunyamba tu ovyoovyo. Wako wale ambao matumbo yao yaliwageuka kwa ghafla na kushikwa na haja ya kuendesha papo hapo, mara tu walipomkata macho. (*ukurasa 33*)

Mahakama kanuni yake ni kutunza haki na kulinda washtakiwa. Lakini hali ya mahabusu huyu ilionyesha udhalilishaji wa hadhi ya kibinadamu. Hata waliohudhuria mahakama walishikwa na kiwewe. Mshtakiwa alikuwa hana chochote wala lolote ila matope. Waliokuja kuhudhuria mahakama walistaajabu juu ya masaibu ya Matope. Waliweza kulipuka kwa ghafula kama volkano kwa moyowe ya hasira na ya hofu wakisema, "Twambiee!! Twambiee ...? Twambiee ...? (*ukurasa 35*)

Baada ya kuulizwa aeleze shida yake, Matope alisema kwa ufasaha, kwa kueleza shida zake. Kwa mfano njaa, kiu, mahali pa kulala, mavazi na huduma za jamii

hasa matibabu. Hata anapokula mapipani wao (walio katika tabaka la juu) waliajiri askari ili kulinda uchafu ili kina yakhe wasile. Chakula chao kilikuwa ni kuchakura mapipa. Chakula hiki mapipani, waliking'ang'ania na nzi na makombamwiko. Hata kupata chakula ilikuwa ni dhiki. Jazanda ya waya wa sing'enge za miiba iliyokaa kama makucha ya tai ni hali ya kuonyesha jinsi watu wa tabaka la juu huwa wanajitenga kwa watu wengine.

Matope alifanyiwa ukatili wa kila aina. Chakula alichokuwa akipata katika pipa jaa lake la kawaida, kilipikiwa ndani sumu ya panya. Matope anasema,

> ... Isitoshe dawa ya kunguni ikawa imepulizwa juu yake kama vile mchuzi ... Niliduwaa kwa kituo hivi huku nikitamani na kukitazama hicho chambo cha mauti. Njaa ilikuwa ikinikata, kunisaga na kunikebehi mno. Nile nisile? Wacha nile nifie mbali nina maana gani basi? Kwanza ni nani atakayejua kumekufa mtu? Si afadhali kujitoa katika hali hii ya unyonge na utesaji pengine huko ahera huenda nikaonewa huruma? ... vicheko vya kwikwi ndivyo vilivyonizindua na kunitoa ganzi moyoni. Niliona mwenyeji wangu ... wakinicheka undwele wangu. (*ukurasa 40*)

Hii ni dhuluma na unyama aliofanyiwa Matope. Matope alikuwa majeruhi wa hulka ya jamii. Utu katika jamii umekuwa unyama. Wanajamii hawaamini utu tena. Mambo ya faida hayazingatiwi, ndipo msimulizi aliposema kuwa, kama tulivyoona hapo awali mafuta yalitumiwa kudumisha falsafa yao ya uongo. Lakini maji yalihitajika na kila mtu. Mafuta ndio thawabu na maji ni mauti. Baada ya Matope kutoa udhuru wake baraza la mahakimu liliweza kumtesa zaidi. Hata ukanda uliokuwa ukimstiri uchi wake ulikatwa kwa hasira ilhali watesi wake

wanacheka na kuona raha. Tukio hili linaweza kulinganishwa na matukio ya jadi huko Roma. Matukio ya kihistoria yanaeleza kuwa, watumwa katika jamii hii ya warumi walitunzwa vibaya. Wangeliwekwa katika jumba la maonyesho ili wapigane na simba. Watumwa wangeweza kuraruliwa na simba ilhali umma umekaa kutazama na kushangilia jinsi huyo mtumwa mnyonge na hafifu alivyoraruliwa na simba. Majumba kama haya yaliitwa gladiata (gladiator). Mahakama hizi zimekuwa kama majumba hayo ya maonyesho katika enzi za warumi. Mwandishi anasema,

> Sasa ikawa mate, halafu makohozi na mwisho, mateke. Ikawa sasa ni mashindano ya yupi angeweza kuja na utesaji wake wa kubuni ambao ulikuwa tofauti kabisa. (*ukurasa 41*)

Matope kama jina lake, lilikuwa jina la majazi. Aliteswa kwa kupigwa kinyama kama msimulizi alivyoeleza hapo juu. Matope alihiari kunyamaza alipopelekwa mahakamani. Hili tukio lilichukuliwa kama uzushi na dharau kwa mahakama. Licha ya Matope kuwa kizimbani aliteswa na kunyimwa haki zake za kibanadamu. Kipande cha tambara alichovaa kustiri uchi wake kilitupiwa mbali na akabaki uchi. Tukio hili ndilo lililokuwa furaha ya watesaji wake. Matope alijua kuwa mahakama hizi hazitoi haki. Kujitetea kwake kungekuwa bure bilashi. Jamii hii haikudhamini maslahi ya akina yahe kama Matope.

Nadharia ya uhalisia wa kijamaa inasawiri matukio ya kijamii kwa kueleza matukio yanayotokea siku hadi siku katika maisha ya watu. Mambo ambayo

hayana budi kuelezwa kutokana na uzoefu wa wanaoyaeleza. Jamii hukabiliana na mambo haya ana kwa ana. Senkoro 1987:65 anasema,

> ... katika uhalisi wa kijamaa, msingi wa kinadharia umejikita katika kuelewa leo ya jamii kwa kutumia jana. Kutokana na nguvu mbalimbali za hizo jana na leo, mwandishi wa tapo hili la uhalisia wa kijamaa huunda fani na maudhui ya kazi ya fasihi yawezayo kueleza kesho ya jamii zao. Wasanii hao wanao uwezo wa kuisawiri kwa undani jamii yao na hata kuielekeza katika ujenzi wa jamii mpya ya kesho. Undani wa kuyaelewa matatizo na kani mbalimbali za jamii unajitokeza.

Katika maelezo haya ya Senkoro tunaona jinsi mwandishi ameichora jamii yake kwa kuchunguza mazingira na nguvu zake mbalimbali. Katika mazingira haya tofauti mwandishi anaonyesha misingi ya kitabaka ambayo ni mojawapo ya mihimili ya uhalisia wa kijamaa. Njia ya pekee ambayo ingelileta usawa ni mabadiliko. Haya ni mabadiliko ya kuondoa mafuta na kuleta maji. Matope katika kisa chake anasema,

> ... Mmepindua hata sheria za maumbile ili kumamatia enzi zenu ... unyama wenu ndio utu na utu ndio unyama. Mafuta ndio thawabu na maji ni mauti. Si maji ni uhai? Ni maisha na ni chanzo? Vipi leo yasemekana ni Mafuta? ... Tutazuka basi na maji tuyakomboe kwani maadamu vidonda viko, nzi kufa si hasaraaa . . . (*ukurasa 41*)

Maelezo ya Matope ni sauti ya kutaka mapinduzi. Jambo muhimu ni kuwa mabadiliko haya hutiliwa nia, hutakwa na hudaiwa. Mahitaji ya mabadiliko katika jamii ni ya nguvu na lazima. Wanyanyasaji hutumia vyombo kama mahakama kuonyesha kuwa wanatenda haki ilhali ni kudanganya umma.

**Mahakama**

Mahakama huwakilisha mahali ambapo Haki hutolewa. Lakini mahakama tunayoiona katika riwaya ya *Mafuta* imekiuka kaida zake za kutoa haki. Haki za Matope kama binadamu zilidhalilishwa na mahakama. Matope akiwa mahakamani alizidi kuteswa. (Tazama ukurasa 41 kitabuni). Hata Dubwana alipokuja alistaajabu. Akiwa mahakamani Matope alikuwa yu tulii. Mwaandishi anasema;

> ... Mate aliyotemewa yakiwa sasa yaanza kumdenwa ute, damu zikimchururuzika, maumivu yakimchoma kama miiba, huku mashavu na viungo vikimwira kwa shauri ya makofi, mateke, bakora na marungu. (ukurasa 43)

Hayo yote ni mateso aliyopata Matope. Huu ni ukiukaji wa haki za kibinadamu. Wapi mahakamani mahabusu wanateswa? Kwa ukatili wa namna hii, ni macho ya nani yasiyolengwalengwa na machozi na uso kushikwa na huzuni. Wakati mwingine watu hucheka mahakamani kutokana na jibu lililotolewa. Lakini katika mahakama hii Mtue na Ti walipocheka majibizano baina ya Matope na Dubwana walikuwa wamejichongea. Waliokuwa mahakamani waliwaona Ti na Mtue kama wasaliti; watu wasiotaka kuendeleza dhana ya Mafuta. Lakini walitaka ukombozi wa maji. Ti na Mtue walisimamishwa labda kupewa adhabu. Lakini Dubwana alipomwona Ti akiwa pamoja na Mtue mambo yaligeuka. Hakudhania mtu anayemjua angelikuwa miongoni mwa waliocheka mahakamani. Kucheka mahakamani ni dalili ya upotovu wa nidhamu au uchochezi. Msimulizi anatutolea hali ya Dubwana kwa kusema,

> "Vile kumwona Ti tu, Dubwana mdomo ukamwanguka. Bumbuazi hili alilificha kwa kujinong'onezea, "kweli kikulacho ... waliokuwepo hawakuweza kutanabahi mshangao wake na pili hakutaka kuwapa fursa ya kuwa na shaka juu yake ... alimgeukia Matope kwa fedheha na akafoka, "mahakama haya yamekata unyongwe ili uwe kielelezo kwa wengine." Akatoka. (*ukurasa 45*)

Uamuzi wa Dubwana (hakimu) juu ya Matope ulishangiliwa na Baraza la wateule isipokuwa Ti na Mtue. Baraza hili lilikuwa la watu ambao hawataki haki kutendeka. Haki kutendeka ni kama kosa la jinai. Mama Fofi ndiye aliyeshikwa na simanzi kwa sababu msiba uliomtokea ulimnyima fursa ya kupanda hadhi na kuwa mteule maishani ili naye aweze kunyanyasa wengine.

Pia tunaona kuwa wasemao wambao wamba kuwa hakuna sheria isiyokuwa na upekee au jambo lisilofuata kawaida. Dubwana hakuwaibisha Mtue na Ti kwa sababu Ti ni miongoni mwa wateule. Lakini Ti hakuridhishwa na yale yaliyokuwa yakitendeka mahakamani. Punde Mtue na Matope wanaonekana pamoja wakiwa wafungwa. Mtue hakudhania angelikuwa mfungwa pamoja na Matope. Kwa upande mwingine Ti aliachiliwa na kwenda zake. Jambo hili linatuonyesha kuwa kuna watu wanaoweza kudhulumiwa bila sababu na wengine kuachiliwa. Wahusika hawa wawili wamenasibishwa na haki katika jamii. Uhalisia wa kijamaa unahitaji vyombo vya kutekeleza haki viweze kutoa uamuzi uliokubalika. Kutokana na dhuluma hizo zote kuna wazo la kuzingatia mapinduzi katika jamii. Mapinduzi haya yatakuwa katika mfumo wa kisiasa, kijamii na kiuchumi. Sera ya jamii kuhusu mahakama inatakiwa kubadilika. Hata hapa nchini (Kenya) baadhi

ya mahakimu na majaji waliweza kutimuliwa kwa sababu ya kutoendesha sheria kwa njia inayofaa. Mahakama ilikuwa ya wale wenye nguvu sio wenye haki. Ukombozi huu umejikita katika nadharia hii ya uyakinifu wa kijamii ambao unataka kumkomboa mfanyikazi na mkulima kutoka kwa minyororo ya ubepari. Katika riwaya ya *Mafuta*, ndimo tunakuta harakati za ukombozi wa wanyonge kama Matope, Chanzo, Pakacha na wengine. Hawa ni watetezi wa Haki.

Kucheka kwa Ti na Mtue kulichukuliwa kama hatia na kulionekana kama dharau, kashifa au uasi. Mahakama hii haikumruhusu mshitakiwa au mtuhumiwa kuuliza maswali, kujibu chochote au kutoa wazo lolote. Ti aliachiliwa na Mtue akaamuliwa kwenda kijiunga na Matope. Dubwasha alisema,

> ... wewe Ti, kwa leo nenda lakini doa unalo ... Na huyo mwenzako mjuaji, kwa uasi wake, ni aende akaungane na Matope kwani huko atajua maana ya chungu kufa siafu wachomwapo. (*ukurasa 44*)

Kwa upande mwingine hivi ndivyo ilivyokuwa hukumu iliyoitwa ya 'Haki' iliyotolewa na Dubwasha. Dhuluma na ukatili huu unaotokea katika mahakama ni dalili ya kutaka kudumisha utabaka. Mnyonge hana haki. Matope na Mtue wanawakilisha kundi la wafungwa waliozuiliwa hapa barani Afrika bila sababu. Waliweza kuwekewa mashtaka ya uongo. Mahakama hizi zilikosa unyoofu na mahakimu wake walikosa uadilifu.

Hadithi hii ya Matope inatoa muhtasari wa shida za wanyonge katika jamii. Wanaoonyesha huruma kama Mtue wao pia huwekwa kizuizini kwa kisingiziwa kuwa wao ni washiriki wa wachochezi.

### 3.1.4 Hadithi ya Ti

**(Mabadiliko)**

Hadithi hii inamhusu Ti. Baada ya Mtue kuzuiliwa, Ti alifunga safari kwenda kuijulisha jamii ya Mtue msiba uliompata (Mtue) walipokuwa naye. Safari hii ilimpeleka katika dunia nyingine, dunia ya wachochole, ulimwengu uliomweka ana kwa ana na matatizo na mateso ya wanajamii. Ti mwenyewe alikuwa mzawa katika tabaka la wateule. Safari yake ni taswira ambayo msimulizi alitumia ili kuonyesha ujinga uliokuwa ukitawala maisha yake. Safari hii ilileta mabadiliko katika maisha ya Ti kwa kumwunganisha na wanaharakati wengine waliokuwa pamoja na Msati. Ti ndiye aliyempeleka Mtue kusikiliza shughuli za mashtaka ya mahakama, alikopatwa na msiba huu wa kuzuiliwa bila kufanyiwa mashtaka. Baada ya Mtue kushikwa macho ya Ti akili yake ilifunguka. Msimulizi anasema,

> ... ujinga ndio uliokuwa ukimtawala mwake maishani ... Ajabu ni kwamba, nilizaliwa (Ti) ujingani. Nikaishi ujingani, nala, nanywa nafa ujingani ... Yaonekana ujinga na wepesi, ni raha, ni starehe na hausumbui. Ujinga si matatizo, bali ni starehe ya kujiona ni mimi tu na mimi tu basi. Ti akawa anajiwazia. (*ukurasa 51*)

Mawazo haya ya kujifikiria pekee ni mawazo ya kibepari. Lakini baada ya fikira hizi Ti alivuka mpaka na kujikuta katika dunia nyingine. Hii ni dunia ya watu

waliokosa mafuta. Hawa walikuwa damu moja na Matope. Kina Matope walikuwa halaiki. Hivi kwamba tabaka la wachochole lina watu wengi. Watu hawa hawakuwa na sauti. Kuuliza swali kulikuwa makosa, lakini macho yao ndiyo yaliyokuwa yakionekana kama yanauliza maswali. Maswali ambayo macho yalikuwa yakiuliza yalikuwa kochokocho. Kwa mfano ukosefu wa chakula, umilikaji wa nyenzo za uzalishaji mali, mbona mkunazi unamilikiwa na mtu mmoja, masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Walio katika tabaka hili ni kina Jasho ambaye anajaribu kuinua kichwa chake na kujitokeza kuwa afueni zaidi sababu ana kioski; wengine ni kina nyepi, Zaitu na Pakacha. Kioski ya Jasho huuza chai na mandazi. Labda hiki ndicho chakula cha maana kinachoweza kupatikana hapa. Wananchi katika sehemu hii ya ulimwengu wamenyimwa uhuru wa kusema na ukweli waumiza. Hili ndilo alilosema Abdilatif Abdalla (1972:23) katika shairi la *Kuno kunena*. Uhuru wa kusema haupo kabisa. Ikiwa utasema lazima uwe ni uongo mtupu – hasa kwa wale wa tabaka la chini. Watu walio katika tabaka la wachochole hawawezi kudai haki zao. Ikiwa watafanya hivyo, basi hilo litachukuliwa kama uchochezi na bila shaka watazuiliwa bila sababu. Hata Jasho na wenzake hawakumwamini Ti walipomwona. Waliona kuwa yeye ni kibaraka wa watawala. Lakini Ti anasema amezinduka kutokana na aliyoyaona. Hii ni hali ya kuleta mabadiliko baada ya kuona udhalimu unaotendewa jamii.

Haya mabadiliko hayawezi kuja kwa kujitia kilema cha ububu na kusema uongo. Lakini yatatokea kwa kusema ukweli na kuamsha ari za wachochole. Mkangi ameeleza kinagaubaga juu ya mifumo itumiwayo kudhalilisha wanyonge. Mifumo hiyo ikiwa ni siasa, uchumi na masuala ya jamii. Kukataza watu kusema ukweli au kutoa mawazo yao ni njia moja ya ugandamizaji. Katika mfumo huu, watu nusura 'washonwe' midomo ili wasiweze kusema lolote. Aliyesikika akinena alipelekwa kizuizini kama Mtue bila kufanyiwa mashtaka. Udhalimu wa aina hii hutendeka katika nchi nyingi za Kiafrika, Kenya ikiwa miongoni mwa nchi hizi. Hali na matendo ya Ti yanaonyesha kuwa mivutano haipatikani baina ya tabaka moja na lingine peke yake bali hupatikana mumo humo katika tabaka moja.

Kushirikiana kwa Ti na Mtue kuliamsha ari yake kuhusu jamii yake. Ti anasema,

> La kwanza ni kuhusu ugawaji wa haya mafuta – mbona ni milki ya wateule tu. Mmoja wao akiwa mimi? Akauliza wenye masikio ... Na la pili ni kuhusu uongo. Kama vile Matope alivyosema, mbona kuyafanya mafuta kuwa ndiyo chanzo hali ni maji ndiyo.
> (*ukurasa 60*)

Maelezo ya Ti yanatuachia masuala yanayohitaji majibu. Pili watawala walitumia uongo ili kuendelea kushika nyadhifa zao, kwa mfano kuwaeleza uteule uliandamana na Mafuta. Wazo la tatu katika maelezo yake linaturejesha kwa suala la ujamaa ambalo ni mojawapo ya mhimili wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Katika suala hili Mkangi anaonyesha kuwa mali ya nchi isimilikiwe na kundi la watu wachache ambao ni mabepari. Kwa kuuliza swali "mbona ni miliki

ya wateule tu?" anashtumu ubepari na kuonyesha kuwa mali ya asili na matumizi mazuri ya malighafi haya ndiyo yanayoweza kuleta maendeleo katika jamii. Pia Ti alionyesha kuwa mienendo ya walio katika tabaka la juu ilienda kinyume na matakwa ya uhalisia wa kijamaa ambao huzingatia uwezo wa kila mtu na hujengwa, huimarishwa na kukidhiwa kwa kusudi kubwa la kushinda kabisa mazingira ya mtu huyo kwa manufaa ya jamii nzima. Msingi ya uhalisia wa kijamaa hukusudia kujenga mtu mwenye furaha, amani, na mwenye nia ya kuubadilisha na kujenga ulimwengu upya. Safari aliyofanya Ti kutafuta mahali ambapo Msati anakaa ilimpa uzoefu na kumwonyesha dhiki ambazo watu wa tabaka la chini hupitia. Ti anataka pawepo na usawa baina ya wanadamu. Yeye anajitokeza kama kiongozi wa wadhalimu na baada ya maswali aliyojiuliza hapo juu anakuwa mwanaharakati.

Ti alijinasibisha na wachochole. Kwa kujinasibisha na kina Zaitu, Jasho na Pakacha ni kama alikuwa akipata ubatizo wa moto. Mwandishi anasema,

> Baridi na Matope haikuwa ikimghasi tena kwa kuwa, juma zima hakuwa akilala pengine isipokuwa ndani ya kidimbwi! Ungeambiwa kuwa huyu ndiye yule Ti hungesadiki! (*ukurasa 60*)

Kukubali ubatizo ni kule kubadili tabaka, kuwa miongoni mwa wanaopigania haki. Hali hii ilimpa uzinduzi juu ya maisha ya wachochole. Msati ambaye Ti alikwenda kumwona aliishi katika banda bovu lililoezekwa kwa matambara ya plastiki, mabati mabovu na mabaki ya makadibodi. Mandhari hii ilionyesha hali duni ya

Msati na wengine. Msati alimkaribisha Ti katika chama hiki cha kupigania haki. Msati alikuwa hapo na wenzake kwa mfano Jasho, Pakacha na kadhalika.

Baada ya safari yake, Ti anasema kuwa amebadilika. Ametoka katika ule utabaka wa wateule. Gweni alimjulisha kuwa msiba wa Mtue si wa pekee. Kuna wengine waliojipata katika matatizo lakini walivumilia. Baadhi ya hawa ni akina Matope na wafungwa wengine wa siasa, kwa mfano Mkangi.

Watoto walidhaminiwa sana kwa sababu wao ndio viongozi wa kesho. Chakula kilipoletwa watoto walipewa kwanza halafu watu wazima wakapewa baadaye na wakala kwa pamoja. Hili jambo ni kinyume na wakati huu ambapo kuna chokoraa na watoto wa mabanda au mitaani kama wanavyojulikana ambao hula mwata. Watu wazima hupewa chakula baadaye na hula pamoja. Ti alifunzwa kuwa na utu na kuishi katika jamii kwa njia ya kijamaa sio ya kibepari ambako alikuwa akijifikiria yeye tu. Mifupa ilikuwa ya jibwa na sio ya watoto kwenda kuokota mapipani kama Matope alivyokuwa akifanya. Wito huu wa kushirikiana ndio uliokuwa muhimu katika maisha ya wanajamii. Msiba wa mmoja ni msiba wa jamii na furaha ya mmoja ni furaha ya jamii.

Tabaka hili hujumuika kwa pamoja kupitia kwa hadithi zenye mafunzo yenye adili. Hadithi hizi zilisisimua sana kiulumbi na kimawazo. Baada ya chakula hadithi hizi zilitolewa. Kujumuika pamoja kwa kipindi cha hadithi ni njia moja ya

kuleta ushirikiano. Hadithi ya Ti inaeleza juu ya ushirikiano, kuondoa ubepari, kushirikiana katika harakati za ukombozi, Mafuta ni uongo, na kuzuiliwa bila kufanyiwa mashtaka kwa washukiwa.

### 3.1.5 Hadithi ya Mbeyu

Hadithi hii ilihusu jamii iliyokuwa na watoto saba na wazazi wawili. Ilikuwa jamii iliyojiweza kifedha. Utajiri wao ulidhihirika wakati wa chakula cha jioni. Meza iliandaliwa na mapochopocho na matunda. Wazazi wa watoto hawa walifanya kazi tofauti. Baba alifanya kazi ya kuwatesa wafungwa, kwa mfano kuwadunga pini vidoleni na kuwachoma na moto wa sigara/spaki hasa katika sehemu zao za siri. Baba alijigamba alipewa kazi hii na Maulana kwa hivyo hayo yalikuwa majaliwa yake. Mshahara wake ulikuwa maridhawa.

Kwa upande mwingine, mama alifanya kazi ya kuavya wasichana mimba na wasichana waliokuja hapa walitoka katika tabaka la juu kwa sababu wazazi wao walichelea aibu. Mama huyu alilipwa pesa maridhawa kwa kazi hii. Wazazi hawa walijidai wanatimiza Utumwa wa Mungu. Kwa hakika huu ulikuwa ukatili wa kukatisha maisha ya viumbe wa Mungu. Kwa baba hii ilikuwa dhuluma kwa wafungwa. Mambo haya yanaonyesha jinsi utu umewatoka watu hawa. Utu wao umekufa. Wanachothamini ni pesa peke yake. Kama tulivyoeleza hapo awali katika ukurasa 12, jamii ya kibepari haioni kitu chochote ila pesa na pia hawajali njia zinazotumika kupata pesa. Wanaona ni afadhali waue lakini wapate

pesa. Wanapotekeleza unafiki huu wanajificha katika wazo kuwa wanatekeleza kazi ya 'Maulana'. Kutesa wafungwa ni kutaka kutimiza matakwa ya wakubwa wao. Mateso kwa wafungwa ilikuwa njia ya kuwatia hofu ili wasiweze kusema ukweli na kuonyesha utu. Mtue anaeleza mateso ambayo wafungwa hupitia kwa kusema,

> Ndio mwisho wangu leo, wazo moja lilimjia. Na jingine, watanitia kitanzi, kunipiga marungu ama kunilipua kwa risasi? ... nadhani wanaenda kunitesa tu. Moto wa spaki uumeni, sindano vidoleni, kutoswa mapipani yaliyojaa maji machafu, kuogofya na majoka ama kupelekwa msituni, kufungwa kidoto na kutishwa na mabastola, kukemewa, kukaripiwa, kupondwa na matako ya mabunduki, kusukumwa, kutukanwa, kudadisiwa, kufyandwa kudungwa, ku- (*ukurasa 83*)

Wengine walitoswa kutoka majumba marefu na kusingiziwa kuwa walijirusha chini. Wengine walisafirishwa wakiwa wamefungwa vitambaa vyeusi usoni ili wasione mahali wanapokwenda.

Katika mahojiano yangu na Mkangi aliweza kunidokezea juu ya mateso ya aina hii.

Haya ni mateso yaliyowakumba wafungwa. Unyama na ukatili huu ndio uliokuwa ukitendwa na baba yake Chanzo. Mamake chanzo alipenda kazi yake ya kuavya wasichana mimba kibandia. Kila mara alisema hayo yalikuwa majaliwa ya Maulana. Hapa nchini Kenya katika jiji la Nairobi, sio kitambo sana, mwezi wa tano mwaka wa elfu mbili na nne palipatikana vijusi vilivyoavywa vimetupwa

kandokando ya barabara. Watekelezaji wa uhalifu huo hawakupatikana. Hili lilikuwa suala la simanzi kwa jamii yakiwemo makundi ya makanisa yaliyoweza kulaani kitendo hiki. Sembuse Mamake Chanzo anayefanya kitendo hiki kisirisiri na kusema kuwa haya ni majaliwa kutoka kwa Maulana. Huu ni unyama na unafiki kuwadhuru viumbe wasio na hatia.

Wakati wa mlo watoto wao walikuwa na zamu ya kutoa sala. Sala hii ilikuwa karibu sawa. Mtoto wa kwanza, pili, tatu ... Maombi yao yalienda hivi,

> ... tukijua kwamba ni kwa kuwateua wazazi wetu na kuwatunukia kazi zao nasi ndipo ukatubariki na chakula hiki. Tunatoa shukrani kwa kukila kwa niaba Yako, ya Mwanao na ya Roho Mtakatifu ... Amen. (*ukurasa 68*)

Baba Chanzo angepongeza kwa kusema kuwa hiyo ilikuwa sala nzuri. Kweli ilikuwa sala nzuri, kutegemea kazi zao? Watoto walieleza kuwa wamebuni sala. Siku ya saba kitindamimba ambaye ni Chanzo alibuni sala yake aliposema,

> "Tunatoa shukrani kwa wafanyakazi wote waliohusika na uzalishaji wa chakula hiki, pia baraka ya Mama Ardhi isifiwe," Amen
> (*ukurasa 69*)

Chanzo alishtumiwa na kuzomewa na wazazi wake. Wazazi wa Chanzo walitaka kujua waliomfunza sala hii ya kiupuzi. Licha ya kusema aliibuni hakuna aliyetaka kusikia. Walimu pia walishutumiwa kwa kuwa wafunza wanafunzi mambo yasiyofaa. Mambo ambayo yanawapotosha. Walimu hawana adabu. Chanzo alifukuzwa na kuambiwa ajiunge na wafanyakazi hao wenzake anaowapenda. Katika sala hii tunaweza kupata maudhui yafuatayo:

Kwanza kuna kule kufuata mfumo fulani kwa sababu tumo katika tabaka hili la utawala wadhalimu na wakatili. Pili, katika jamii ya kibepari wafanyikazi ndio wanaofanya kazi za sulubu ili kutoa mazao na kuzalisha mali lakini huwa hawamiliki chochote. Nyenzo za kuzalisha humilikiwa na mabwanyenye na mabepari. Mali hapa hupatikana kwa kunyonya umma hasa wafanyakazi. Huu ubepari utavunjiliwa mbali kutokana na nguvu za wafanyakazi.

Hao wafanya kazi huweza kuungana pamoja na kuleta mabadiliko (mapinduzi). Tabaka hili la wafanya kazi ni tabaka la watu wanaodhulumiwa. Mara nyingi wao huhitaji tu kupewa uongozi na watachochea mapinduzi. Kwa hivyo Baba yake Chanzo aliposikia 'wafanyakazi', alishikwa na 'kiwewe' kwa sababu alijua hatima yake. Jambo la tatu ni kuwa katika misingi ya kiuchumi, ardhi ni kitu muhimu kwa jamii; ni nguzo ya uzalishaji mali. Ardhi hii ni mali ya jamii. Lakini katika mfumo wa kibepari huwa imemilikiwa na watu wachache, ambao hutumia wafanyakazi kwa shughuli zao za kujilimbikizia na kuzalisha mali ilhali wao (wafanya kazi) hulipwa kidogo. Faida huenda kwa mabepari wanaomiliki mashamba. Hili huzua migongano na migogoro baina ya matabaka haya mawili.

Mwisho hadithi hii inaonyesha kuwa msema kweli ndiye huadhibiwa. Hadithi hii huchukuana na maneno ya Matope kuwa,

> Ukweli umekuwa uongo na uongo ukweli... Yeye yuangojea kifo cha yule mtoto. Kwa kinamna yake, ile adhabu yake pia ilielekea huko mautini. Kwani

> akunyimae chakula lengo lake kubwa si ni kukuua kabisa.
>
> (*ukurasa 70*)

Chanzo aliadhibiwa kwa kusema ukweli. Tawala za wadhalimu huwa hazipendi wanaosema ukweli. Mara nyingi huwekwa kizuizini bila kufanyiwa mashtaka yoyote. Wengine hushtakiwa chini ya sheria ya usalama wa nchi na kuhatarisha amani.

### 3.1.6 Hadithi ya GWENI

**(Mfalme aliyeenda uchi)**

Hiki ni kisasili cha Wayunani. Lakini mwandishi amekitumia hapa kutoa maudhui yake. Kisa hiki pia kimetumiwa katika uandishi mwingine wa Robert Bolt (1960). Mfalme kwa kawaida hapungukiwi na chochote ambacho kinaweza kufanya kukosa raha. Mfalme alighasiwa na maumbile ambayo hayakumpa tofauti yoyote na akina yakhe. Jambo hili lilimtia simanzi na kiwewe, hali iliyozorotesha afya yake. Mfanyakazi ambaye alifanya kazi ya kushona nguo alipiga moyo konde na kumwuliza mfalme amweleze shida yake. Mfalme alihiari kumweleza. Fundi alimwambia hilo lilikuwa jambo dogo. Mshonaji alitoa suluhu hii, kwanza kumshonea mfalme joho ambalo ni la kipekee. Baadaye mfalme angelipanda ulingo na mavazi yake rasmi. Huyu mshonaji angelipanda ulingo pia na kumtoa mfalme nguo zake zote na kuacha taji la kichwani pekee. Kisha akajifanya anamvika joho lililokuwa la thamani ya ajabu ambalo lingeonekana tu na wale

wasiokuwa na doa. Mshonaji aliwageukia mawaziri, majemadari na wale wote mashuhuri waliokuwepo na kuwauliza, Je mwalionaje? Walijibu kwa kusema;

> ... Ni joho la kipekee, hatujaliona lizidilo hili ! Haya yakawa majibu ya kulisifu. Ni wakati huu, yule mfalme alikuwa akiteremka zile ngazi kwa kimadaha na huku mikono akileweshalewesha kiutukufu. Na jinsi alivyokuwa akiwasogelea, ndivyo wale wakubwa walivyozidi kuusifu jinsi utukufu wake ulivyoongezewa na hilo joho ! Kila mmoja alimsifu kivyake na huku wanawake wao wakimpigia vigelegele. Kifika chini ya ngazi . . . Lile jilango la jumba lilifunguliwa naye akajitoa nje ili raia pia nao waweze kulihusudu joho ... raia walipigwa na bumbuazi walipoona mfalme akiwa katika hali kama hii. (*ukurasa 73*)

Ingawa raia waliduwaa na kushikwa na mshangao kwa hofu kuwa mfalme wao amekuwa kiruu, wafuasi walizidi kuropokwa sifa za kila aina. Lakini kulitokea mtoto mdogo aliyemwendea mfalme na akamwuliza, "Mtukufu, mbona uko uchi." Mfalme na mkuruto wake walitanabahi wehu wao kwa kukimbilia jumbani na kijifungia wasitoke tena milele.

Katika hadithi hii maudhui haya yanaweza kupatikana. Kwanza kabisa ni kuwa, wale wanaoimba nyimbo za utawala na kufuata sera zake za ugandamizaji hawawezi kumwambia mtawala/kiongozi ubaya wake kwa sababu watatengwa au watashushwa madaraka. Wazo hili limeonekana mahali pengi katika utawala mwingi wa nchi za kiafrika hasa hapa nchini Kenya. Wafuasi wa kiongozi huimba sifa ya kiongozi hata bila kufikiria. Wazo la pili hapa ni kuwa viongozi wenyewe hupenda kuvikwa kilemba cha ukoka ndiyo waone raha. Baadhi yao hupewa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

cheo kama 'mtukufu'. Mbona wasitumie cheo cha kikazi, "mheshimiwa"? Wazo la tatu ni kuwa, baada ya kuwa katika ngazi za uongozi, kiongozi huweza kulewa huo uongozi mpaka akawa anafanya vitu ambavyo hastahili kufanya. Upumbavu wa mfalme ulipodhihirika mfalme hakuendelea kutawala. Jambo hili ni dhahiri katika mataifa mengi ya bara la Afrika. Viongozi huwa uongozini kana kwamba waliumbiwa kiti cha uongozi. Lakini wakati wao hufika kama anavyosema Gweni kuwa "Yule mfalme na mkurutu wake walitanabahi uwehu wao kwa kukimbilia jumbani na kujifungia wasitoke tena milele."

Raia wanapogundua kiongozi wao ni mwehu hawana budi kumwondoa. Labda niulize swali, ni viongozi wangapi ambao wameweza kuondolewa kwa njia hii? Jibu ni wengi. Wengine huondolewa kupitia kwa upigaji wa kura. Nchini Kenya kura ndio silaha ya viongozi kama hao. Jambo la nne ni kama alivyosema Msati kuwa historia imeonyesha kuwa msema ukweli yeyote huadhibiwa vikali sana. Mifano inayotolewa katika riwaya hii ni kochokocho. Kwa mfano Matope alihukumiwa kifo, Yesu Kristo aliuawa, Mtume Mohammed alifukuzwa kutoka Mecca hadi Medina. Mahatma Gandhi na Martin Luther King waliuawa kwa kusisitiza kuwa utu wa mwanadamu ni sawa. Mwanasayansi aliyegundua kuwa Jua ndilo lililo kati ya Ulimwengu, alishtumiwa na kuitwa mkosa dini, mwongo na mchochezi na kanisa Katoliki likamlaani mpaka wa leo. Aliyesema kuwa moyo hauko kichwani bali kichwani kuna ubongo na kifuani ndiko kuna moyo, alishtumiwa na karibu auawe. Aliweza kunusurika kwa kuwaeleza watesi waende

wamwangalie ng'ombe aliyekuwa amechinjwa sokoni. Walipohakikisha kuwa ubongo upo kichwani na sio moyo, basi hapo ndipo aliponusurika.

Huu wote ulikuwa ukatili na dhuluma. Katika nchi kama hii hakuna uhuru na haki. Sheria katika nchi hii ilikuwa imeenda segemnege. Ti anapinga dhuluma hii kwa kusema kuwa,

> ... Papa hapa kwetu pia wasema ukweli nao wakiuawa, kufungwa, kuhamishwa, kuteswa, kuitwa waongo na kadhalika? Mwisho si twajua kilichomtokea huyu rafiki yetu ambaye twamwita Matope aliposema, maji ndio chanzo cha uhai si Mafuta?... Ama historia yasemaje? (*ukurasa 77*)

Mara nyingi katika tawala za wadhalimu wasema ukweli huadhibiwa vikali. Tumeona mateso ambayo wao hupitia, wengine huwekwa kizuizini bila kufanyiwa mashtaka. Jambo hili limetokea katika nchi nyingi za bara hili la Afrika. Matope ni jazanda iliyotumika kuonyesha udhalimu wa namna hii hapa kwetu Kenya. Mwandishi wa *Mafuta* na *Walenisi* ni miongoni mwa wale waliodhulumiwa na utawala huu usiotaka ukweli. Utawala usiotaka mtu kuzungumza juu ya dhiki na dhuluma wanazotendewa wanajamii. Walioweza kusema ukweli waliweza kujichongea na kutiwa kizuizini. Miongoni mwa hawa ni Al-Amin Mazrui, Mkangi, Okong'o Oyugi na wengine wengi. Walipokuwa kizuizini walinyimwa uhuru wao na kudhalilishwa kwa kila namna.

Mwisho mwandishi anasema kuwa,

> Ukweli ndio maendeleo. Tusiposema ukweli tutakuwa kama wanyama. Wasiotaka maendeleo yaani ukweli kwa sababu ya kudunisha ubinafsi wao tu, hawa huwa kama visiki. Kwani haichukui muda kung'olewa mbali kwa jembe la ukweli ... Ukweli ni mapambano. (*ukurasa 77*)

Mapambano yanahitaji viongozi walio wakakamavu kama huyo mtoto aliyemjulisha mfalme wehu wake. Matope, Msati na Ti ni watu walio katika mstari wa mbele kuleta mabadiliko. Wazo lingine ni kuwa haya mapambano yataendelezwa kwa njia gani? Mapambano yataendelezwa kwa njia ya kujitolea bila woga. Ngugi 1987:112 anasema "Uwoga mwingi huleta umaskini nchini." Wazo lingine kuendeleza mapambano ni kushirikiana kwa sababu umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Wazo hili litawasaidia kuota kuyabadilisha maisha yao na kuwa na uongozi bora katika tabaka linalodhalilishwa. Uongozi huu unaweza tolewa na wasomi au watu walioasi kama Ti. Mapinduzi yanaonyeshwa kuwa ndiyo suluhu kwa mivutano hii baina ya mabwana na wadhulumiwa.

### 3.1.7 <u>Hadithi ya JASHO</u>

**(Nyani na Chui)**

Katika hadithi hii nyani na chui wanapanda mti mrefu kuona kama vita vinakuja. Nyani alikuwa mbele na Chui nyuma. Chui alimtia nyani makucha walivyopanda na kuramba damu. Wakiwa kileleni chui alimwuliza nyani ikiwa kulikuwa na vita vinavyokuja kutoka nje. Nyani alijibu kuwa vita havikuwa nje bali ndani. Hii ni hadithi ya kudhihirisha 'kikulacho ki nguoni mwako'. Kisa hiki ni hurafa kwa

sababu kinatumia wahusika wanyama, nyani na chui ili kufafanua uhalisia wa mambo duniani. Hadithi hii inaweza kufananishwa na za waandishi wengine kama Shaaban Robert *Adili na Nduguze* (1951) au hata George Orwell (1975) *Shamba la Wanyama.* Katika hadithi hii maudhui yafuatayo yanaweza kupatikana. Kwanza kabisa nyani na chui huwa hawana uhusiano mzuri. Chui mara nyingi humwinda nyani kama kitoweo chake. Kwa hivyo kuna migogoro ya kindani, baina ya watawala na watawaliwa. Watawaliwa wanadhulumiwa na watawala jinsi chui anavyofanya. Pili, wenye nguvu kama chui huwagandamiza wasio na nguvu, kwa mfano jinsi chui alivyomdhulumu nyani. Nyani hana makucha na nguvu kama chui. Katika hadithi hii pia tunaona suala la uongozi, usalama wa jamii na mahusiano ya watu katika jamii hasa baina ya wanyonywaji na wanyonya au baina ya wenye nguvu na wanyonge.

Katika jamii kuna wale wenye nguvu ambao kwa njia zozote huwadhulumu wengine. Dhuluma hizi zinakiuka haki za mwanadamu kuishi na kuufanya ulimwengu mahali bora pa kuisha. Matatizo haya yanaweza kusuluhishwa kwa masikilizano. Ti baada ya kuwa katika kundi la wateule na pia katika kundi la wachochole aliweza kujifunza jinsi ya kuishi. Aliweza kujua uhalisia wa maisha. Baada ya hadithi hizi, Ti alifunga mkao huu kwa 'kuvunja ngasu' – kwa kueleza siri za wateule. Naye Msati alisema kuwa,

> Usimwone nyuki akitafuta asali pekee ukadhani yu peke yake, na ukidhani ukimwua, basi ushawamaliza wote kwa sababu walio mzingani huwajui, ama na hata huujui uliko. (*ukurasa 80*)

Matope ndiye aliyekuwa katika mstari wa mbele katika kueleza kuwa maji ndiyo yana nguvu sio mafuta. Uongo huu wa watawala ulikuja kufika hatima baada ya wanaharakati kama Ti na Msati walipoungana na kutangaza maji pekee ndiyo Haki.

Pia hadithi hii ya nyani na chui inaonyesha migogoro na mikinzano inayoweza kutokea baina ya wale walio katika ngazi za utawala. Kama kawaida kila tabaka huwa na misukosuko yake. Msukusuko huweza kutoka ndani na suluhu pia huweza kupatikana kutoka ndani.

Mwisho Jasho hakumfukuza wala kumpigia kelele au mayowe mwenda wazimu kwa sababu alitambua kuwa huyu (mwenda wazimu) sio ndiye sababu ya kudhalilishwa kwake. Kudhalilishwa kwake (Jasho) kunatokana na ugawaji mbaya wa rasilimali za nchi na pia wenye nguvu kuwadhulumu wanyonge.

### 3.1.8 <u>Hadithi ya Mtue</u>

Hadithi ya Mtue inatoa maelezo kuonyesha yaliyomsibu Mtue. Mtue katika sehemu hii ametumiwa kuonyesha namna maisha yalivyo kule kizuizini. Pili ameonyesha jinsi baadhi ya watuhumiwa wanaweza kuachiliwa bila kufanyiwa mashtaka kwa sababu wanatoka katika ngazi za watawala (wateule). Hili si jambo geni hapa kwetu Afrika, limewahi kutokea mara kadha. Hali kadhalika Mtue anaeleza sababu za kuzuiliwa kwake anasema;

> ... Ukweli ni kwamba, ameachiliwa (Ti) na wewe kwa nini uko hapa? Eti ni kwa sababu pale ulipokuwa ukijibizana na lile njemba tulicheke kwa kwikwi ... Lakini yeye aliambiwa aende kwa sababu ni mteule. Najua si kwa sababu ya kucheka kwikwi, lakini kikubwa ni kwamba sijitambulishi na wateule ingawa kwa namna yoyote ile nimo katika tabaka yao. (*ukurasa 81*)

Maelezo ya Mtue yanaonyesha kuwa katika tabaka la wateule kulikuwa na wale waliokuwa na mamlaka zaidi kushinda wengine. Ingawa yeye (Mtue) alikuwa katika tabaka hili hakuwa na hadhi yoyote. Hakuwa miongoni mwa wale walio kuwa katika mstari wa mbele na kutambulikana kwa cheo. Kuwa katika tabaka fulani hakuwezi kufanya usifungiwe, hasa unapofarakana na walio katika ngazi za utawala. Tumeona hata mawaziri na wasaidizi wao wakitiwa kizuizini. Mahali ambapo hawakutarajia. Kwa mfano Marehemu Stanley Shapasina Ole Tiptip aliyekuwa wakati mmoja Waziri wa Serikali za Wilaya alipokwaruzana na mababe hasa waliokuwa katika ngazi za utawala alifungiwa. Kuzuiliwa huko kulizoretesha afya yake na mwisho akaaga dunia.

Mwandishi wa *Mafuta* ni baadhi ya watu waliotiwa kizuizini kwa kuhusishwa na kundi la *mwakenya* mwaka wa 1986 na kuachiliwa mwaka wa 1988. Mwakenya lilikuwa kundi la wanaharakati la chini kwa chini lililotaka kupindua serikali kwa kutumia nguvu. Mtue na Matope baada ya kukutana kule kizuizini walionyeshana uhusiano wao wa kiutu kwa sababu wanakabiliwa na adui mmoja. Mwandishi anasema,

> Walitazamana, na kwa ghafla walikumbatiana kama kudumisha ubinadamu wao ... wakiwa katika hali ya

> kugundua kuwa utu ndio kiini cha umoja wao, watu hawa walikaa tayari kusbiri kilichokuwa kikiwajia. Walikata kauli kuwa, lije na lijalo, hawatampa yeyote furaha ya kuwaona kuwa wamesaliti utu huu. (*ukurasa 82*)

Katika maelezo haya Matope na Mtue wanasisitiza utu na haki. Tumeona Mtue hakutendewa haki, hata mahakamani watu walicheka. Kuchukuliwa kwake ni kisababu tu cha kutaka kuwakomesha wale waliowahusudu au kuwaonea wenzao huruma hasa wanapokuwa katika mateso kama ya Matope. Katika jamii ya udhalimu wale ambao huongea kuhusu dhuluma iliyotendewa watu fulani, wao pia hunasibishwa nao na huchukuliwa kuwa wanawaunga mkono wanaodhalilishwa na kufanyiwa dhuluma.

Kisa cha Mtue kinatueleza mateso ambayo wafungwa wa kisiasa hupitia (tazama kitabuni ukurasa 83). Frantz Fanon (1963:216) akizungumza na mmoja wa watesaji alisema,

> Kitu ambacho huniumiza zaidi ni mateso. Hujui kwa nini haya yanatendeka. Wakati mwingine huwa wanawatesa wafungwa au watuhumiwa kwa muda wa masaa kumi mfululizo ... Nini hufanyika kwako unapowatesa? Huwezi kujua lakini huchosha. Watesaji hawa kweli hufanya utesaji kwa zamu. (*tafsiri yetu*)

Hakika Frantz Fanon anaeleza jinsi wafungwa huteswa na njia tofauti zinazotumiwa na watesaji hawa. Watesaji hawa ni watu ambao kwa maneno ya Wole Soyinka (1968) 'utu wao umekufa'. Frantz Fanon (1963:226) anaonyesha mifano ya mateso ya watuhumiwa hawa. Baadhi ya mateso haya husababisha

vifo kwa wafungwa. Wafungwa hawa hawatendewi haki kwa kuteswa usiku na mchana.

Mtue alipochukuliwa na Dubwana zake zilikuwa zimefika. Lakini lile Njemba lilimwambia "ni wachache sana tuwafafanuliao siri hii".

Katika kukilalia kitanda ni kujua siri za wateule. Siri ya kitanda ilikuwa ikitumiwa ili kuwapumbaza na kuwanyanyasa raia. Kuwanyima haki zao na kuwagandamiza. Mtue alielezwa kuwa,

> ... Ukweli ni kwamba amefanywa (Mteule) mpumbavu, hapo hatakubali na ataficha. Kwa hivyo ataeneza uongo. Na huo ndio ambao mpaka wa leo ndio umekuwa ukweli ... Na pia usisahau ni uwongo huu ndiyo udumishao masilahi yetu. (*ukurasa 85*)

Ni dhahiri shahiri kuwa baadhi ya washutumiwa hawa walisingiziwa uongo. Pia majina ya viongozi hawa wenye hila za uwongo waliitwa Bwagu kwa maana ya Pwagu na Bwaguzi kwa maana ya Pwaguzi. Kiisimu sauti /b/ na /p/ zinaweza kuleta utata au athari ya matamshi ya lugha ya kwanza. Kutokana na uwongo wao Mtue alitambua kuwa Mafuta ni ya aina moja na yalitiwa katika vyungu saba na kubandikwa majina tofauti. Jambo lililokuwa la kustaajabisha sana ni asili ya Mafuta. Mafuta haya yalikuwa mikojo ya paka. Hapa wateule waliojipaka mafuta haya walikuwa wanataka kudumisha hadhi yao. Haya yalikuwa maajabu ya kipekee. Mikojo ya paka kama mafuta ni jambo la kuaibisha. Wateule walitumia hila zozote kuwagandamiza wachochole.

Katika hicho kitengo cha utawala kulikuwepo na mambo yaliyochukuliwa kama siri. Watu walifanya bidii zozote wawezazo ili wapate mali. Maisha ya wenzao yalikuwa si chochote si lolote. Kitanda hakikuwa na msimamo kamili kutokana na kule kufungwa juu. Kingeliweza kuwekesuka kutokana na upepo. Hili ni jambo la viongozi wasio na msimamo (vigeugeu). Wakisema jambo halafu wanukuliwe na vyombo vya habari watakana na kusema, "Nimenukuliwa vibaya, sikusema hayo." Wateule wamekula yamini (ukurasa 87) ili wasifichue uwongo huu.

Baada ya kumfunulia Mtue ukweli wa mafuta walimweleza kuwa ilibidi wamwangamize. Mwandishi anasema "Na wewe ... inatulazimu tukuangamize kama yeye (Matope) kwa kuwa tumekufunulia ukweli wa siri kali yetu."

Neno hili 'siri-kali' linachukua matamshi ya kimzaha ya serikali. Kwa hivyo wadhalimu wako katika ngazi za utawala. Baada ya kuelezwa haya Mtue alishikwa na hofu. Lakini paliweza kutokea upepo ambao ulifungamana na ngurumo na zilizala. Kitanda kilianguka, nyungu pia zilianguka na kutawanywa, huku mikojo ya paka ikiishia mavumbini. Yaliyotokea kama zilizala, upepo mkali na ngurumo za radi ni harakati za wanamapinduzi waliokuwa wamechoshwa na kudanganywa huku wakinyanyaswa. Nguvu hizi za wanamapinduzi zilikuwa

nguvu kweli. Bwagu na Bwaguzi walijikunyata kwa hofu. Utawala wao ulikuwa umeangamizwa. Mara kulisikika sauti za MAJI TU! MAJI TU! Kwa mbali.

Huu ndio wakati ambapo wanaharakati waliunda makundi ya kisiri ya kutetea haki zao na kutaka mabadiliko, kwa mfano kulikuwa na 'pambana,' 'mwakenya' na 'Maskini Liberation Organization' – Shirikisho la ukombozi wa maskini (MLO). Huu unaweza kuwa wakati ambapo tulikuwa na harakati za kupindua serikali mwaka wa 1982. Ingawa maasi haya yote yaliangamizwa kulikuwa na jambo ambalo waliokuwa katika ngazi za uongozi walijifunza. Mwandishi akinukuliwa na Chacha (2003:47),

> Niliandika *Mafuta* mwaka 1984 wakati wa serikali ya ugandamizaji. Niliandika kuonyesha udhalimu mkubwa uliokuwepo wakati huo. Nilikuwa katika mapambano ya kuona kwamba nchi yetu inajitoa katika hali iliyokuwepo. Ilibidi niandike *Mafuta* kimafumbofumbo.

Maneno ya mwandishi yanatomelea mapinduzi yaliyoletwa na wanaharakati dhidi ya dhuluma za Bwagu na Bwaguzi, watu ambao wamechukuliwa kama ndumakuwili, wao ni 'viongozi' watesaji. Washiriki wao kama mama Shibe hawakuwa na la kufanya ila kusalimu amri, mwandishi anasema,

> Lao lilikuwa ni bumbuazi la kukumbana na bafe uso kwa uso. Mishindo ya MAJI Tu iliwafanya kuzirai na kuduwaa namna ya sanamu. Kwao kulikuwa mwisho wa dunia, kwa kuwa ukweli ukijidhihirisha, uwongo hujitenga. (*ukurasa 88-89*)

Ukombozi huu umeletwa na wengi. Mtue aliyekuwa kizuizini pia hakuweza kusadiki macho yake, jinsi uhuru ulivyoweza kupatikana. Machozi ya utu yalimtoka Matope. Mapinduzi haya yaliletwa na wengi. Mwandishi anasema,

> ... Hakuwa akitaka (Mtue) kusadiki macho yake, lakini usoni pake kulisimama akina Msati, Ti, Matope, Gweni, Mbeyu, Jasho, Pakacha, Nyepi, Zaitu na wengine wengi. Wote wakiwa na tabasamu nyusoni. Twende, kwani MAJI tumeyakomboa na kuwakaanga na mafuta yao wenyewe. (*ukurasa 89*)

Katika dondoo hili tunaona utawala wa kimabavu ukiangushwa. Pili waliodhalilishwa sasa wamejinasua kutoka katika minyororo ya udhalimu. Kwa desturi maji ni kitu muhimu kwa maisha ya binadamu. Kila kitu kinataka maji – mimea, watu na wanyama. Hivi kwamba raia walikuwa wamenyimwa na kuhiniwa mahitaji ya kimsingi kama chakula, mavazi, matibabu, ushirikiano, elimu, kazi na mahali pa kujisetiri dhidi ya baridi, jua na mvua. Jambo la tatu katika dondoo hili ni kuwa katika harakati lazima pawe na viongozi, ambao wanatoka katika matabaka tofauti za jamii husika. Kwa mfano Ti alitoka katika tabaka la wateule. Yeye ni mwanamke ambaye amechukua jukumu la kubadilisha jamii yake baada ya kuona jinsi wanajamii, kina Matope, Mtue wanavyonyimwa haki. Ti anaweza kufananishwa na Lanina katika tamthilia ya *Kilio cha Haki*. Hawa viongozi ndio walioweka vuguvugu moto wa harakati kuendelea kuwaka. Baada ya ukombozi tunaona watu waliowekwa kizuizini bila sababu wakiachiliwa. Wasema ukweli kama Matope hawakuamini.

Mwisho mwandishi anatueleza kuwa tatizo la ukombozi huwa ni wapi pa kuanzia. Chinua Achebe katika kongamano la wanafasihi huko Uingereza akinukuliwa na Ngugi wa Thiong'o (1972:52) alisema "... tunachotakikana kufanya ni kutazama nyuma na kujaribu kuangalia ni wapi tulipotoka, ni wapi ambapo muvua ilianza kutunyea?"

Ukweli wa mambo haya ni kule kwenye mkunazi. Ndipo Zuka na Kazamoyo waliporudi kumwuliza na kumsomea mwenye mkunazi anaeleza,

> Ni kivipi ni yeye tu ndiye mwenye mkunazi? Inakuwaje ni yeye tu aruhusiye zitundwe, azipangaye mafungu, ayape bei ...?" Ni yeye ... kila kitu ni yeye! Na ukiangalia tusio na mkunazi tu wengi.

Katika dondoo hili tunaona kuwa shida ya jamii ilianza na mfumo wa uzalishaji mali. Watu wachache ndio waliomiliki nyenzo za uzalishaji mali huu, kwa mfano mwenye mkunazi. Mfumo huu wa ubepari ukiambatana na ubwanyenye umewaacha wengi wakiteseka. Ili kulinda mwenye mkunazi serikali ilitumia sheria za ukandamizi na vitisho ili kuwanyamazisha kina Matope.

Walipokuwa wakirudi kwa mwenye mkunazi kuuliza maswali na kumsomea, walijikuta wako wengi wanafanya maandamano. Miongoni wa waliofanya mkururo wa mandamano ni mafalahi na wazururaji wasio na kitu. Kundi hili linaweza kuunga yeyote mkono kama tulivyosema hapo awali. Hili ni kundi lililopoteza matumaini. Haya mandamano yanayoongozwa na Zuka na Kazamoyo



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

yalinuia kuondoa ubwanyenye na ubepari ambao umeshamiri katika nchi za ulimwengu wa tatu.

Tukirejelea maneno ya Achebe, mvua ilianza kutunyea baada ya kuja kwa wageni waliokuja na istiimiri zao na baada ya kupata uhuru mambo yalibadilika zaidi. Watawala waafrika walipendelea uongozi na mali na kukaingia ukoloni mamboleo. Wanadamanaji walitaka kuvunjilia mbali ubepari na misingi ya mabaki ya uchumi wa kikoloni ili kuleta usawa wa kijamii, kisiasa na kiuchumi. Huduma za jamii zilikuwa zimezoroteka. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa huo ndio ujamaa ambao Mkangi anapigania.

Jamii ambayo Mkangi alitaka ni ile ambayo usawa wake wa kisiasa, kijamii na kiuchumi umefungamanishwa pamoja ili kuleta usawa wa kibinadamu kwa kuyashinda mazingara makali ya kimaumbile. Yeye (Mkangi) anaona matarajio yoyote ya haki za kijamii yakididimia mbele ya ubepari na umwinyi. Wazo aliloliona bora ni utaratibu wa kijamaa kama njia ya kipekee ya kuteka matarajio ya wengi. Hili ndilo Ngugi wa Thiong'o (1972:xiv) anasema,

> ... lazima tujitahidi kupata mfumo wa kijamaa ambao utaweza kufungua pingu zilizofunga mioyo na nguvu za watu wetu ili tuweze kujenga nchi mpya na kuimba wimbo mpya. (*tafsiri yetu*)

Maneno haya ya Ngugi wa Thiong'o yanarejelea mawazo ya Mkangi ambaye alisema lazima tusiwe na uwoga, tusiwe watu wa kunyamaa na kuogopa. Hii

ndiyo njia ya kuondoa uwele huu kwa kutovumilia kwa sababu vumilia ni jipu la ndani na huua.

Hali ya kutovumilia kugandamizwa ndiyo iliyozua mapinduzi na mabadiliko ambayo yalileta wengi katika harakati za ukombozi. Victor Hugo (1862:105) alisema;

> Hisia zilikuwa zimebadilika bila kujua kulingana na mabadiliko ya wakati. Waliokuwa watiifu wanabadilika kuwa wenye mawazo mapana na huru, pia hawa wenye mawazo mapana na huru walikuwa wanabadilika na kuwa wanademokrasia. (*tafsiri yetu*)

Mhusika Ti katika riwaya ya *Mafuta* alibadilika na kuchukua mrengo wa kushoto. Wanademokrasia ni wale ambao wanataka utu na haki. Ti angekuwa nyoka, ingesemekana kuwa ngozi yake imebambuka kwa sababu ya mabadiliko. Hisia zilibadilika kutokana na dhuluma walizotendewa.

Mabadiliko haya ni baadhi ya misingi ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa ambamo utafiti huu umejikita. Hadithi ambazo zimechunguzwa na utafiti huu zina misingi yake katika fasihi simulizi. Kama tulivyoona baadhi ni visasili, hurafa na zingine zimebuniwa ili kuhodhi maudhui mazito ya mwandishi. Visa vinavyosimuliwa vina uchangamfu wa juu ambao chini yake ni kilindini ambako kuna maudhui yenye kukabili masuala tofauti ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Pia kuna mikinzano, mitafaruku na harakati za kitabaka katika jamii ya mwandishi. Matukio ya jamii hii yameenda kinyume na kanuni za uhalisia wa kijamaa,

ambayo huweza kupinga, kunyonya au kunyonywa. Hili ndilo tatizo kuu ambalo Mkangi alitaka liondolewe katika jamii.

**HITIMISHO**

Hadithi ambazo utafiti huu umechunguza zimefungamana na kupinga unyonyaji na kugandamizwa wa kila aina. Hadithi hizi zimetumiwa kijazanda kama nyenzo ya kutolea maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Pili katika mazungumzo yangu na marehemu George Katama Mkangi tarehe 6-08-03 kabla hajaiaga dunia kwa ajali ya barabarani, alieleza kuwa mwandishi hukua na hukomaa kama mti, kwa hivyo aliweza kutoa mawazo yaliyokomaa ikilinganishwa na mawazo yaliyo katika riwaya yake ya kwanza *Ukiwa* (1975). Pia akinukuliwa na Chacha Mwita (2003:47) alieleza kwa nini aliandika kwa mafumbo (Tazama mtindo wake).

Mikinzano ya kitabaka imesaidia kuleta mapinduzi. Kwa mfano Zuka na Kazamoyo walipokuwa wanaenda kumsomea mwenye mkunazi hawakuwa pekee yao waliungwa mkono na tabaka la wazururaji. Maandamano haya ni mapinduzi ya kuleta mabadiliko katika jamii. Senkoro (1982:97) alisema,

> Mapinduzi ni kitendo cha tabaka moja, tabaka nyonywaji la wanyonge walio wengi, kuchukua madaraka ya kiuchumi na kisiasa kwa nguvu, kutoka kwa tabaka la kinyonyaji la mamwinyi na mabepari ambao ni wachache mno walinganishwapo na hao wanyonge.

Katika riwaya ya *Mafuta* matumizi ya nguvu yamehalalishwa kuwa njia ya kufyekelea mbali tabaka la wanyonyaji liishilo kwa matumizi ya nguvu, mateso na uongo. Mapinduzi haya ni yale ya kuziteka njia kuu za uzalishaji mali na madaraka ya kisiasa.

Tabaka la wazururuaji halikujua adui wao licha ya kushiriki mapinduzi. Mwenye mkunazi ndiye adui mkubwa wa jamii. Anamiliki nyenzo za uzalishaji mali. Jambo hili ndilo linalopingwa na wanaharakati ambao wanataka usawazishaji na ugavi wa mali ya asili na kuondoa ugandamizaji na ukatili. Waandishi wengine hutumia migomo kuonyesha kutoridhika kwa wafanyakazi. Mkangi ametumia maandamano na mikutano ya siri, kundi la wazururaji na wacheza kamari kuonyesha jinsi umaskini umeshamiri katika jamii hii.

Hadithi katika jamii zetu zilikuwa mali bia. Jambo hili limedhihirika katika riwaya ya *Mafuta* kutokana na hadithi zilizosimuliwa. Nyingi za hadithi hizi zilisimuliwa wahusika wakiwa pamoja kwa Msati. Licha ya madhumuni ya hadithi ya kuadibu na kuelekeza jamii katika mkondo unaokubalika na amali zake, kwa muktadha wa utafiti huu, hadithi hizi ni chombo cha kuwaleta wahusika ambao ni wanajamii pamoja ili waweze kujadili matatizo yanayowakabili. Kwa maoni ya Senkoro 1982:70 anasema kuwa ngano,

> "... Hujaribu kujenga utu bora na wakati huo huo ngano – viini
> hujibu maswali ya "kwa nini" na "kwa namna gani?"
> katika kueleza mambo yaliyotokea. Pia historia ya jamii
> ilielekezwa kupitia kwa ngano."

Katika dondoo hili Senkoro anaonyesha jinsi hadithi zilikuwa zikitumiwa hapo jadi. Lakini Mkangi katika kazi yake amezipa hizi hadithi hizi za jadi sura mpya, mweleko mpya na umbo jipya kwa kuziweka hadithi hizi katika maandishi yanayotumia sifa za fani asilia kubeba maudhui mapya.

Pili Mkangi amefaulu katika kuupa utanzu wa hadithi jukumu jipya kwa kutumia maelezo ya utanzu huu wa fasihi simulizi kutolea maudhui yake. Hadithi katika jamii zetu zilikusudiwa kuburudisha na kuliwaza. Lakini hadithi hizi za riwaya ya *Mafuta* zimepiga hatua mbele zaidi, zimechukua mwelekeo mpya unaoshughulika na kuyachambua mambo ya jamii ya kisasa. Masuala mbalimbali ya kisiasa, kijamii na kiuchumi yanayozikumba jamii za leo yameshughulikiwa kupitia kwa hadithi hizi. Mtindo huu uliotumiwa na Mkangi hauonyeshi tashwishi kuwa mambo yanayoelezwa yanachamba serikali. Mtindo huu wa kutumia utanzu wa fasihi simulizi pia umetumiwa na Ebrahim Hussein (1976).

Kwa mujibu wa mtazamo wa uhalisia wa kijamaa maadili ya kimsingi ya sera ya ujamaa ni juhudi za binadamu kujikakamua na kujikwamua kutoka kwa minyororo inayomfunga ya umaskini, ujinga, ukosefu wa chakula na mavazi na hifadhi dhidi ya baridi kali na mvua. Katika hadithi hizi Mkangi aliweza kushughulikia masuala haya kwa kuonyesha jinsi jamii inavyodhalilishwa na mfumo wa ubwanyenye na ubepari. Ameonyesha mbinu zinazotumiwa na watawala kuwakandamiza watawaliwa, kwa mfano raia wananyimwa Haki

ambayo ni jambo la kimsingi katika maisha ya wanadamu. Waliodai Haki walitiwa kizuizini. Mahakama ni vyombo vya ukandamizaji. Kupitia kwa masimulizi haya tunaona ujanja, udhalimu na propaganda zinazotumiwa na serikali nyingi za Kiafrika kukandamiza raia wake. Jambo lingine ni kuwa kupitia kwa hadithi hizi Mkangi ameliweka wazi suala la unyonyaji unaofanywa na waliomiliki nyenzo za uzalishaji mali.

Mkangi alitaka malighafi ya nchi nzima yatumiwe kwa manufaa ya wote katika jamii. Hadithi ya Matope ilishutumu maisha ya wachache ambayo ni ya raha ilhali wananchi wengi wanaishi katika ulitima. Msati anatoa mfano wa ujamaa kwa kuwaita pamoja wanaodhalilishwa. Huu ndio ujamaa uliopiganiwa na Mkangi. Kwa mujibu wa uhalisia wa kijamaa, usawa katika jamii ni jambo muhimu. Hufanya kila mtu kushiriki vilivyo katika maendeleo ya taifa kwa manufaa ya wote.

Hadithi ya mwenye mkunazi ni zao la ugavi mbaya wa mali ya asili. Mkunazi hautumiwi kwa manufaa ya jamii nzima. Kitula King'ei katika kazi yake iliyochapishwa katika *Weekly Reivew* 10th may 1996, *The Ethics of Socialism* alieleza;

> ... Maendeleo ya jamii hujengwa katika misingi kamili ya ushirikiano wa wanadamu wote na nyenzo zingine zote katika mfumo wa uzalishaji mali ... ambao hutumia kigezo cha maendeleo na hali ya maisha ya wanadamu katika jamii, kuliko kumilikiwa kwa mali ya jamii na mabepari wachache. (*tafsiri yetu*)

Maoni ya Kitula King'ei yanaenda sambamba na mawazo ya Mkangi kuhusu ujamaa. Mkangi anapiga vita ubepari na unyonyaji. Kwa maoni yake uovu ulio katika jamii umesababishwa na ubepari ambao unatokana na ugavi mbaya wa mali ya asili na kunyonywa kwa wafanya kazi na wakulima wadogo. Katika makala ya *Weekly Review* August 20th 1985, Mwalimu Nyerere alisema haya;

> Ujamaa haumaanishi ugawanyaji wa umaskini kisawa. Lakini maisha yangekosa maana na hadhi ikiwa uchumi wa nchi ungelikuwa mikononi mwa watu wachache matajiri ambao ni wenyeji au wageni. (*tafsiri yetu*)

Kwa muktadha wa mwanajamii huyu aliyeathiri fikira za Mkangi, maisha hayatakuwa na maana ikiwa uchumi wa nchi uko mikononi mwa mabwanyenye na mabepari wachache ilhali wakulima wadogo wadogo na wafanya kazi wa sulubu hawana chochote. Mkangi kwa upande wake anataka mabadiliko katika mfumo wa kisiasia na utawala ambao utatilia maanani walio wengi hasa walio katika tabaka la chini. Wazo hili la Mkangi linaweza kutekelezwa ikiwa wadhulumiwa wanajua na kutambua adui wao. Kwa kuwa tabaka la mafalahi halijui adui wao, ukombozi wao unakuwa mgumu kupatikana. Ukombozi huu unawezekana tu baada ya kupata uongozi ulio madhubuti na kuungana kwa wote wanaodhalilishwa chini ya ubepari na utawala wa kiimla.

Ingawa Mkangi alitaka kujenga jamii yenye usawa ambayo haingekuwa na wanyonyaji na wanyonywa, ni vigumu kuwaleta pamoja watu wanaodhalilishwa.

Safari ya Ti inaonyesha vikwazo vilivyokuwa njiani wakati wa kutaka kuleta huu usawa wa kijamii. Lakini pia alipendekeza njia za kupambana na mfumo huu wa kimabavu. Hapa anapendekeza mwungano baina ya walio katika tabaka la chini na lile lililo katika tabaka la juu ambalo halioni mambo yakiendelea vizuri. Kuna walio katika tabaka la uteule ambao 'wamechanuka' na hawaridhiki na jinsi mambo yanavyoendelea. Hawa ni kama Mtue na Ti, ambao waliweza kuungana na watu wa matope na kuleta mabadiliko.

Kwa kutoa mhutasari, riwaya ya *Mafuta* imetumia ufundi wa hali ya juu kuonyesha jinsi jamii ilivyo na jinsi Mkangi angelipenda jamii kuwa. Mkangi ameonyesha mabadiliko katika jamii yanaweza kupatikana tu kupitia kwa harakati za wanaonyanyaswa kuungana pamoja. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa, Mkangi amefaulu katika kutumia hadithi za fasihi simulizi kumulika masuala ya kisiasa, kiuchumi na kijamaa yanayozikumba jamii nyingi za Kiafrika.

## SURA YA 4

## 4.0 RIWAYA YA WALENISI

### UTANGULIZI

*Walenisi* (1995) ni riwaya ya tatu ya Mkangi. Jina la riwaya hii ni akronimu ya 'wale ni sisi, na sisi ni wale', kama anavyosema Mkangi katika riwaya hii. Walenisi ni nchi ya kimawazo ambayo ilitawaliwa na Wachuna. Wachuna ni kundi la wadhalimu na walowezi waliotawala Walenisi. Hawakuwa na utu na waliwatendea Walenisi unyama wa kila aina. Utawala wao ulikuwa wa mabavu. Wakati huo (wa utawala wa Wachuna ilijulikana kama 'W*aleni*' kirefu chake kikiwa "Wale na Waliwe". Baada ya Wachuna kutimuliwa nchi hii ilibadisha jina na kuwa *Walenisi*, yaani umoja usiobandukika. Kubadilisha jina si jambo geni. Baadhi ya nchi za Kiafrika na watu walibadilisha majina yao baada ya uhuru. Kwa mfano James Ngugi alibadilisha jina lake na kuwa Ngugi wa Thiong'o. Hili linafanyika ili kujinasibisha na nchi yao, hasa bara la Afrika, na pia kuonyesha mabadiliko yaliyokuwa yametokea katika nchi zao. Nchi kama Congo ilibadilisha jina na kuwa Zaire. Rais wao pia alibadilisha jina lake Joseph Mobutu na kuwa Mobutu Sese Seko Kuku Bandu wa Zabanga. Hali hii ndiyo iliyojitokeza kwa Walenisi, ili kudumisha na kusisitiza utu baina yao (Walenisi) waliweza kuweka kiambishi awali 'Mtu' kabla ya kutaja jina la mhusika. Hivi ndivyo wahusika wa riwaya hii walivyoweza kupata majina yao. Kwa mfano, Mtu-Bint-Fikirini, Mtu-Tabia, Mzee Mtu-Mwenzio, Mtu Bint Hekima, Mtu-Wazo na Mama Mtu-Maanani. Familia hii ndiyo iliyomlaki Dzombo baada ya kuepuka

kifo kupitia kwa njia ya sayari. Dzombo alitua katika nchi hii ya ajabu. Wazo hili la matumizi ya safari katika riwaya si geni. Katika riwaya ya *Kusadikika,* mwandishi Shabaan Robert alitumia wajumbe kwenda safari ili kutalii maendeleo yaliyokuwa yakitendeka katika nchi zingine. Wajumbe waliotumwa kwa safari hizi walihitajika kuwasilisha matokeo ya safari zao pindi warudipo. Kutokana na utawala wa kidhalimu ulioendelezwa na wahusika kama Boramimi, ambaye alikuwa Mudir wa Sheria, waziri Mkuu Majivuno na viongozi wengine walioshikilia ngazi za utawala, hawakupenda yaliyoletwa na wajumbe kutoka nchi hizo za kigeni. Wazo hili la taswira ya safari limetumiwa katika riwaya zingine kama Mohamed S. Mohamed *Nyota ya Rehema* (1976), Ngugi wa Thiong'o *Petals of Blood* (1977), *Matigari* (1987), Mohamed S. Ahmed *Utengano (1980),* Shabaan Robert *Adili na Nduguze (1952)* na *Kusadikika (1951);* Hata vitabu vya Kiingereza vilivyotafsiriwa kwa mfano Janathan Swift *Safari za Gullive,* (1963), Sofokile *Mfalme Edipode* (1971). Vitabu hivi ni baadhi tu ya riwaya zilizoshughulikia taswira ya safari kwa maksudi tofauti.

Katika riwaya ya *Walenisi,* safari ya Dzombo ilimpeleka hadi nchi ya Walenisi, baada ya yeye kukiongoza chombo kilichokuwa kimedhamiriwa kumwangamiza baada ya kuhukumiwa kifo kwa sayari. Safari hii ni sawa na zile zinazojitokeza katika riwaya ya *Kusadikika,* ambazo zilidhamiria kuleta mabadiliko. Mahojiano baina ya Mkangi na mtafiti, na baina ya Mkangi na Chacha (2003:47),

yalionyesha kuwa uandishi wa Mkangi uliathiriwa na marehemu Shabaan Robert, kama Mkangi mwenyewe anavyosema;

> ... Nilikuwa nimevisoma vitabu vyake vyote hasa *Kusadikika*. Kutokana na kupenda maandishi ya Robert niliutumia ule muundo wa kuwa katika dunia nyingine. Robert alipoandika *Kusadikika* na *Kufikirika*, vyote vilikuwa na muundo wa kufundisha wananchi. Mawazo na maoni yake ya jamii nzuri yalikuwa muhimu sana. Lakini wakati wake asingeweza kuyaandika kwa sababu ya ukoloni. Aliogopa kuandika mambo maovu ambayo wakoloni walihusika nayo na ambayo walikuwa wakiyadumisha wakati huo. Mimi nilichukua ile mbinu ya Shabaan Robert na kusafiri mahali fulani. Lakini mawazo yangu wakati wa *Walenisi* yalikuwa tofauti kabisa na yale ya Robert.

Jambo lililo muhimu ni kuwa, riwaya ya *Walenisi* iliandikwa wakati mwandishi alikuwa kizuizini huko Naivasha kwa muda wa miaka miwili (1986-1988), kama mwandishi mwenyewe anavyosema;

> "Nilipata fursa ya kuandika kitabu hiki cha Walenisi nilipokuwa kizuizini. Wakati unapokuwa kizuizini ni sawa na kuwekwa katika dunia nyingine. Kule kuwekwa kizuizini kulinisaidia kwa kiwango kikubwa ..."

Si ajabu kuwa katika uandishi huu wa *Walenisi* Mkangi alikuwa anazungumzia juu ya dhuluma na mateso katika nchi yake ya Kenya katika kipindi fulani cha kihistoria. Kwa mfano wakati wa Mau Mau, wakati wa utawala wa Kenyatta na utawala wa Moi.

Watu wengine waliomuathiri Mkangi kimawazo ni kama Frantz Fanon, Nyerere, Karl Marx, Paul Frere, Rodney na Yesu Kristo. Wengine ni wanamapinduzi kama Mao Tse tung, Hochimin, Fidel Castro, Sheikh Vera na Augustino Neto. Pia mtindo wa Yesu Kristo wa kutoa maelezo kwa njia ya hadithi na usawa mbele ya Mwenyezi Mungu, umeathiri uandishi wa *Walenisi* na *Mafuta*. Mkangi anataka usawa katika jamii. Mawazo haya ya Mkangi yanatuelekeza katika nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Mawazo yake anayatoa kupitia kwa hadithi anazozitoa katika kazi zake. Hadithi hizi zinachangamsha na kutoa mafunzo mwafaka kwa jamii yake. Senkoro (1982:116) anasema,

> Hadithi hizi ... zinatumia mtindo wa 'mtoa michapo', unazozifanya zikumbukwe kwa urahisi. Mithili ya mafumbo-mifano (parables), visa vinavyosimuliwa vina uchangamfu wa juu ambao chini yake kunatokota maana nzito zenye kukabili masuala mbalimbali ya kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi.

Hadithi ambazo Mkangi alitoa ni zake za kubuni. Katika mazungumzo baina ya mtafiti na Mkangi, alinitolea hadithi ya majitu yaliyokuwa yakiwala watu. Lakini baada ya majitu kuuwawa na kuchomwa, majivu yalibakia. Wenyeji waliosalia waliyapiga majivu kwa fimbo na kuita jina la mtu aliyeuliwa, hapo yeye alifufuka. Hili alisema ni ujenzi wa jamii mpya. Mkangi anatumia hadithi hizi kama nyenzo au jazanda kwa kutoa maudhui yake. Pili jazanda hizi zinaficha ukweli wa mambo ili majasusi na vibaraka wasielewe kuwa riwaya hii inaponda serikali na mfumo wa umwinyi na ubepari.

Katika riwaya ya *Walenisi* msimulizi wa hadithi alifanya uchunguzi katika maktaba ya Walenisi na kupata visa hivi vilivyotendewa Walenisi na utawala mbaya wa Wachuna. Uchunguzi huu, kwa maoni ya Wamitila (2003:10) ni;

> ...ni historia ambayo inaweza kuangaliwa kama mtazamo mpana wa historia ya binadamu pamoja na ukuzaji na uendelezaji wa mifumo mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Dzombo anatambua jinsi wakati fulani huko nyuma nchi hiyo ilivyotawaliwa na viongozi waliokuwa dhalimu na wa kiimla. ... Hata hivyo raia waliungana na hatimaye kuuangusha mfumo huo mbaya na kuanzisha utawala unaowajali watu wote bila ubaguzi katika misingi yote ile.

Baada ya uchunguzi huu Dzombo anafunga safari kurudi kwao Jehanamu (Hii ni taswira ya ulimwengu wa mwandishi ambako udhalimu ulikuwa umekithiri) ambako angeliweza kuleta mabadiliko. Alifunga safari hii pamoja na mke wake mja mzito Mtu Bint Fikirini. Dzombo alipokuwa huko kwa Walenisi, alijifunza umuhimu wa upendo, ushirikiano, usawa katika jamii baina ya wanajamii na utu. Dzombo alihiari kuja kuzindua jamii yake. Mkangi anatoa muhtasari wake kwa kusema;

> "Walenisi wenzangu, tungekuwa vilima, hatungekuwa na matatizo lakini sisi si vilima. Tuna uhai na tunawasiliana. Lengo na nia ya ustaarabu wetu ni kurahisisha maisha yetu siku baada ya siku. Tujipongezeni kwa hatua ambazo mpaka wa leo tumezipiga. Tulianza kwa kutaifisha udongo, kugeuza mfumo wa uchumi wetu na kuleta siasa zisizo za umwinyi, ubepari na ubwanyenye. Hii ilikuwa ni mipaka ya kijamii nasi tumeisukuma nyuma ili kujiendeleza zaidi. Hatujarudi nyuma katika nyanja ya ufundi, uhandisi, teknolojia na sayansi kwa jumla. Vyote hivi tunazidi kuvitumia katika harakati za kuleta

> usawa, mapenzi na ufanisi kati yetu. Hakika vita vya kusukuma nyuma mipaka ya mazingira havitakoma."
> *(ukurasa 211-212)*

Maelezo haya ya Mkangi yanaenda sambamba na mihimili ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Kutokana na maelezo haya Mkangi alitazamia uhalisia wa mambo katika jamii yake; anataka mabadiliko. Katika muktadha huu jamii yake ingeliweza kumulika masuala ya kijamii ambayo yanahusu mambo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, na kutoa utatuzi. Hii ndiyo ingekuwa njia ya kupambana na mazingira makali na kuufanya ulimwengu mahali bora pa kuishi kwa mwanadamu. Pia anaonyesha jinsi unyonyaji ni haramu na pia ni njia ya kudhalilisha umma na kuugandamiza.

Dzombo anapoenda kuzuru kiwanda cha Trimi anapewa kijitabu cha maelezo na mkurugenzi Mtu-Bint Fikirini. Katika utangulizi wa kijitabu hicho aliweza kusoma jukumu na uhusiano wa kiwanda hiki na viwanda vingine katika ujumla wa uchumijamii wa Walenisi. Maelezo katika kijitabu hiki yanasema;

> Nchi hii ni yetu na uchumi hauna budi kuwa wetu. Kati yetu hakuna mwinyi, kabaila wala bepari. Sote tuko sawa. Kwa hivyo ... Utajiri wote na mali yote ni yetu sisi umma. Na umma ni wewe ... ukipuuza mali ya umma, wa kwanza unayempuuza na kumzorotesha si mwingine bali ni wewe mwenyewe binafsi.
> *(ukurasa 139 - 140)*

Maelezo haya yanasisitiza wanadamu kuwa sawa. Hii ni hali ya ujamaa ambapo jamii hushirikiana kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya kuja kwa Wachuna na istiimari zao. Pia mwandishi anataka jamii iliyokamilika na isiyokuwa na matabaka. Anaeleza;

> Huko kiwandani, akawa ameona uelewano na ushirikiano wa hali ya juu sana. Hakukuwa na nyapara wala mpagazi. Kila mtu alitimiza wajibu wake katika imani ya kujua kwamba alilolifanya lilikuwa la maana na muhimu katika ujumla wa harakati za kuendeleza jamii. *(ukurasa 149)*

Maelezo haya pia ni msingi wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa kama inavyoelezwa katika umarxi kwamba jamii zisiwe na matabaka. Ingawa wazo hili yeye mwenyewe (Mkangi) anakiri ni gumu kwa kusema kuwa;

> Hapo kiwandani aliona wafanya kazi waliovaa nguo zilizofanana (sare). Haikuwa rahisi kwake kumjua nani ni mkubwa na nani ni wa chini kama ilivyo kawaida huko kwao ... kwa kuvaa sare viwandani, Dzombo hakuwa na budi bali kuuliza msaada kwa yeyote yule aliyekutana naye. *(ukurasa 98)*

Katika uhalisia wa mambo lazima jamii au familia iwe na msemaji wao au kiongozi. Maoni ya mwandishi ni kuwa hata serikali haitakikani kwa sababu ni chombo cha ugandamizaji. Maelezo haya ya Mkangi yamejikita katika siasa ya ujamaa. Kwa hivyo, serikali ambayo Mkangi anapendekeza ni ile ambayo ni tofauti na serikali ya Wachuna, na ambayo inazingatia haki na malighafi ya nchi kutumiwa na umma kwa manufaa ya wote.

Baada ya kufanya uchunguzi katika Maktaba Kuu ya Walenisi, Dzombo aliweza kuibuka na hadithi hizi:

1. Hadithi ya Mapacha
2. Hadithi ya Maskini Jeuri
3. Hadithi ya Wachuna
4. Hadithi ya Mabavu
5. Hadithi ya Moto
6. Hadithi ya Mchawi/Mganga
7. Hadithi kuu ya Dzombo

Katika sehemu zinazofuata tutajadili hadithi tofauti kama zinavyosimuliwa na Dzombo baada ya kufanya utafiti katika Maktaba Kuu.

### 4.1.1 HADITHI YA MAPACHA

Hadithi hii inahusu wasichana wawili walioitwa Medza na Chihenyo. Wasichana hawa walizaliwa mapacha na walipendana sana. Walipozaliwa walikuwa wamekumbatiana mithili ya wapenzi. Ndipo kisa hiki kikaitwa mapacha.

Walitenganishwa walipokuwa nje baada ya kuzaliwa. Pili walisisitiza waolewe siku moja. Arusi hii ndiyo iliyokata kitovu kilichokuwa kimewaunganisha kwa sababu kila mmoja aliendа zake na bwanake. Wote walijifungua watoto wakati mmoja. Mtoto wa Medza aliitwa Tabu au Metabu kwa ufupi wa jina la

mama yake Tabu. Chihenyo akawa mamake Furaha au Mefuraha. Ufupi wa mamake Furaha. Haya ni majina ya majazi. Ajabu ni kuwa wakati Furaha na Tabu walipokuwa wanakua, pacha hawa (Chihenyo na Medza) pia walishika mimba. Mimba zao zilipokuwa miezi sita, majaribio magumu yaliwasibu. Medza alipokua amekalia kibao akijaribu kumfumia Tabu kirinda kutokana na mabaki ya matambara ya mavazi yake ya harusi ili kusitiri mwanawe uchi na baridi, Tabu alishikwa na ugonjwa na akaanza kutapika, kuhara, kupapatika na kujikojolea. Medza pasipo na lingine, alimzoa mtoto wake na kumkimbiza katika zahanati kwa miguu. Alifika zahanati akiwa amechoka na amejaa matapishi na kinyesi. Msimulizi anasema;

> Hapa palikuwa ni pa huduma ya kwanza. Hakuwa wa kwanza hapo. Alikuta na kuungwa na wengine wengi wa aina yake kitabaka. Mgonjwa alihitajika kungojea hapo kwa huduma na uchunguzi. Baada ya hapo ndipo ilipojulikana ikiwa angelazwa ama la. Wakisubiri Metabu aliona sakafu imejaa wagonjwa waliotapatapa kwa uchungu. Migumio yao ya maumivu ilisikika na kupajaza hapo pote. Wagonjwa wengine walionekana wamelala tuli pale sakafuni na macho yasiyo na tamaa kutumbuka. Mstari wenyewe ulijikokota kwa mwendo wa kinyonga. *(ukurasa 182)*

Ugonjwa ulimzidia Tabu. Roho ilimwenda mbio na kutapika mara kwa mara. Mama alikaa foleni na mtoto bila kupewa huduma. Medza alihuzunika sana mtoto wake alipokuwa anaumwa lakini hakuwa na namna yoyote. Baada ya Tabu kuangaliwa, daktari aligundua kuwa Tabu hakuwa na kitu tumboni, aliugua utapia mlo na marasimi. Huu ni ugonjwa wa kukosa lishe bora.

Ukosefu wa lishe bora ni hatari kwa watoto wachanga. Tabu alikula tunguja-mwitu wakati njaa ilikuwa haivumiliki. Hizi tunguja ni matunda yenye sumu. Daktari alimkemea Medza kwa kusema kuwa hampi mtoto wake lisho bora. Medza alitaka kumjibu lakini alinyamaza. Msimulizi anasema;

> Kama ningekuwa nacho ningemnyima mwanangu? Lakini hakutamka hayo. Badala yake alikaa kimya tu kama ilivyo desturi ya watu wanyonge kama yeye wakiwa mbele za watu wa vyeo. *(ukurasa 184 - 185)*

Tabu hakuweza kulazwa kwa ukosefu wa vitanda. Hospitali hata haikuwa na 'drip'. Mwuguzi alipendekeza mama aende kuinunua katika maduka ya kuuza dawa. Lakini la kusikitisha ni kuwa Medza hakuwa na pesa za kununua dawa hiyo. Kwa kumtia moyo, daktari alimwambia kuwa angejaribu kesho. Medza alipokuwa njiani peke yake akirudi nyumbani Tabu alikata roho. Mama alijawa na biwi la simanzi. Mumewe Medza alikuwa ameajiriwa kazi ya mlinzi wa usiku, kumlinda Mchuna mmoja ili aweze kulala bila kero za usiku.

Kwa upande mwingine, Dzombo alinakili kisa cha Chihenyo. Katika kisa hiki Furaha alichomeka alipovutiwa na sufuria iliyokuwa mekoni na akaiburuta. Alichomeka vibaya sana. Lakini familia hii ilikuwa ya tabaka la juu. Daktari alipigiwa simu na pindi mtoto alipopelekwa huko mambo yalikuwa yameandaliwa tayari. Kama kawaida watu wenye uwezo wa kiuchumi huwa na daktari wao wa kibinafsi. Furaha alipelekwa hospitalini kwa gari na kutibiwa.

Daktari anasema;

> --- ni nguo zake zilizomsaidia na kumkinga ama angekuwa amapeta majeraha mabaya zaidi--- mshtuko ndiyo uliompumbaza kwa hivyo nimempa dawa ya kumlaza. Kitu cha kuchunga ni kuona kuwa nguo zake hazimgandami pale alipochomeka--- Nitawatembeleeni kesho asubuhi nione amelalaje, lakini ikiwa kutatokea mabadiliko yoyote, msikawie kunipigia simu". *(ukurasa 186)*.

Furaha alipata matibabu ya hali ya juu Aliweza kusoma na hata kuhitimu kuwa daktari. Kwa upande mwingine mazingira makali yalikuwa yamewabana Medza na mwanawe Tabu. Tabu alikufa kabla ya kufika umri wa miaka mitano. Hadithi ya mapacha iligusa mioyo sana. Hata ikawekwa kama kumbukumbu katika Maktaba kuu. Hadithi hii ilionyesha hali ya utabaka kupitia kwa ndoa. Kwa mujibu wa hadithi hii huduma za matibabu zilikuwa tofauti. Huduma za afya ni muhimu sana katika nchi. Huwa ni jukumu la serikali kutoa huduma za afya kwa raia wake. Katika utawala huu wa Wachuna, hospitali za wanyonge zilikosa dawa, wagonjwa walitapakaa sakafuni nzima na wahudumu walikosa utu.

Jambo kama hili si geni hapa kwetu nchini Kenya. Kwa muhtasari huduma zilikuwa hafifu. Msimulizi alitoa picha za Wachuna aliposema,

> Nokolani za Wachuna zilijulikana kuwa safi, dawa tele, vifaa vingi, waganga, wauguzi na wasaidizi tele, shwari na kutokuwa na msongamano. Kila mchuna hakukosa kuwa na daktari wake wa kibinafsi. Huyu alimtibu kwake nyumbani na hata akiwa nokolani. Kwa Wachuna, madaktari wa kibinafsi ndiyo waliokuwa hirizi zao za viunoni. *(ukurasa 178)*

Tofauti hii ya kitabaka ndiyo Dzombo alitaka kusawazisha. Kusiwe na sehemu fulani ambayo inadhulumiwa. Huduma za afya zilionyesha ubaguzi, kuhusiana na jinsi zilivyotolewa. Tukirejelea ukweli wa kihistoria Walter Rodney (1989:26) anasema;

> Watoto wengi wa Kiafrika hufa kabla ya kufikia umri wa miaka mitano. Ukosefu wa madaktari ndio hurudisha nyuma juhudi za kupambana na maradhi. Katika nchi ya Italia, daktari mmoja anahitajika kuhudumia watu 580, Niger ni watu 56140 kwa daktari mmoja. Jamhuri ya Czech daktari mmoja kwa watu 510, huko Chad daktari mmoja huhudumia watu 73460.

Ripoti ya *inteneti (2003) w.w.w. teh express. Com.* kwa mada *Doctors: To many, to few?* Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani ulionyesha kuwa katika nchi ya Tanzania daktari mmoja huhitajika kukudumia watu elfu ishirini na sita. Lakini baadaye uchunguzi mwingine ulifanywa na Bugando University College of Health Science (BUCHS) kutoka Tanzania ulionyesha kuwa Kenya na Uganda wana madaktari wengi kuliko Tanzania. Nchini Kenya, uwiano wa daktari na wagonjwa ni 1:7,000, Nchini Uganda ni 1:6000 na Afrika Kusini ni 1:2000.

Maelezo haya yanatoa uwiano na jinsi huduma za Afya zilivyo katika nchi nyingi za bara la Afrika. Tukirejelea riwaya ya *Walenisi*, Tabu anakufa kwa sababu huduma za matibabu ni duni na wagonjwa lazima wagharamie huduma hizo. Medza mamake Tabu hakuwa na pesa za kugharamia matibabu ya mtoto

wake. Inambidi arudi na mtoto nyumbani hata bila kupewa dawa yoyote. Jinsi hali yake ya ulitima ilivyokuwa basi si rahisi kupata matibabu. Afya ya jamii ni kitu muhimu. Taifa haliwezi kuendelea bila kuwa na raia wenye afya. Huduma za afya katika ulimwengu wa tatu ni wazo ambalo lingali ndotoni kwa wingi. Inaaminika kuwa serikali ndiyo ingetoa huduma kwa raia lakini jambo hili haliwezekani. Katika muktadha wa riwaya ya *Walenisi* raia wa kawaida walinyanyaswa na kudhulumiwa. Madaktari wamejaa ufisadi na uroho – hasa walipodai kiasi kikubwa cha pesa kwa kufanya upasuaji. Wazo hili la ufisadi linadhihirika pia katika riwaya ya Mohamed *Nyota ya Rehema* (1976). Kwa maoni ya Mkangi ni kuwa Wachuna waliweza kueneza uchuna wao na kudhalilisha watawaliwa kwa kila njia.

Hali hii ya matibabu iliyosawiriwa katika riwaya ya *Walenisi* inatoa ukweli wa mambo katika nchi nyingi za Kiafrika. Ripoti ya intaneti w.w.w. statehousekenya.go.ke inamnukuu Waziri wa Afya nchini Kenya Mheshimiwa Charity K. Ngilu kwa kusema;

> Katika juhudi za kutoa huduma ya matibabu kwa mamilioni ya Wakenya, serikali ilitangaza kuwa itatoa huduma ya bure katika zahanati za serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2004... wagonjwa watalipa pesa ya usajili pekee. Lakini watoto chini ya miaka mitano hawatalipa chochote. Serikali imetenga shilingi bilioni 4.1 (US$51.5 milioni) ili kutekeleza kuduma ya bure ya afya katika kipindi cha mwaka 2004/2005... wachochole wanaokisia kuwa milioni tisa hawana uwezo wa kupata huduma yoyote ya afya. Hata wale wanaoishi mita mia kutoka kwa zahanati au hospitali

> hujifia nyumbani kwa sababu hawawezi kugharamia huduma za afya. Vifo vya watoto wachanga walio chini ya miaka mitano vimeongezeka kwa asilimia thelathini (30%) tangu miaka kumi iliyopita. Vifo hivi viliongezeka kutoka watoto sitini (60) mwaka wa 1989 hadi vifo themanini na tisa (89) mwaka wa 2003 kwa kila watoto elfu moja (1000) wanaozaliwa hai. Pia vifo miongoni mwa watoto walio chini ya miaka mitano viliongezeka kutoka themanini na tisa (89) mwaka wa 1989 hadi mia moja na kumi na nne (114) mwaka wa 2003, kwa kila watoto elfu moja. Waziri aliendelea kusema ili kuboresha afya nchini serikali imeanza kukarabati sekta ya huduma za matibabu. Tayari kuna mswada Bungeni kuhusu kuanzisha huduma za Bima ya Afya kwa Taifa.

Maelezo ya waziri ni njia moja ya kutaka kuonyesha jinsi huduma za afya zilivyo. Ili kulinda maisha ya watoto ni muhimu kutoa chanjo kwa watoto, kuwapatia lishe bora na jinsi ya kukinga na kuzuia magonjwa mengine kama malaria, homa ya matumbo, kichocho na kadhalika. Jambo hili la waziri litatimu ikiwa ufisadi utaondolewa. Uhaba wa chakula ni tatizo lingine linalokabili nchi hizi za ulimwengu wa tatu. Kuhusu matumizi ya chakula katika nchi za ulimwengu wa tatu, Rodney (1989:25) anasema;

> --- kila mtu huhitaji kiasi fulani cha chakula kwa siku ambacho hupimwa kupitia kwa 'kalorisi' kiwango kinachotakikana ni kalorisi 3000 kwa siku. Nchi nyingi za Kiafrika hazifikii kiwango hiki--- kiwango cha protini iliyo katika vyakula vinavyoliwa ni muhimu sana. Lakini katika nchi nyingi za Kiafrika zina ukosefu wa vyakula vyenye protini. Hii ni kusema kwamba chakula kingi kinacholiwa huwa kina wanga (starch) nyingi na protini kidogo.
>
> (Tafsiri yetu)

Watoto wachanga chini ya miaka mitano wakila vyakula nyenye wanga nyingi hupata ugonjwa wa utapia mlo na marasimasi. Dalili za ugonywa huu ndizo alizokuwa nazo Tabu.

Hapa nchini Kenya, huduma za matibabu zilikuwa zikitolewa bure tangu nchi hii ilipojipatia uhuru wake kutoka kwa wakoloni hadi mwaka wa 1989 wakati waliposhinikizwa na mataifa ya kimagharibi kuunda mikakati mipya ya kiuchumi, ndipo ikazua mfumo wa kugawana gharama katika huduma za afya. Kutokana na kuongezeka kwa hali ya umaskini hapa nchini idadi nyingi ya wakenya walio milioni 31.6 hawapati huduma bora za matibabu kama ilivyoelezwa na waziri. Jambo la nne ni kuwa madaktari na wauguzi hawajali kazi zao. Msimulizi katika riwaya ya *Walenisi* anasema;

> Hali hii ilizidishwa na wauguzi, madaktari na wafanya kazi wote kwa jumla, kujiona, kukosa nidhamu na moyo wa kiutu. Kwa upande wao, wagonjwa hawa hawakuhalisi kuendewa mbio. Kwa hivyo wakati wa chai ulipofika, wote walipatoweka bila kigegezi rohoni. Hiki ni kitendo chao cha kawaida kama vile kula na kwenda choo. *(ukurasa 183).*

Wazo hili la msimulizi ni uhalisia wa mambo katika zahanati na mahospitali ya hapa nchini Kenya.Mkangi alipoandika riwaya ya *Walenisi* alilenga jamii nyingi za ulimwengu wa tatu. Mkangi aliona kuwa njia ya kipekee ya kuondoa ubaguzi huu, dhuluma na kunyanyaswa, ubepari na umwinyi, na mali ya asili kumilikwa na watu wachache, ilhali wengi hawana chochote, alipendekeza mfumo wa

ujamaa. Mfumo ambao kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa hakutakuwa na ubaguzi na dhuluma. Mambo mengi yatakuwa sawa.

Kwa kufunga tangalachi Mkangi alitumia sanaa kama kioo kumulika masuala halisi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika jamii yake. Hili ni jambo linalochukuana na maelezo ya Plekanov katika *Marxist Esthetics* (1973:12) ambako fasihi hutekeleza jukumu la kijamii la kuzindua, kuhamasisha na kuweka wazi uhalisi wa mambo. Huduma za afya huwa duni kwa sababu ya umaskini, ufisadi na ubaguzi baina ya watawala na watawaliwa. Watawaliwa si chochote si lolote. Kisa hiki cha mapacha ni miongoni mwa shida nyingi zinazokabili jamii. Msimulizi anasema;

> Kisa hiki kilikuja kikawa--- kilichowazindua Wawalenisi. Kiliwafanya kutambua kuwa uadilifu si kwa kuzaliwa ama kwa bahati mbaya, bali ilikuwa kwa sababu ya uhusiano wa kijamii uliodunishwa na sheria za utawala wa kichuna--- kilikuwa kisa kilichoanzisha harakati ambazo mwishowe zilifanikiwa kwa kuwatimua Wachuna na uchuna wao. *(ukurasa 186)*

Mwandishi anapendekeza harakati na namna fulani ili kuondoa dhuluma katika jamii. Harakati hizi ndizo zitakazoleta usawa wa kijamii, (kisiasa, kijamii na kiuchumi). Uanzishaji wa karakati ili kubadilisha mfumo wa uzalishaji katika jamii si jambo geni. Harakati hizi ndizo huleta mabadiliko au mapinduzi.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Kwa muhtasari hadithi hii ya mapacha inaonyesha ukosefu wa huduma za kimsingi kama chakula, mavazi na huduma za afya. Pili, kisa hiki kilionyesha utabaka katika jamii na athari zake, na ubaguzi baina ya Wachochole na wenye nguvu za kiuchumi. Katika kisa hiki ndugu wawili wanaweza kutengana kama ardhi na mbingu. Katika misingi ya uhalisia wa kijamaa ungelitaraji ndugu hawa kushirikiana kwa vyovyote kama ulimi na mate. Lakini msimulizi anatuchorea mazingira makali ambayo yanaonyesha utengano na kutokuwa na utu. Ushirikiano wa kindugu haupo kwa sababu mabepari huthamini pesa zaidi kuliko utu na huduma bora huwaendea walio katika tabaka la juu. Hili ni tabaka ambalo humiliki nyenzo za uzalishaji. Kisa hiki kinaonyesha maisha kwa njia ya ulinganifu.

### 4.1.2 HADITHI YA MASKINI JEURI

Kadhia ya Maskini Jeuri ni kumbukumbu ya matukio fulani yaliyomsibu Dzombo na rafiki yake walipokuwa huko Jehanamu. Katika kadhia hii Dzombo alikuwa amechezewa shere na rafiki yake Maskini Jeuri. Siku ya kadhia hii Dzombo alienda kutafuta mafuta ya taa na kuyakosa kwa sababu mabepari walikuwa wamehodhi mafuta na bidhaa zingine ili wapandishe bei na kupata faida maridhawa. Jamii hii haikuwa na maduka ya wanyonge. Mabepari wangelienda kuwanyonya maskini kwa kila njia na kuwadhalilisha kwa vyovyote. Dzombo anawaza kunyimwa mafuta kwa sababu maskini hana namna ya kujiendeleza zaidi au mahali pengine pa kwenda. Uhusiano huu baina ya maskini na

mabwanyenye ndio unaosababisha ukosefu wa bidhaa madukani na kuongezwa kwa bei. Pili wenye bidhaa hizi huwabagua wateja wao wanaotoka katika tabaka la wanyonge. Waliouziwa mafuta ni wale wenye vyeo, mamlaka na uwezo. Hali hii ya utabaka inamwuudhi Dzombo sana, hasa aliposisitiza auziwe mafuta. Mwuuza mafuta alimwambia;

> Nimeshakwambia hakuna – ala ! Akakodolewa macho.
> "Sikiliza bwana," akawa anamsihi "ikiwa ni pesa, basi hata mimi nina---"
> "Usinisumbue! Ondoka hapa haraka – ama wataka nikuitie polisi?"
> Hakutaka--- aliondoka kama vile jibwa lifanyavyo baada ya kumwagiwa maji. *(ukurasa 70)*

Katika maelezo haya kuna mambo matatu yanayojitokeza. Kwanza Dzombo hakuuziwa mafuta licha ya kuwa na pesa. Mabepari wanahodhi bidhaa ili waziuze kwa bei ghali na kupata faida zaidi. Jambo pa pili ni kuwa wanataka kuwa na ukirtimba katika mauzo ya bidhaa ili wawauziwe watecha kwa bei wanayoitaka ili kupata faida ya juu zaidi. Jambo la tatu ni kuwa polisi walitumiwa kama chombo cha ugandamizaji, wachochole walikuwa wametiwa hofu na polisi. Polisi hao walikubali haraka madai ya wenye uwezo wa kifedha. Katika jamii zetu polisi hujitokeza nadra sana baada ya mnyonge kudhulumiwa hata kama wamepigiwa ripoti. Hawadhamini kazi yao. Wao huona yale watakayopata kando na ujira wao wa mwisho wa mwezi. Pia wao hupenda kulinda maslahi ya wenye mali – wanyonyaji. Haya matatu yanafanya Dzombo kijinyima haki yake ya kudai kuuziwa mafuta. Mkangi akatueleza katika riwaya

hii kwamba wanyonge hunyimwa hata kile ambacho ni haki yao. Pia anatuonyesha kuwa utawala wa mabavu hutumia polisi kama chombo cha kuwalinda ili waendelee kudumisha masilahi yao. Wachuna nao walitumia polisi ili kulinda maslahi yao. Tawala nyingi barani Afrika zinatumia mabavu kwa kutumia polisi kama chombo cha kugandamiza wanyonge. Mkangi anasema;

> Pia waliunda vikosi vya kila aina – kutoka kwa kitaifa mpaka vya kibinasfi. Vyote hivi vikiwa na silaha zao za kutisha, vilionyesha umma kwa makusudi, kwenye maandamano ya kusherehekea utawala wao. Wenyeji wenyewe hawakukosa kuupata ujumbe huo. Ujumbe wenyewe wakaubatiza "H F F U" yaani "Hebu Fanya Fujo Uone".
> Kwa sababu hii, figa la uoga likafanikiwa sana mpaka ile tabia ya kukebehi na kukejeli binadamu ikachukuliwa kama ndiyo ya kistarabu. Umma ulitiwa hofu zaidi kwa Mabavu kutoa sheria, na sheria kuzua magereza.
> *(ukurasa 188)*

Mwisho Mkangi anapendekeza jinsi ya kung'oa uozo huu katika jamii. Njia ya kuondoa uozo huu ni kung'oa wanyonyaji hawa au mfumo huu wa ubepari na mizizi yake. Kifo hakiwezi kuwa suluhisho jinsi Dzombo anavyoona. Suluhisho ni kutafuta njia ya kuung'oa ufisadi kupitia kwa mapinduzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Hapa ndipo anakutana na rafiki yake Maskini Jeuri. Maskini Jeuri anamweleza, "ikiwa umekosa mafuta, basi twende kwako tukawashe taa". Nimebeba mafuta hapa, twende. Maskini Jeuri alikuwa amebeba chang'aa, aina ya kileo kikali cha kienyeji. Dzombo bila kujua maana ya 'kuwasha taa' anachukua hayo 'mafuta' na kuyatia katika taa ya kibatari. Taa inalipuka baada ya kuwashwa.

Baadaye anagundua kuwa hayo hayakuwa mafuta bali chang'aa na kumwuliza Maskini Jeuri, kwa nini anamtenda hivyo? Maskini Jeuri anamwambia, "nilikuwa nikifikiri ulikuwa unafanya utafiti, ingawa hukufanikiwa".

Nyumba ya Dzombo inadhihirisha mandhari ya umaskini uliokithiri. Pembejeo na samani zilizo nyumbani mwa Dzombo zinaonyesha hali yake ya uchochole. Punde Maskini Jeuri anamweleza Dzombo kuwa 'kuwasha taa' kwa maskini ni kutumia hivyo vileo ili kusahau umaskini wao. Ulevi huwapatia 'nguvu' zaidi za kusahau uchochole wao. Mwandishi anaonyesha kuwa kulewa hakuwezi kuondoa shida. Baada ya ulevi kumwisha mlevi machoni, shida iliyokuwepo bado itakuwa ingalipo na huhitaji mbinu za kuisuluhisha.

Hadithi hii ilitokea katika mawazo ya Dzombo. Mawazo ya Dzombo yaliranda hadi kwa Mzee Matingasi kwa ulevi ambako walikuwa wameenda na Maskini Jeuri ili kuwasha taa angalau wasahau shida zinazowakumba. Kinywaji hiki cha kienyeji kilikuwa kimepigwa marufuku na serikali. Vileo vilivyoruhusiwa vilikuwa ni vile vya kigeni. Mzee Matingasi alihitajika kuendeleza biashara yake haramu kwa njia ya kisiri. Kulikuwa na sheria za ubaguzi kiuchumi ili kuzuia wenyeji wasitumie vileo vya asili ila kutumia vileo vya kigeni. Ili kuendeleza biashara hii 'haramu', askari mmoja aliyekuwa akija kuwasumbua watengenezaji wa kinywaji hiki alikomeshwa na mlungula. Hili ni tatizo la ufisadi katika jamii. Pia mwandishi anatuonyesha majibizano baina ya walevi na kutuonyesha nafasi

duni ya mwanamke. Lakini kwa maoni yake anataka kuonyesha kuwa wanawake wana nafasi muhimu katika ujenzi wa taifa. Safari ya utu ilimfunza kuwa hapakuwa na ubaguzi baina ya wanawake na wanaume. Wote ni binadamu na hushiriki katika maendeleo ya nchi bega kwa bega. Wanawake wana jukumu kubwa la kuendeleza kizazi cha jamii na pia wanastahili madaraka kama vile tunavyoona Mtu Binti Fikirini akiwa mkuu wa kiwanda cha Trimi kinyume na hali ya huko Jehanamu ambapo wanawake ni viumbe duni visivyostahili wadhifa wowote.

Katika dhifa iliyoandiliwa kwa niaba ya Dzombo, Mtu Bint Fikirini anamtaka Dzombo amfafanulie maana ya 'Yes' na 'I am sorry' na ikiwa hii ndiyo lugha ya duniani. Dzombo alieleza maana ya lugha hii na kumweleza Mtu Bint Fikirini kuwa hii ni lugha ya 'English' yaani Kiingereza. Wenyeji wa Dzombo walifasiri neno English kama 'Iblish', kumaanisha udhalimu kwa sababu ibilisi huhusishwa na ubaya. Wakoloni walitumia lugha kama chombo cha ukandamizaji na kuendeleza masilahi yao kama asemavyo Ngugi wa Thiong'o (1986) kuwa lugha ndiyo iliyotumiwa kuwakengeusha Waafrika ili kufuata utamaduni wa wageni. Kwa hivyo 'ibilish' inaleta taswira ya ibilisi. Hii ni mojawapo wa minyiri ya istiimari. Maoni ya mwandishi ni kuwa lugha hii ndiyo iliyotumiwa kueneza ubepari na istiimari katika nchi za Kiafrika. Iliwabidi watawaliwa watumie lugha hii ya wageni. Kuhusu jambo hili Ngugi wa Thiong'o (1986) analichukulia kama istiimari na ubeberu wa kiutamaduni uliokusudiwa

kumfunga mwafrika kiroho na kimawazo. Lugha hutumiwa kwa mawasiliano na kuendeleza utamaduni. Matumizi ya Kiingereza yalikusudiwa kuwateka bakunja watawaliwa ili kusau utamaduni wao na kuendeleza utamaduni wa kigeni. Wakati wa ukoloni wanafunzi walilazimishwa kuzungumza Kiingereza. Yeyote ambaye angezungumza lugha yake ya kwanza angeadhibiwa vikali kwa kuchapwa viboko. Lugha ya watawala hasa wakoloni ilitumika kuendeleza na kueneza sera na propaganda yao ili kudhibiti utawala wao.

Kwa muhtasari, hadithi ya Maskini Jeuri inatuonyesha ufukara uliokumba jamii. Pili, inadhihirisha ubaguzi wa aina tofauti tofauti kama vile baina ya matajiri na maskini, wanawake na wanaume na matumizi ya lugha yanayojinasibisha na tabaka. Na waliotumia lugha ya kwanza shuleni waliadhibiwa. Mwisho kulikuwepo ambao umekumba serikali nyingi za Kiafrika. Polisi katika jamii hizi hutumiwa kama chombo cha ukandamizaji badala ya kuwalinda wananchi. Mwandishi anasema;

> "Serikali ni chombo cha kulinda na kuendeleza maslahi ya tabaka fulani tu peke? --- Na huku wakidai kuwa ni watumishi kwa wote--- huo sio unafiki?
> *(ukurasa 202)*

Kulingana na Mzee Matingasi, polisi wanaendeleza ufisadi. Mambo haya yote yanafanya maisha kuwa magumu kwa watu wa tabaka la chini. Ndiposa wanaenda 'kuwasha taa', lakini pindi tu 'inapozimika' wao hujipata bado wapo pale na shida zao. Maoni ya mwandishi ni kuwa mwanadamu anahitaji

kujikomboa kutoka kwa istimari hii na udhalimu wa wenye nguvu. Hadithi ya Maskini Jeuri na Matingasi inadhihirisha uhalisi katika jamii na hivyo kuafiki kanuni na mtindo wa uhalisia wa kijamaa.

### 4.1.3 HADITHI YA WACHUNA

Wachuna ni tabaka ambalo halikuwa na utu. Wachuna ni istiara yenye maana ya wageni hasa waliotawala bara la Afrika. Pili jina hili ni majazi linalotokana na kitendo kuchuna, yaani kutoa ngozi kwa mnyama. Katika muktadha wa dhamira ya mwandishi inaweza kufasiriwa kama kuvua hadhi, mali na heba na kumwacha mtu bila stara. Hivyo ni kumfukarisha mtu na kumnyima utu. Hapa linachukua maana ya kumdhalilisha, kumbagua, kumnyanyasa, na kumdhulumu mtu kwa kila namna. Wachuna waliweza kudumisha utawala wao kwa kutumia njia tofauti kama tutakavyoona katika maelezo yanayofuata. Hadithi ya Wachuna inasheheni matukio ya kihistoria hasa majilio ya wageni kutoka ulaya katika mwisho wa karne ya kumi na nane na mwanzo wa karne ya kumi na tisa. Kundi hili la Wachuna lilifilisi nchi ya Walenisi kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Wachuna walikuwa watu wabaya waliojaa ulafi na wasiothamini utu wowote. Hadithi hii inaonyesha vitendo vyao vya kikatili. Enzi ya Wachuna inaweza

kufananishwa na maisha yalivyokuwa Jehanamu au duniani kwa wakina Dzombo.

Wachuna waliharibu mali ya asili ya Walenisi kwa kukata misitu na kufyeka mapori. Kwa kufanya hivyo walipanua majangwa. Miti hii ilitumiwa kwa shughuli zao za kibinafsi kama kuchoma makaa na kuuza kuni kwa walio katika tabaka la chini. Wachuna hawakuweza kueneza umeme kwa wale wa tabaka la chini kwa kuhofia kuinukia kwa wachochole. Lakini kwa wakati huu Walenisi walikuwa wakipanda miti zaidi kama mali ya taifa. Uhifadhi wa mazingira ni jambo muhimu kwa jamii kwa sababu miti huwa na faida furifuri. Faida hizi zilipuuzwa na Wachuna. Kwa sasa *Wawalenisi* wanajitahidi kutumia umeme ili wasiangamize misitu kwa kuchoma makaa na kuni. Wazo lingine ni kuwa Wachuna hawakuwapatia vijana fursa kamili ya kushiriki katika uzalishaji mali katika taifa lao. Wengi waliishia kuwa malaya, wakora, majangili na walofa. Lakini kwa upande mwingine, ili kudumisha maslahi yao, Wachuna waliwashika na kuwaweka gerezani. Mwandishi hatuelezi kama walifanyiwa mashtaka. Lakini walitiwa kizuizini. Kutia raia kizuizini ni njia moja iliyotumiwa kujidumisha katika uongozi. Wengine waliuawa na kusingiziwa kuwa walikuwa wakitaka kutoroka. Katika utafiti wake Dzombo alikumbana na maelezo kuhusu marika tofauti ya vijana. Taswira ya marika ya vijana yanatuonyesha kushughulika kwa wananchi katika sekta mbalimbali za jamii ili kuzalisha mali na pasionekane kuna wale wasiofanya kazi. Wazo hili ni tofauti na enzi za

Wachuna ambako kulikuwa na msamiati kama kustaafu, kukosa kazi, kuachishwa kazi na kuachiriwa kazi. Wachuna walichukulia msamiati kama huu kuwa hali ya maumbile. Pia katika ulimwengu wa tatu, watu huweza kuachishwa kazi au kustaafishwa au wakakosa kazi. Baadhi ya matatizo ya ulimwengu wa tatu hutokana na shinikizo kutoka kwa mataifa ya kimagharibi. Wachuna waliigawa nchi katika vipande vipande. Kwa kufanya hivyo walididimiza nchi kwa kuwanyang'anya wenyeji mashamba yao na kujilimbikizia ekari nyingi za mashamba. Ulafi huu ulizua matabaka ya kimwinyi na ubepari. Kwa upande mwingine kama tulivyosema '*Berlin Conference 1884*' iligawanya bara la Afrika miongoni mwa wageni. Baada ya uhuru kulizuka kundi la watawala walioendeleza uchuna. Huu ukawa ndiyo ukoloni mamboleo. Ilibidi nchi nyingi zikombolewe kutoka kwa udhalimu huu wa Wachuna na pia kuwe na sera ya taifa kuhusu jamii. Katika harakati hizi mashairi yalitungwa kama nyenzo ya kuendeleza umoja wao. Vijana walianzisha vyama vya ushirika ili kujikinga na tawala dhalimu za Wachuna. Mkangi anatumia ushairi ili kutoa hisia zake kuhusu mambo ya ushirika na hasa ujamaa. Makundi ya vijana yanafanya kazi kwa pamoja kusisitiza umoja wao. *Azimio la Arusha* lilisitiza kushirikiana na kuunda vyama vya ujamaa kwa faida ya wote. Kwa mujibu wa uhalisia wa kijamaa, wanadamu wanahitajika kushirikiana kwa manufaa ya wote. Kutokana na ushirikiano huu Wachuna waliondolewa. Hili ni wazo linalogusia harakati za kupigania uhuru katika nchi nyingi za Kiafrika ili kumwondoa mkoloni. Umoja huu wa wawalenisi ndio uliokuwa ngao yao katika

juhudi za kuwaondoa Wachuna. Wahenga hawakukosa walipolonga kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Utengano huu ni udhahifu wa kuleta umoja lakini hukuza wale wenye ubinafsi ambao kuzuka kuwa mabwanyenye na mabepari. Mkangi anasema;

> Hatua hii ilikuwa cheche iliyoshika moto na kumwondoa Mchuna muda mfupi baadaye.
> *(ukurasa 113).*

Katika harakati za kupigania uhuru, nyimbo zilitumiwa ili kusisimua ari ya wenyeji. Kwa mfano katika harakati za Mau Mau hapa nchini, nyimbo zilikuwa chombo muhimu. Al-Amin Mazrui katika kazi zake, *Kilio cha Haki* (1981) na *Chembe cha Moyo* (1988) anatumia ushairi kuamsha ari za wanaharakati na kuwatia moyo. Nyimbo na ushairi ni chombo muhimu cha kuliwaza na kusisimua ari za wazalendo.

Wachuna walitoa propaganda kuhusu mfumo wao wa uzalishaji mali. Mkangi anasema;

> Wakati wa utawala wao wa kunyanyasa watu, propaganda yao ilikuwa ikitoa porojo zilizokuwa zikisema kuwa, kula na kushiba si jambo muhimu--- Wako wale waliobahatika kushiba – hapa wakimaanisha wao wenyewe, na kwa wale wengine waliokonda kwa njaa, ni kwa sababu hawakubahatika. Kuombaomba ndiko kulikuwa maisha yao na mwisho kifo kikawa mkombozi wao.
> (*ukurasa 114*).

Nchi za bara la Afrika zina rutuba nyingi lakini watu hufa kwa njaa kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Wachuna hawakuona faida ya kuzalisha chakula. Wachuna walikuza utegemezi wa misaada. Vyakula vya asili vilitupiliwa mbali ili nchi za Kiafrika zizidi kutegemea mataifa ya kimagharibi. Dhana hii ndiyo iliyokuzwa na nchi hizi za kimagharibi zinazotoa misaada. Wanazipatia nchi za Kiafrika misaada ili kuendeleza istiimari yao. Lakini *Walenisi* walibuni mwito wa 'Chakula kwa wote', na matumizi bora ya ardhi ili kuzalisha chakula zaidi. Utawala wa Wachuna ulitumia udongo kwa njia mbaya ili kujipatia utajiri wa kibinafsi. Waafrika walioajiriwa au kulazimishwa kufanya kazi katika mashamba ya mabepari ambako walilipwa mishahara midogo. Walter Rodney (1989), na Bathwel Ogot (1969) wanadai kuwa Waafrika walipewa ujira mdogo na 'posho' ili kuwakimu waendelee kufanya kazi. Wengine walikodisha mashamba yao kwa Waafrika kama asemavyo Mohamed Suleiman Mohamed (1976:1);

> Ah! Vizuri (Fuad) alisema kuwambia wakulima wapatao darzeni walioleta gunia na vipeto vya mazao yao, zawadi kwa bwana shamba. Utatusamehe Bwana, safari hii tumekawia alisema mmoja wao kwa sauti nyenyekevu huku akigoteza kichwa kilichoeleka gunia, haidhuru lakini msikawie kuniletea kodi yangu. (*ukurasa 1*).

Mawazo ya Fuad yanaonyesha mfumo wa ukabaila. Wakulima lazima walete kodi kwa Bwana Shamba na vipeto vya mazao. Tatu, wenyeji iliwabidi walipe kodi kwa matumizi ya mashamba ambayo yalikuwa yao. Hii ndiyo ilikuwa sera

ya Wachuna. Sera hii ilikuza ubwanyenye, umwinyi, ukabaila na ubepari. Sera ya Wachuna ilidhalilisha wenyeji kwa kuweka matabaka na kuwanyonya kama kupe. Wachuna waliweza kukuza viwanda vyao kwa malighafi yaliyotoka bara la Afrika, bara lenye mito na mvua ya kutosha inayoweza kutoa maji ya kunyunyizia mimea ili kuzalisha chakula cha kutosha. Lakini hili halifanyiki. Kutozingatia kilimo kuliwafanya *Walenisi* kutegemea misaada wakati wa utawala wa Wachuna. Kutimuliwa kwao kulikuwa ushindi kwa *Walenisi*. Mkangi katika kuzungumzia suala hili anasema;

> Udongo haukuwa chombo cha kuzalisha chakula, ila rasilimali ya kuchezea kamari kwa minajili ya kujipatia utajiri wa kibinafsi hata bila kutoka kitandani. Ama kulima kwao kulikuwa kuajiri watu kwenye mashamba yao, ama kuyakodisha kwa atakayelima. Lao lilikuwa ni kuchukua kodi tu na kunenepa kwa jasho la wengine. Si ajabu--- Kuwa aliyelima kutokuwa na shamba, na yule asiyelima kuwa nalo. *ukurasa 114)*

Kwa mujibu wa maelezo haya ardhi ilitumiwa kwa manufaa ya kibinafsi badala ya kutumiwa kwa manufaa ya taifa nzima. Kama tujuavyo, ardhi ni nyenzo muhimu ya uzalishaji mali. Juhudi za Walenisi baada ya kuwaondoa Wachuna zilifanya njaa kusikika kama hekaya na magonjwa ya watoto kama utapia mlo na marasimasi hayakuwepo. Mwito wa Walenisi ulikuwa;

> Ashibaye haugui,
> Asiyeugua hufikiri
> Na afikiriaye huendelea--- *(ukurasa 119)*

Mwito wa Walenisi ni sawa na mwito wa Watanzania wa *Azimio la Arusha (1967)*, kuzalisha mali kwa jamii. Mwito wa namna hii haupo hapa nchini Kenya kwa sababu ni nchi ya kibepari. Hivi majuzi serikali ya chama kinachotawala, NARC imetoa Mwito 'A working Nation' lakini umebadilishwa na wanaharakati (Kundi la wanajamii ambao hawakupenda mabadiliko haya mapya wengine walikuwa wanafanya stihizai baada ya Waziri wa Uchukuzi kusema kuwa kila gari liwekewe vidhibiti mwendo na mikanda na kukawa na ukosefu wa magari ya usafiri. Ilibidi wananchi kutembea kwa mwendo mrefu kwenda kazini na kurudi nyumbani. Baada ya haya matatizo ya magari ndipo walipobadilisha mwito huu wa 'a Working Nation' na kuwa 'a Walking Nation' kwa sababu wanatembea muda mwingi badala ya kufanya kazi).

Enzi ya Wachuna ilidhalilisha mwanamke kama chombo cha kumfariji mwanamume. Mwanamke ilimbidi afuate maagizo ya mwanamume. Enzi yao iliwachukua wanawake kuwa waovu sana. Mwanamke alichukuliwa sawa na zulia kwa wanaume kukanyaga tu.

Safari ya utu ilimfahamisha Dzombo kuwa watu katika nchi ya Walenisi hushirikiana. Furaha ya mmoja ni furaha ya wote. Huzuni ya mmoja ni huzuni ya wote. Pia alijua kuwa Jehanamu kweli hakukuwa na utu. Wanadamu kutoka duniani wamefananishwa na Wachuna. Wakoloni waliligawagawa bara la Afrika

kupitia kwa mkutano wa Berlin Conference 1884-5 uliofanyika huko Ujerumani.

Mwandishi anaeleza;

> Wachuna waliigawa nchi
> Vipandevipande karatasini
> Nayo njaa kujaza nchini---
> Udongo ukawa mali ya Wachuna wachache. Haijulikani ikiwa walitazamia hawa wengine wengi waishi hewani ama vipi? ... baada ya wao kuwanyima wakulima udongo, walishindwa kuulima. Badala yake walitumia mabavu na kuwashuritisha wakulima kuzalisha kisha kuchukua mazao na tena kujibandika kuwa hao ndiyo wakulima halisi.
> *(ukurasa 170).*

Hapa ni namna nchi za Kiafrika zilivyoangukia istiimari za wageni. Haya ni matukio ya kihistoria yaliyotokea mwaka wa 1884 baada ya mkutano uliofanyika, huko Ujerumani kwa jina *'Berlin Conference'.* Washiriki wa mkutano huu walikuwa Ufaranza, Ujeremani, Uingereza, Italia, Ureno na Ubelgiji. Mataifa haya yalinyakua na kugawana bara la Afrika. Huu mkutano ulizigawa na kuzitenganisha jamii za Kiafrika zilizokuwa pamoja, kwa mfano Wamasai waligawanywa mara mbili. Baadhi wako nchini Tanzania na wengine wako nchini Kenya, katika nchi ya Somalia baadhi ya Wasomali wako Uhabeshi (Ethiopia) na wengine wako nchini Kenya, waliobaki (Wasomali) wako katika nchi ya Somalia. Wageni hawa walizigawanya jamii hizi kinasibu bila kutilia maanani asili, itikadi na mila zao. Wakoloni hawa walituma walowezi wao ambao walionyakua sehemu kubwa ya nchi kama mashamba yao, ambayo walishindwa kuyatunza.

Wakoloni hawa walijigamba kuwa kuja kwao kulikuwa majaaliwa ya Maulana. Walitumia silaha kuwadidimiza Waafrika. Utawala wa Wachuna ulipuuza elimu ya Waafrika, huduma za afya na matibabu zilipuuzwa, kilimo na hifadhi dhidi ya baridi, mvua na kuendeleza ujinga. Wachuna walisisitiza kazi ni bahati ya wachache. Jambo lililozua utabaka na mafalahi. Wachuna hawa hawakuwaona Walenisi kama watu. Mkangi anasema;

> Hawakuchukuliwa kama binadamu tena – yaani mtu awezaye kusikia njaa, kuugua, kufanya mapenzi, kustarehe na kadhalika: kama vile Wachuna walivyokuwa, ela nambari au tarakimu tu basi. Nazo tarakimu hazina uhai--- kujibagua kwao na kujiona kuwa walikuwa watu bora kuliko binadamu wenzao, kujidhihirisha sana kwa sana kwa maskani yao.
> *(ukurasa 174).*

Wachuna walikuwa na maskani bora, madaktari wengi na nokolani zao hazikuwa na msongamano; utawala wao ulizua ubaguzi, ubwanyenye na ubepari. Kuja huku katika bara la Afrika ilikuwa ni njia ya kutanda minyiri yao ya kuchuna uchumi wa bara la Afrika.

Kwa muktadha huu wa hali ya Wachuna mwandishi anatueleza matukio ya kihistoria yaliyojikita katika misingi ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa kwa sababu jamii ya wanadamu hutawaliwa na matendo yao ya kihistoria. Hadithi hii ya Wachuna inatoa umuhimu wa hadithi, kutoa maelezo ya historia ya jamii. Historia hii ya Wachuna bado inawaathiri waafrika kwa njia tofauti. Historia ya Wachuna ilipatikana katika Maktaba Kuu ya *Walenisi* ambako Dzombo alikuwa

anafanya utafiti. Udhalimu wa Wachuna ulikithiri. Waliweza kuwadhulumu kwa njia tofauti. Mkangi anasema haya;

> --- elimu isiyo na usawa, sheria zisizo na haki, uchumi usio na mapenzi, siasa zisizo na ukweli, mawasiliano yasiyo na dira, maendeleo yasiyo maendeleo, utamaduni usio na dhamira, na uhusiano wa kinyama kati ya watawala na watawaliwa, mke na mume, na mnyonge na mwenye uwezo--- Wachuna waliweza kueneza uchuna wao--- (*ukurasa 187*)

Dondoo hii inatupatia picha kuhusu mienendo ya Wachuna. Walikuwa hawaachi kusisitiza kuwa jamii ya binadamu, siafu na nyuki zilikuwa zinafanana na kuendelea kusisitiza kwamba tofauti za kijamii asili zao ziko katika sheria za maumbile. Haya yalikuwa matusi na kudhalilisha wanadamu wengine. Bathwel Ogot (1969) anaeleza kuwa elimu iliyopewa Waafrika ilikuwa ya kiwango cha chini. Watoto wa Kizungu walitumia shilingi mia nane kwa mwaka ilhali Mwafrika alitumia shilingi thelathini na mbili kwa mwaka. Pili, elimu waliyopewa Wafrika ilikuwa ya kuwaelekeza kujua kusoma Bibilia na kuwa wafanya kazi bora wa mashambani na kufanya kazi ya mikono. Huu wote ni ubaguzi wa hali ya juu.

Walizua kila namna ya vitimbi ili kuwachuna wenzao. Sera yao ilikuwa, kila mtu kujipigania na kujifikiria ili aweze kuishi. Ubinafsi na ulafi ukasibu kuchochea ubinafsi na uchoyo. Hapo ilikuwa kujirundikia mali. Wachuna waliamini katika msemo usemao kuwa kila mtu peke yake, na Mungu awe wetu sote. Huu

ulikuwa msemo wa kusifu ulafi wao. Uhalisia wa kijamaa unapinga ulafi na kubaguana. Binadamu wote ni sawa.

Mwisho Mkangi anatueleza jinsi Wachuna walivyoondolewa na uchuna wao - kwa kusema;

> Mwanzoni, miale ya mapambazuko ya ufahamu ilionekana hafifu sana. Lakini haya yalikuwa mapambazuko, kwani uzuri wa mapambazuko ni kwamba hayazuiliki! Kwani kwa polepole na kwa utaratibu miale hii ilimwamsha wa kwanza, wa pili---; wa kumi--- wa mia, ---, elfu---, wa laki moja--- wa mamilioni--- mpaka mwisho ulimwengu wao wote ukawa macho--- kwa mwangaza huu mpya wa ufahamu, wakaweza kuona unyama na uchafu uliokuwa kati yao. Unyama wa wachache kushiba hali wengi wameachwa kufa njaa, unyama wa wachache kutawala wengi kwa mabavu. Unyama wa kunyanyaswa. Unyama wa dhuluma. Unyama wa kila aina. (*ukurasa 193 - 194*).

Katika dondoo hili tunaona jinsi ari ziliamka dhidi ya udhalimu wa Wachuna. Hata hivyo haikuwa rahisi kwa sababu Wachuna walipigana kukinga kitumbua chao kisiingie mchanga. Mapigano haya yalikuwa baina yao na umma. Vilikuwa vita baina ya utu na uchuna ama kati ya ukweli na unyama. Mapambano baina ya wachache na wengi. Mkangi anaeleza kuwa, sauti ya wengi ndiyo sauti ya Mungu, basi juhudi za Wachuna hazikufua dafu. Kwa maoni ya Mkangi, udhalimu lazima ukabiliwe vilivyo kwa njia zozote ziwezekanazo. Mwisho Mkangi anasema;

> --- Walikuwa wamekwenda kulala wakiwa wapo, lakini walipoamka wakawa hawapo!!! Mapambazuko haya yakawa si yao tena milele. Haya yalikuwa ni mapambazuko mapya, mapambazuko ya kujenga ulimwengu mpya usio na karaha. Jua la ufahamu likazidi kuangaza na watu wakaanza kujenga ulimwengu mpya. *(ukurasa 195 )*

Maelezo haya ya Mkangi yanatuonyesha juhudi za nchi nyingi za Kiafrika kujikomboa kutoka kwa minyororo ya wageni. Pili yamefungama na misingi ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa inayosisitiza ujenzi wa jamii mpya ili kuleta mabadiliko katika maisha ya wanadamu na kuvunjilia mbali istiimari za walowezi na ugandamizi wao. Ujenzi huu wa jamii mpya unachukuana sawia na mawazo ya Mbughun (1978) katika maelezo yake, *The Theme of A New Society in Kiswahili Prose Tradition* katika Tuki Kiswahili Vol. 48/2 Septemba. Tatu, ulimwengu huu mpya usiwe na karaha. Wanajamii wote ni sawa, ubaguzi na udhalimu umeondolewa. Kuwepo na umoja baina ya wanajamii wote. Nne, Mkangi anasisitiza kupigania haki, kukomesha mateso na kutetea wanaonyanyaswa. Kabla ya kifo chake, Mkangi alikuwa mwenyekiti wa Chama cha Wanaume Wanaopigwa na Kunyanyaswa na Wake Zao. Jambo la tano ni kuwa mawazo ya Mkangi yameathiriwa na mawazo ya aliyekuwa raisi wa Tanzania Mwalimu Nyerere. Wazo la Ujamaa limejitokeza kama msingi muhimu katika maisha ili kuondoa ubaguzi, ubwanyenye na ubepari baina ya wanajamii wote.

### 4.1.4 HADITHI YA MABAVU

Mabavu alikuwa msasi hodari. Sifa zake zilienea kama moto katika nyika au majani. Msasi huyu alimpenda msichana kwa jina Kadzo. Kadzo alikuwa kipenzi na tunu ya jamii. Mabavu alimmezea mate bila kupata. Uzuri wa Kadzo ulijulikana kila pembe za kijiji. Umbo la Kadzo liliwateka wengi. Mabavu alikuwa kila mara haachi kumkonyezea kila alipomwona lakini Kadzo hakumpenda bali alimpenda kijana aliyeitwa Dutu. Hili halikumpendeza Mabavu mpaka siku moja akataka kujua kwa nini yeye ni shujaa lakini Kadzo hampendi. Lakini Kadzo alimjibu kuwa Dutu huwa anampa nyama ya ulimi. Mabavu kwa kutokujua maana ya msemo 'nyama ya ulimi' aliingia mstituni na kuwinda wanyama ili kuleta ndimi. Mkangi anasema;

> --- Kwa kusikia hivyo akasema kwa mshangao, ni ndimi tu ndizo utakazo? Basi nawe utazila mpaka uchoke ! Alimwacha na kwenda kuwinda. Alifuma wanyama wengi na baada ya juma moja, akarudi kwa akina Kadzo na ndimi za wanyama wa kila aina zikimlewalewa. Haya shika – nini zaidi wataka?
> (*ukurasa 163*)

Kadzo alimweleza Mabavu maana ya 'nyama ya ulimi'. Nilikuwa nikimaanisha maneno matamu. Dutu alikuwa mwenye kutenda mambo kwa utaratibu na mnyoofu wa moyo. Alikuwa na utu. Hizi ndizo sababu zilizomfanya Kadzo kumpenda Dutu. Mabavu, aliangusha uso na kwa hasira akafoka 'tutaona' na akatokomea kwa sababu ya kukataliwa na Kadzo.

Lakini muda si mwia, katika usiku wa manane kijiji kilishambuliwa na simba, ambaye aliwahepa mashujaa wa kijiji waliokuwa wametoka na pinde zao. Mara bin vuu wakasikia kiambaza kimevunjwa na Kadzo akipiga mayowe. Alikuwa amenyakuliwa na simba. Mashujaa wa kijiji hawakuweza kumwokoa Kadzo. Usiku huo Mabavu hakuwa kwake. Lakini alipoulizwa asaidie kumwokoa Kadzo ambaye alikuwa lulu ya jamii, Mabavu alisema, "Dutu aende akamuue huyo simba". Umma haukujua mzaha huu wa Dutu. Lakini wazazi wa Kadzo walimuendea kwa unyenyekevu na kumweleza kuwa, "kama Kadzo wetu atapatikana hai basi sisi tungekuoza na awe mkeo. Ahadi hii ilimtoa Mabavu chapuchapu hadi milimani alikomwandama simba. Aliweza kumwua na kumchukua Kadzo akiwa mzima.

Hapo ikawa Kadzo ameokolewa kutoka kwa kinywa cha simba. Kadzo akaishia kuolewa na Mabavu. Mwandishi anasema;

> Alizidi kutumia ujanja huo huo na kujipatia wasichana warembo wote. Kwa hofu watu hawakukosa kumjia wakitafuta ulinzi.
> 'Simba', hivi sasa ndivyo walivyokuwa wakimwita, chukua huyu binti yetu lakini utapatie ulinzi tafadhali. Naye aliozwa hao wasichana--- Ikawa sasa haulizi wasichana tena ili awaoe, bali kujipa jukumu la kuwabikiri tu ili wazazi wao waweze kupata ulinzi wa simba. (*ukurasa 165*).

Mabavu sasa alikataa kwenda mawindoni. Alihitaji watu wamletee chakula kama fidia ya ulinzi atakaotoa. Alitunga sheria na watu wakalazimika kuitikia. Hakuweza kupingwa na ndivyo alivyozidi kujijenga na kujipa ufahari wa simba. Kutokana na ukali wao walijipa 'chapa ya simba' kama kitambulisho cha

utawala wao. 'Chapa ya Simba' ni taswira kuonyesha bendera ya Waingereza, ambapo bendera yao 'The Union Jack' ina ishara ya simba. Pia inaweza kuwa taswira ya nchi za kigeni zilizogawana na kutawala nchi mbalimbali za bara la Afrika. Pia kule kujulikana kwa Kadzo kwa ruembo wake ni taswira ya bara la Afrika lililojulikana kwa kuwa na malighafi yake. Malighafi hii inamezewa mate na akina 'Mabavu', mataifa ya kigeni. Halafu akina Dutu ni mataifa maskini ya bara Afrika.

Katika hadithi hii ya Mabavu kuna maudhui kadha yanayojitokeza. Kwanza kabisa 'Mabavu' ni majazi yenye maana ya kutumia nguvu. Hadithi hii inaning'inia juu ya mfumo wa uzalishaji mali. Mabavu aliletewa mali hasa vyakula ili aweze kutoa ulinzi kwa wahusika. Jambo hili linatupeleka kwa mifumo ya ukabaila, ubwanyenye na umwinyi. Watu wachache wanamiliki mali nyingi na wengi wanawakula mwata. Mkangi anasema;

> Kwa sababu ya uhaba wa vitu, kila mtu alilazimishwa kujipigania na kujifikiria ili aweze kuishi. Ulafi basi ukasibu na kuchochewa na ubinafsi uchoyo. Chochote ulichotaka, uliweza kukinunua na kukirundika. Vitu muhimu vilinunuliwa haraka haraka na wasiokuwa na uwezo wa kichumi wakichelea na kuvikosa baadaye. "Kila mtu peke yake, na Mungu awe wetu sote", ndivyo msemo wao mmoja ulivyosifu ulafi huu wao.
>
> (*ukurasa 189*)

Kulikuwa na uhaba wa kina Mabavu wa kutoa ulinzi, ndiposa watu walimiminika kwake ili waweze kupewa ulinzi. Ulinzi huu ulizua ubinafsi.

Kuhusu jambo hili la wachache kumiliki nyenzo zote za uzalishaji tazamo dondoo lililo katika hadithi ya Wachuna (ukurasa 112). Pia hotuba ya mzee Mtu – Mwenzio inaonyesha kuwa Uchuna ulikuwa urundikaji wa mali na faida ya kibnafsi.

Pili katika enzi za zamani hakukuwa na pesa. Biashara iliendeshwa kwa njia ya kubadilishana mali bila kujali thamani halisi ya kitu. Mabinti walibadilishwa na ulinzi – ambao ulitolewa na Mabavu. Hali kadhalika ndoa ilitumika katika kuleta uelewano baina ya jamii au koo mbili tofauti ingawa kwa muktadha huu haikutumika hivyo.

Jambo la tatu ni kuwa wakati wageni hasa kutoka Uingereza au Ujerumani na nchi zingine za Magharibi walipokuja barani Afrika walitumia ujanja mwingi ili kuteka nchi na miliki tawala za Kiafrika. Watawala Waafrika walidanganywa kuwa wanapewa ulinzi dhidi ya tawala zilizokuwa na nguvu na ambazo ziliwanyanyasa. Miongoni mwa watawala waliopoteza himaya zao kwa njia ya namna hii ni Mumia kutoka Wanga nchini Kenya, ambaye aliahidiwa kulindwa dhidi ya Wanandi na Wanajaluo. Kabaka Mutesa wa Buganda alihaidiwa ulinzi dhidi ya Mpinzani wake wa jadi kwa jina Kaberega kutoka Bunyoro, na mwisho ni Marealle wa Marangu kutoka nchini Tanganyika. Punde si punde watawala hawa Waafrika walipoteza himaya zao. Wakoloni hawa waliweza kuweka bendera zao. Waingereza waliweka bendera yao yenye chapa ya simba,

ambayo ni alama yao ya ufalme kama kitambulisho cha utawala na nasaba yao. Wazo la bendera linatoa mfano wa jinsi wakoloni walivyoingia na kuleta istiimari zao barani Afrika. Bendera hii ilifuatwa na udhalimu wao, hasa Mkangi anaposema kuwa, "sasa hakuwa anachukua mabinti wazuri kama wake zake bali sasa alijipa jukumu la kuwabikiri tu ili wazazi wao waweze kupata ulinzi wa 'simba'." Udhalimu wa namna hii ulitendwa na wakoloni nchi Tanganyika. Ebrahim Hussein (1969) anaeleza jinsi kundi la Wajerumani walivyoenda kwa nyumba ya Kitunda na kunyakua binti yake mbichi kwa jina Chausiku.

Wakoloni walitumia mabavu katika kuchukua ardhi yetu, kuchukua wasichana wetu, kutunyanganya utawala wetu, kuharibu utamaduni wetu, kuchukua mifugo wetu na kudhalilisha utu wetu. Hadithi ya Mabavu inachukua taswira inayotoa maudhui ya kihistoria jinsi wakoloni walivyokuja na kisha kutunyanyasa.

### 4.1.5 HADITHI YA MOTO

Hiki ni kisasili cha mtu aliyegundua moto. Mtu huyu pia alikuwa msasi aliyekwenda kutega kulungu. Mahali hapo ndipo palipokuwa na njia ya wanyama hawa wakitoka au wakienda kunywa maji. Huyu mwindaji alijulikana kwa jina Moto. Moto hakuwa amepiga hatua kiustaarabu kwa sababu akimpata mnyama alikuwa akimchuna kwa kutumia jiwe halafu angemla mbichi. Akiwa

katika harakati za kusubiri matokeo katika mtego wake aliona amtengenezee mpenzi wake utunda. Malighafi yake yalikuwa mti na jiwe kwa sababu ushanga ulikuwa haujavumbuliwa. Moto alichukua vijiti viwili, kikubwa akakiita 'Mama' na kile kidogo 'Baba'. Aliweka kijiti Mama chini na kukitumia kijiti Baba kupekecha tundu. Haja yake ilikuwa atoboe matundu mengi. Baadaye angeliyakata haya matundu na kuyaviringisha, kisha ayaunge kwa uzi wa muwaa ili apate huo ushanga. Wakati wa kupekecha cheche zilitoka na kuanguka kwa majani makavu yaliyokuwa chini ya mapaja yake. Moto ulianza kufuka na kutoa moshi na kumchoma. Alikuwa na uoga kwa sababu alikuwa hajaona kioja kama hiki. Cheche hizi zilisambaaa na kuwasha majani, nyasi na kuteketeza miti. Moto huu ulienea kwa upesi.

Moto huu ulimteketeza na kumchoma kulungu aliyekuwa amenaswa mtegoni. Kulungu aliokwa vizuri sana kwa nguvu hizi ngeni. Hakuwa (moto) ameonja kitu kilichokuwa kimepikwa au kuchomwa kwa sababu msamiati huo haukuwa katika lugha yake. Alipoonja kinofu cha kulungu akaona ni kitamu na kisha akaanza kula nyama ya kulungu iliyochomwa. Hakuweza kumla kulungu na kummaliza, kwa hivyo nyama iliyobaki aliifunga vizuri na kupelekea jamii yake. Pamoja na kulungu alichukua kinga kilichokuwa kikiwaka na vile vijiti viwili vilivyozua moto baada ya kupekecha. Alifanya miujiza yake na kuuwasha moto wake. Wanakijiji walikuja kutazama kioja hiki. Kioja hiki kiliwavutia zaidi kwa sababu jinsi walivyozidi kukisogelea ndivyo vile ile baridi ya asubuhi ilivyozidi

kuwatoka. Moto huu pia ulikuwa unafuka moshi. Huu ulikuwa ugunduzi wa moto. Nguvu hizi mpya za moto ziliweza kugeuza maisha ya wanajamii. Mwandishi anasema;

> Akiwa bado ana sehemu ya nyama ya kulungu, akagawia na kuwaambia wale. Kila mmoja wao akakubali kuwa ilikuwa tamu sana. Naye ndipo alipowaambia siri ya kioja. Hakuwambia ule ukweli wa mambo, badala yake aliwaambia ati ni malaika ndiye aliyemtunukia uwezo huu! Aliwalambisha kwa kuwapa kaa kuchukua makwao. Nao kwa kukosa jina la kufaa wakaliita 'Moto'. (*ukurasa 157*)

Watu walizoea moto na kumiminika kwake kwa wingi. Ndipo akatoa masharti haya; moto ulipatikana kwake tu kila jioni, na baada ya matumizi uzimwe. Yeye pekee ndiye angelitoa 'moto mpya'. Tatu, moto hauibiki wala haufichiki. Atakayefanya kitendo cha kuuficha au kuiba atajuta mwenyewe. Uwezo huu na masharti haya yalimtia hisia za ukubwa na utukufu. Basi ikawa kwa wanajamii hakuliwi chochote bila moto. Utegemezi wake ukazidi. Mara akawaambia ili kulinda moto usife ilibidi aiache kazi yake ya kuwinda kulungu. Kwa hofu ya kukosa tunu hii, wanajamii walisema kuwa wangelimgawia chakula chao ili azidi kuchunga moto mtakatifu ili usife. Hapa akawa sasa yeye na familia yake wamekuwa kupe.

Mwandishi anaeleza;

> Basi, kwa kila mtu kumpatia theluthi ya chakula chake, Moto akapata uwezo wa kurundika zaidi. Siku si nyingi mkewe na watoto wake wakawa hawana

> haja ya kufanya kazi. Hali watu hawakukoma kumpatia 'kodi ya moto', ndivyo yeye na kizazi chake walivyozidi kujiepusha kufanya kazi, huku wakizidi kuzua masharti magumu ya kuficha utukufu wa moto.
> (*ukurusa 158*)

Ujanja huu ulipogunduliwa Wachuna na nasaba ya moto wakawa wameshazawa, kupevuka na kuenea na kuweza kujikinga kwa kila hila. Waliweza kugeuza jina la 'Moto' kwa sababu limekuwa la kawaida na kujibandika jina jipya lililojulikana kama kizalia cha ukoo wa 'Tai'.

Kutokana na kisa hiki cha moto ukoo mmoja wa Kichuna ulizuka na kuweza kujipatia Utukufu, uwezo na hekima kwa kutumia hila zilizoweza kuwapa utawala juu ya wenzao na kuwala jasho lao. Katika hadithi ya moto tunaweza kupata mambo yafuatayo. Jambo la kwanza kabisa, mkangi ambaye ni mwandishi wa riwaya hii ameathiriwa na kazi ya Shabaan Robert (1951), hasa kwa upande wa matukio ya kusimulia hadithi za wajumbe waliotumwa katika nchi tofauti. Pili anatueleza jinsi jamii za binadamu zilivyoweza kuvumbua mambo fulani. Baadhi yalitokea kwa sadfa kwa mfano uvumbuzi wa moto. Uvumbuzi wa moto ni matukio ya kihistoria yaliyotokea miaka milioni moja iliyopita kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Wakati huo jamii ziliishi kwa kutegemea nguvu zao kama kuwinda na kujikinga dhidi ya mazingira makali. Ilikuwa wakati huu ambapo mwanadamu alianza kupanda mimea kama shayiri,

mawele na mtama. Haya ni mabadiliko katika maisha ya binadamu. Mabadiliko haya yaliweza kufanya maisha kuwa bora.

Wazo la tatu ni kuwa, kutokana na mabadiliko haya, wanadamu walianza kuishi katika jumuiya ili waweze kujikinga dhidi ya wanyama wakali wa mwituni. Hata hivyo kwa muktadha wa hadithi ya moto, jamii ilizua jamii ya umwinyi miongoni wa jamii ile kubwa. Kundi la wachache lilianza kujilimbikizia mali na kutegemea wengine. Hawa ndio sasa walikuwa mabwanyenye na mabepari. Wanajamii bila 'kujua' walipoteza ile haki yao ya ujima na wakajipata wanalipa kodi, na kutoa vipeto vya vyakula kwa matumizi ya moto. Wenyeji sasa wanakuwa watumwa katika nchi yao. Jambo hili linaenda sambamba na jinsi Mohamed S. Mohamed (1976:1) anavyosema kuwa iliwabidi wenyeji kuleta vipeto vya mazao na kulipa kodi kwa bwana shamba. Pia kulizuka ukiritimba, nchi za kgieni zilizokuja barani Afrika zilitumia ukiritimba huu ili kulinda sehemu zao walizokuwa wamenyakua. Ukirimba huu ulizuia mataifa mengine kufanya biashara katika sehemu hizo zilizonyakuliwa. Sehemu hizi ziliitwa kwa kimombo 'Sphere of influence' au 'protectorate'. Himaya kama hizi zilikuwa Buganda, Kenya na Tanganyika miongoni mwa zingine.

Wakati wakoloni walipokuja katika bara la Afrika hasa Kenya na kwingine waliwalazimisha wenyeji kulipa kodi. Ulipaji wa kodi ilikuwa njia moja ya kuendeleza istiimari ya wageni. Waafrika walifanya kazi nyingi kwa sababu

walitawaliwa kwa njia ya ujanja. Kwa mfano baadhi ya wakoloni walikuja kueneza injili, kufanya biashara, kuvumbua bara hili na kadhalika. Jambo la kodi lilidhalilisha wale ambao hawangeweza kulipa. Bila kodi basi huwezi kupata moto.

Wazo la nne ni kuwa kwa maoni ya mwandishi bwana Moto alikuwa kupe. Aliweza kula jasho la wengine. Hali kadhalika huu ukoo wa 'Tai' kama ulivyojulikana ni jazanda ya ukoo wa Wamerika. Hapo awali katika hadithi ya mabavu, mwandishi alitueleza (ukurasa 166) kuwa "Wachuna walijipa ufahari wa 'simba' na mwishowe wakajipa ufirauni wa chapa ya 'Simba' kama kitambulisho cha utawala wa nasaba yao". Tuliona kuwa hawa walikuwa Waingereza kwa sababu bendera yao "Union Jack" ina kitambulisho cha Simba. Ukoo huu wa Waingereza ndio uliozaa ukoo wa 'Tai'. Jamii hii ya ukoo wa Tai ni Wamerika, ambao bendera yao ina alama ya kitambulisho cha Tai. Matumizi ya 'Tai' ni jazanda kuonyesha jinsi walivyoenea sehemu nyingi za dunia kwa kupaa juu sana. Hali kadhalika baada ya himaya hii ya ukoo wa 'Tai' kueneza istiimari yake kwingi duniani, Uingereza haikuweza kushindana nao tena.

Nchi hii ya Amerika imeweza kutoa makampuni makubwa, kama Firestone Rubber Company of United States of Amerika, ambayo Walter Rodney (1989:168) anaeleza;

> Katika mwaka wa 1926, the Firestone Rubber Company of the USA, iliweza kunyakua ardhi kiasi cha ekari milioni moja huko Liberia kwa gharama ya senti sita (6 cents) kwa kila ekari na asilimia moja ya mipira iliyosafirishwa nje ya Liberia --- Faida liyopatikana kutoka Liberia ilifanya faida ya kampuni hii kuongezeka na kuifanya kuwa miongoni mwa kampuni zilizopata faida nyingi zaidi. *(Tafsiri yetu)*

Kampuni hizi zilipata faida hii kwa kula jasho la Waafrika. Kampuni zingine zilikuwa za Wafaransa, Waingereza, Wajerumani na Wabelgiji baada ya kugawanya bara Afrika katika mkutano wao wa '*Berlin Conference 1884*'. Kampuni hizi zilichukua malighafi ya Afrika na kupeleka kwao. Faida zilizopatikana zilitumiwa kwa manufaa yao. Kupitia kwa unyonyaji huu nchi za Kiafrika hazikuweza kupiga hatua kimaendeleo. Mishahara ya Waafrika ilikuwa duni. Walter Rodney (1989: 162-165) anaeleza malipo waliyopewa na kujadili hali ya kazi ya Waafrika. Mwisho anaonyesha jinsi Waafrika walivyonyonywa. Maelezo ya Rodney yanachukuana sawia na maelezo ya Mkangi kuhusu hadithi ya moto kwa kuonyesha kwa njia ya taswira jinsi wageni walivyovumbua masoko mapya, wakatoza wenyeji kodi, wakachukua nchi yao, kula jasho lao kwa kuwatawala na kukita mizizi ya ukiritimba.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Kwa muhtasari Chacha (2003;18) anasema;

> Baada ya muda mrefu wa kutawaliwa na kunyanyaswa hivi, watu walierevuka wakaona unyama waliokuwa wakitendewa. Kwa kutumia silaha zile zile zilizowanyanyasa wakapata ujasiri, ukinaifu na fahamu. Umma ukazuka ukafanya mapinduzi yaliyowakandamiza Wachuna.

Maelezo haya yanaonyesha jinsi nchi za Kiafrika zilivyopata uhuru. Licha ya kupata uhuru, ukoloni mamboleo uliweza kuzuka. Nchi hizi zikawa za kutegemea wakoloni tena. Mabadiliko haya ya hatua za maendeleo ya maisha ya mwanadamu tangu alipopata moto ulioweza kumfaidi yanachukuana na nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Mabadiliko dhidi ya mazingira magumu, unyonyaji, ukupe, ubepari, ubwanyenye, umwinyi na kujikomboa dhidi ya udhalilishaji wa aina yoyote ndiyo yanayosisitizwa na mwandishi. Usawa wa kijamii ndio nguzo ya maendeleo, na ndio msingi wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa.

### 4.1.6 KISA CHA MCHAWI

Kisa hiki kinahusu mtu mmoja aliyeenda haja msituni. Alipokuwa katika harakati hizo za haja, kwa ghafula alisikia 'Chakarachakara' huko juu matagani. Naye kuangalia choo kikamwisha ! Hivi ndivyo ule msemo wa 'kukata choo' ulivyozuka. Majoka mawili yalikuwa yakipindana. Hivi vilikuwa vita baina ya bafe na chatu. Vita hivi vilikuwa vya kufa na kupona. Bafe alimtapikia chatu sumu kichwani ili kummaliza. Lakini chatu aliyekuwa amenyooka twaa

alijifyatua kwa ghadhabu na kumzonga bafe katika matiko yake na kumsaga mpaka akawa kima. Vita vikawa vimekwisha ingawa chatu alikuwa hoi. Baada ya muda mchawi aliona chatu akijikokota na kuenda chini ya mti mmoja na kuanza kuchimbua. Alivunja mizizi ya mti huo na kuanza kuimeza. Pia akaona chatu akibambua magomba na majani ya mti huo na kuyameza. Baada ya muda mfupi chatu huyo alipata afueni na kutoweka kwa kasi.

Baada ya kadhia hii ya chatu, mchawi aliende pale mtini na kubambua maganda, kuchimba mizizi na kuchukua majani na kuweka kikapuni na kuenda zake. Haya ndiyo sasa yangekuwa dawa siku za usoni. Kabla ya hapo yeyote aliyeumwa na nyoka siku zake zilikuwa zimekwisha (hangepona), na ilimbidi kutoa wosia. Lakini baada ya muda usiokuwa mrefu mchawi alitumia mizizi, maganda na majani aliyopata. Jirani wake aliumwa na bafe. Mwandishi anasema;

> Mchawi alionekana akiingia huko akibeba mizizi, maganda na majani. Mizizi na magamba aliyasaga unga na yale majani akayaingiza ndani ya chungu cha maji na kuyavuruga vuo. Huku akijitia kusema maneno yasiyoeleweka – ingawa ukweli ni kwamba alikuwa akiigiza zile kelele zilizowatoka majoka walipokuwa wakipigana, akatumbukiza ule unga wa mizizi na magamba ndani ya hilo vuo. Akichelea mgonjwa huenda akapatoka mbio baada ya matibabu kama vile chatu alivyofanya, akaamua kumfunga miguu. Kwa bahati nzuri, alipomfungia pakawa jeraha liko chini ya kifundo ... Akiigiza (mchawi) vile chatu alivyofanya, mchawi naye alijilaza tuli baada ya kumganga mgonjwa.
>
> *(ukurasa 160-161)*

Mchawi alimnywesha mgonjwa dawa hii aliyotengeneza. Muda si muda mgonjwa alionekana akiangaza macho hatimaye alikaa. Baada ya muda alipona kabisa. Mchawi alipoulizwa jinsi alivyopata huu uganga hakuwaeleza. Aliweka siri hii. Baadaye alipanua matibabu yake kuchukua magonjwa tofauti.

Kama moto, mchawi alitoa vitisho vyake kwa kusema kuwa hangeweza kuendelea kutoa huduma za matibabu kwa sababu ilimbidi naye aende kwake makondeni. Baada ya kusikia haya wanajamii walimwambia kuwa wangemlisha. Basi kutokea hapo ziada zikazidi kwake. Utajiri huu alioupata ulimtia hisia za kifalme, utukufu na mjua yote. Pia aliweza kurithisha watoto wake wa kiume siri hii. Aliwalisha kiapo ili wasitoe kwa mtu mwingine yeyote. Baadaye walibadilisha jina la mwanzilishi wao 'Mchawi' na wakajiita ni wa kutokana na ukoo wa 'Nyoka'. Alama hii ya nyoka hutumiwa kama ishara ya ujuzi wa madaktari ili kuonyesha juhudi wanazofanya kupambana na sumu. Alama hii ni taswira kuonyesha magonjwa tofauti kwa sababu nyoka huwa na sumu tofauti kutegemea aina ya nyoka na pia mahali ambapo nyoka hao hupatikana. Sumu tofauti huonyesha magonjwa tofauti. Jinsi nyoka walivyo wengi na tofauti ndivyo magonjwa nayo yalivyo.

Kisa hiki cha mchawi kinatoa maudhui yafuatayo; kwanza kinaonyesha uvumbuzi wa madawa tofauti kwa magonjwa tofauti. Pili kinatoa faida ya miti. Misitu ambayo ilikuwa imeharibiwa na Wachuna na kugeuza nchi kuwa jangwa.

Jambo jingine ni kuonyesha ubuguzi dhidi ya wanawake. Mchawi aliweza kurithisha ujuzi huu kwa wavulana peke yake. Inaonekana pia, baadhi ya kazi hizi za ufundi ziliwekewa watu fulani. Katika jamii za kibwanyenye ujuzi fulani wa kazi ulikuwa mikononi mwa watu fulani, ambao waliweza kuulinda ujuzi huu. Hata sasa taaluma hii ya udaktari imelindwa sana. Watu wachache huhitimu kutoka vyuo vikuu kuwa madaktari kila mwaka. Pia tunaona kuwa baada ya kuacha kazi yake kondeni, aliletewa vyakula. Mali aliyokuwa akiletewa ilizidi hivyo kwamba mchawi hakuwa akifanya kazi, kwa hivyo akawa 'kupe'. Alitegemea jasho la wengine. Kwa kuwa ndiye aliyekuwa na ujuzi wa matibabu aliwatoza bei ghali walioleta wagonjwa wao kutibiwa. Hata wakati wa sasa madaktari hutoza wagonjwa gharama kubwa kwa matibabu ambayo wao (madaktari) hutoa. Mwisho tunaona mchawi akinyonya jamii na kujitwika mamlaka ya kuwa mfalme au kutaka apewe heshima ya utukufu.

Hali kadhalika tunaona hali ya utabaka ikizuka. Kuna wafanya kazi na mabwanyenye.

Kwa kumalizia Mkangi anashtumu hali ya unyonyaji na utabaka. Mkangi anasisitiza hali ya ujamaa ambapo hakutakuwa na utabaka. Wanajamii watashirikiana kwa manufaa ya jamii nzima.

### 4.1.7 HADITHI KUU

**(Hadithi ya Dzombo)**

Hadithi ya Dzombo ndiyo hadithi kuu. Hadithi hii inaanza wakati Dzombo alifutwa kazi baada ya kumwambia ndugu yake kwamba hali yao ya ufukara inatokana na kunyanyaswa na kunyonywa na tajiri wao. Dzombo alifutwa kazi kwa kuchochea wafanya kazi. Baada ya kisa hiki Dzombo alikata shauri kujiajiri mwenyewe. Alishiriki kilimo. Alitaka kutegemea jasho lake. Alipanda mahindi. Mwandishi anasema;

> Mahindi sasa yameshaanza kutoa punga. Mengi yao (mahindi) yalikuwa bado yakificha nyoe. Na kila alipoamka na kuyatupia macho, ndivyo alivyozidi kuwa na imani katika uwezo wake wa kuzalisha mali. Harufu ya shibe ilikuwa imeshaanza kunusika alipoona jioni moja matingatinga yakiingia shambani mwake ! ... (*ukurasa 16*)

Waliendelea kuyafyeka mahindi yote shambani. Kisa na sababu ya kuharibu Mahindi yake ni kwamba alilima bila kufuata sheria – kupanda mahindi katika sehemu ambayo hairuhusiwi. Mimea ambayo ingelipandwa katika sehemu hii ilikuwa kahawa, kakao, pareto na hata maua ya waridi au katani. Yaaminika kuwa mazao hayo yangelileta pesa za kigeni. Wazo la kupata pesa za kigeni ni wazo ambalo huleta utegemezi. Mara nyingi shinikizo za utegemezi hutoka kwa mataifa ya kimagharibi. Katika muktadha huu shinikizo lilitoka kwa *Benki ya Dunia*. Huu ulichukuliwa kama ushauri wa kitaalam na hapakuwa na wa

kupinga. Dzombo katika harakati za kutaka kujua zaidi alizomewa na mrasimu aliyesema " na ikiwa una siasa zako za kipuzi, basi usizilete hapa ! Kisha akagonga meza kwa nguvu na kumfukuza ofisini".

Dzombo alirudi nyumbani ingawa alijua kuwa dau la mnyonge haliendi joshi. Alilima shamba lake tena na kupanda katani, kahawa, chai, pareto na miwa. Ajabu ni kuwa ilimbidi Dzombo aende kupiga foleni ili apewe kibaba cha unga wa chachu na maharagwe yenye vidudu ndani. Dzombo aliweza kutiwa hima kwa kuelezwa kuwa angefaidika kwa sababu bei ya mazao hayo katika soko la ulimwengu ilikuwa juu. Mavuno yalipelekwa kwa idara ya serikali inayojishughulisha na ununuzi wa mazao. Kwa mfano hapa nchini Kenya tuna Halmashauri ya Nafaka (Cereals Board) ambayo hununua mazao kutoka kwa wakulima na kuwalipa kwa njia ya hewala au hundi. Dzombo hakupewa pesa taslimu lakini kijikaratasi. Wakati alipoenda kwa malipo hakupewa chochote ila aliambiwa kuwa bado alidaiwa kwa sababu bei za ulimwengu zilishuka ghafla. Alipotaka kujua kile ambacho angekula wakati huo, aliambiwa na karani "Usijali. Tutapewa mkopo na marafiki zetu ili tuweze kukukopesha utulipe deni letu ili mradi uzidi kulima Kachatapami".

Kachatapami ambalo ni neno lililoundwa kutokana na maneno yafuatayo: kahawa, chai, katani, pareto, pamba na miwa. Hapa tunaona kuwa nchi nyingi za Kiafrika hazina uhuru wa kujiamulia mambo yake. Nchi nyingi zinategemea *Benki ya Dunia* kwa misaada ya kifedha. Pia nchi hizi za Kiafrika hutegemea

misaada ya chakula kutoka ng'ambo kwa sababu hazikulima mazao ya chakula. Hata kama nchi ina rutuba ya kutosha na mvua, vyakula lazima tutaletewa kutoka ng'ambo. Nchi nyingi za ulimwengu wa tatu hazima sera kuhusu uzalishaji wa chakula. Tunapanda kahawa, maua, pareto, chai ili kupata fedha za kigeni. Lakini hatupandi mahindi ili tuweze kutumia kwa chakula chetu. Mohamed, S.A. (1995), anatuonyesha kuwa baadhi ya misada hiyo huwa mibaya na huathiri wenyeji, Ongeti (1987) anaonyesha jinsi jamii zinashinikizwa kupanda maua ya waridi yatakayoleta pesa za kigeni na mimea ya mahindi iking'olewa kwa sababu haileti pesa za kigeni. Lakini mahindi ni chakula cha moja kwa moja. Naye Walter Rodney (1989) amezungumzia juu ya biashara hii isiyochukua usawa – biashara ya upande mmoja. Biashara ya aina hii haiwezi kufanya nchi zinazotoa malighafi kuendelea ila zinazidi kutegemea nchi zilizoendelea. Uombaji huu hutufanya kuwa wategemezi wa mataifa ya magharibi. Wakati mazao kama pamba, chai, kahawa na kadhalika yamenawiri, haya mataifa hupunguza bei. Ajabu ni kuwa bei ya mazao kutoka bara la Afrika hasa ya kuuza huwekewa bei huko ng'ambo!

Hadithi hii kuu inaishia kortini ambako Dzombo alihukumiwa kifo kwa sayari. Mashtaka dhidi ya Dzombo yalikuwa kwamba aliwachochea wafanya kazi. Mazrui (1981) anaeleza kuwa Lanina alishtakiwa na kuzuiliwa kwa sababu ya kuchochea wafanya kazi. Hii ndiyo mbinu ambayo wadhalimu hutumia ili kuwanyamazisha wanaharakati wanaotetea haki zao. Katika mahakama hii

Dzombo hakutarajia haki kutendeka. Hizi zilikuwa mahakama za wenye nguvu. Mahakama hizi hazikuwa zikilinda na kudumisha haki kwa mujibu wa sheria zilizowekwa. Kazi kubwa ya mahakama hizi ilikuwa kumtia hatiani yeyote yule aliyepatikana na kisirani na kushtakiwa. Kuhusu mashtaka dhidi ya Dzombo mwandishi anasema;

> Hakimu aliingia kama malaika wa mauti humo mahakamani, kwani alipaoingia tu na watu kuamriwa kuketi, yule hakimu aliegemeza miwani yake ya nusu glasi puani kwake. Huku akimtazama kwa ile sehemu iliyokuwa wazi akamwamrisha kusimama. Zama hizo, mahakama hayakuwa yakifuata sheria kwa mujibu wa kulinda au kutetea, wala kudumisha haki za binadamu. Kazi yake kubwa ilikuwa ni kumtia hatiani yeyote yule aliyekuwa amepatwa na kisirani cha kushtakiwa... hakimu naye bila kusita, akatamka: kifo! Baada ya kuhukumu akazoazoa majoho yake na kuelekea ofisini kwake chembani. (*ukurasa 1*)

Mahakama za namna hii zilitumiwa kudumisha udhalimu katika jamii. Hizi ndizo zilizokuwa mahakama za jehanamu. Hukumu za namna hii zinanaweza kufananishwa na zile zilizotolewa katika nchi ya *Kusadikika* katika Riwaya ya Shaaban Robert *Kusadikika* (1951) au katika riwaya ya Mohamed, S.M. *Nyota ya Rehema* (1976). Hukumu za namna hii ni zile za kugandamiza wanyonge wanaopigania haki zao. Hapa nchini Kenya kuna mabadiliko yaliyofanyiwa idara ya mahakama kutokana na ufisadi uliokithiri kwa muda mrefu.

Pia katika hadithi hii kuu mwandishi anatumia msamiati <u>Paa</u>, <u>egesha</u>, <u>kwepa</u>, <u>mbizi</u> na <u>tua</u>. Huu msamiati umejikita katika jazanda ya 'usukani' . Kila mfumo

huwa na sera au itikadi yake. jazanda ya usukani inaashiria uongozi wa namna fulani. Huu uongozi hutegemea kiongozi ambaye huwa na wasaidizi au washauri. Mwandisi anasema;

> Sio wote wajiitao marubani huwa kweli wanao uwezo wa kumiliki usukani ! Huwa ni marubani bandia. Hawa hufurahikia sana kuitwa marubani pasipo hata kujua usukani wenyewe uko wapi? Wao pamoja na vyombo vyao hutekwa nyara na marubani halisi ambao huwa wamejificha nyuma ya pazia na kuwaacha hawa marubani bandia kuwa wanaserere au shehena ya mzigo. Wakishinda kuviegesha hivyo vyombo vya kule wasemapo wanaenda hujikuta wakivurumishwa maporomokoni na miambani kwa makusudi, huku wakiachiwa kupiga mayowe.... Aghalabu mabadiliko haya hayazuii hata kidogo kuendelea kwa safari kwa mujibu wa matakwa ya wale waliokaa nyuma ya pazia.
> (*ukurasa 7 - 8*)

Mawazo ambayo mkangi anatoa kuhusu safari ya Dzombo yanaashiria kwenye uongozi. Kiongozi mara nyingi huwa na wasaidizi wake. Lakini ushauri mbaya kutoka kwa wasaidizi hufanya maongozi kwenda mrama. Huu ushauri mbaya ndio huleta uhasama na dhuluma kwa watawaliwa, hata inabidi watawaliwa kutamani mabadiliko ya uongozi. Hapa Mkangi anatoa ushauri wa uongozi bora kwa kusema;

> Dzombo alijua – ili yeye aweze kuishi, usukani alikuwa hana budi aushike na kuumiliki. Nini tena maana ya maisha ya mtu kuwa mwake mkononi?" Mwenzako anayo yake – atapata vipi nafasi mwake mikononi kuyachukua yako na kuyapuuza yake? *(ukurasa 8)*

Baadhi ya washauri huweza kumpotosha kiongozi. Lazima kiongozi adhibiti uongozi vilivyo. Nchi nyingi za ulimwengu wa tatu zimejikuta taabani kwa sababu ya uongozi mbaya.

Katika safari yake Dzombo alikumbana na shida tofauti. Shida hizi zinadhihirika kupitia kwa taswira ya jabali la ujinga, ugonjwa na udhalimu. Nchi za Kiafrika zilipopata uhuru mwanzoni mwa miaka ya sitini zilikabiliwa na matatizo makubwa matatu, ambayo yalikuwa ugonjwa, ujinga na umaskini. Viongozi wa wakati huo walihiari kutangaza vita dhidi ya maadui hawa watatu. Baadhi ya magonjwa haya yaliweza kukomeshwa kupitia kwa chanjo. Lakini mengine ambayo yalikuwa rahisi kuzuiliwa bado yangali nasi hadi wa sasa. Kwa mfano ugonjwa wa utapia mlo. Katika *kisa cha mapacha* jambo hili limejadiliwa. Vyakula vinavyofaa ni bora kwa afya yetu. Watoto kutoka matabaka ya chini hushikwa sana na ugonjwa wa utapia mlo. Chacha (2003:7) anasema;

> Pia anakutana na miamba ya magonjwa ya marasimi na 'kwashiokor' ambayo ni ya kitabaka. Haya yanatokana na ukosefu wa chakula bora na hali hii hulipata tabaka la chini, utatuzi wake ni 'kuangusha paa' yaani kuondoa tofauti za kitabaka.

Pia kuna ujinga, huu ndiyo hutufanya sisi kuwa watumwa na mataifa ya kimagharibi. Tunakuwa watu wa kutegemea wageni kwa kila hali, hasa *Benki ya Dunia, Hazina ya kilimwengu ya Pesa* (IMF) na misaada mingine kama anavyosema Mohamed Said Ahmed katika tamthilia ya *Amezidi* (1995).

Uwekezaji wa wageni ni ule wa kunyonya malighafi ya Afrika kwa manufaa yao. Wakoloni walitaka tu kuendeleza uchumi ulioweza kuleta pesa, kwa mfano mpira (Rubber) katika nchi ya Liberia, dhahabu kutoka Afrika Kusini, shaba kutoka Mkoa wa Shaba (Katanga) au katani kutoka Tanganyika. Unyonyaji huu ndio uliodhalilisha nchi nyingi kutoka bara hili Walter Rodney (1989:227) alizungumzia suala hili kwa kirefu aliponukuu katika *Azimio la Arusha*, kwa kusema "tumedhulumiwa sana, tumenyonywa na kunyanyaswa sana, tumedhalilishwa na kutodhaminiwa sana."

Ukweli huu ulioelezwa kuhusu ukoloni katika bara la Afrika ulionekana katika huduma za jamii zilizotolewa, miundo msingi na mawasiliano. Hata hivi sasa uhuru wetu ni uhuru wa bendera. Mwandishi anasema;

> Kifafa hiki huleta majereha ya kuomba kusikoisha ili ati mgonjwa aweze kujitibu maradhi yake. Hali hii humfanya mgonjwa kutokwa na majipu ya kuombaomba mwili mzima. Hapo, ndipo kule kutokuwa na pesa kuzidipo kujidhihirisha kwa mwili mzima kupachikwapachikwa mabendeji ya matibabu ya misaada. Mabendeji haya hukazwa machoni na kuachiwa mdomo. Mgonjwa hupewa kijiti na kushikwa mkono kuongozwa. Ajabu ni kwamba ingawaje yuko mahututi namna ile, mgonjwa huyu haachi kubwata na domo lake lililo wazi wakati wote: "Mimi niko huru. Mimi niko huruu. Mimi niko huruuu", kama sahani ya santuri iliyokwama, kila hatua asaidiwayo kujikokota.
>
> (*ukurasa 27*)

Hatuwezi kufanya chochote kando na mahitaji yao (wageni). Hapo sasa kilichobaki ni ukoloni mamboleo. Utegemezi unaozongumziwa katika hii dondoo ndio uongozi wa kutoka nyuma ya pazia uliozungumziwa na mwandishi.

Jambo la tatu ambalo Mkangi anazungumzia ni jabali la dhuluma. Dhuluma hizi ni dhidi ya Wakristo, Waislamu, Waafrika, Wayahudi na Wasomi. Wasomi wengi walikuwa wametendewa udhalimu wakati riwaya hii ilipoandikwa. Kupitia kwa jabali la udhalimu mkangi alitaka kuonyesha dhuluma iliyojikita katika jamii. Magonjwa, udhalimu na ujinga vimeweza kufanya ulimwengu mahali pabaya kwa mwanadamu. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia wa kijamaa ulimwengu ulihitajika kuwa mahali salama pa mwanadamu. Hadithi hii kuu ni hadithi ya uzinduzi kwa wanadamu.

Ingawa Dzombo alihukumiwa 'kifo' aliweza kutua katika nchi ngeni kwa jina Walenisi. Akiwa katika nchi ya Walenisi jina la Dzombo liliambishwa kwa kiambishi awali 'mtu'. Kiambishi hiki kinamaanisha utu. Kutokea hapo jina lake likawa Mtu-Dzombo. Dzombo alilakiwa na familia ya watu sita. Hawa ndiyo waliokuwa wenyeji wake. Walenisi ilikuwa kama mbinguni, ni kinyume cha Jehanamu (duniani) ambako Dzombo alitoka. Alipofika hapa Dzombo alichanganyikiwa asijue la kufanya. Chumba alicholala kilikuwa vioo tupu. Maandalizi ya staftahi yalikuwa tofauti kabisa na alikotoka. Hapa aliona kwamba yumo katika jumba la kugeuza mwili wake uwe sasa wa kiroho. Hii ni hatua ya kwanza ya mabadiliko. Alipokewa katika nchi ya Walenisi na kupelekwa kwa safari ya utu.

## Safari ya utu

Safari hii ilikuwa ya kumfahamisha Mtu-Dzombo nini maana ya utu. Katika safari hii Dzombo aliandamana na Mtu Bint Fikirini na kakake Mtu Wazo. Safari hii ilikuwa kwa trimi, chombo cha kusafiri kinachoenda mwendo wa kasi sana. Kwanza alitembea kwa miguu. Katika matembezi haya yaliyotangulia safari hii ya utu, mwandishi anasema;

> Dzombo alishtuka kugundua kuwa, kokote kule alikotembezwa, hakuwa ameona dalili yoyote ya umaskini kama waombaji, watu wasio na makao, umalaya, majaa ya takataka yenye uvundo na nzi chungu nzima, walofa, watoto chokora, wachoma mihogo na mahindi, na dalili nyingi kama hizol Hakuwa ameona uchoyo. Hakuona uvivu... unyonge... ubarakala. Hakuona unyapara,...dhuluma...Hukuona... ala ! Wewe hapa ni mbinguni aka ! Mambo lazima yawe mazuri, sawa na ya kupendeza. Sio kama duniani utokako. *(ukurasa 49)*

Mkangi anatuonyesha sura ya mandhari ya Walenisi. Mandhari hii ni ya kiutopia. Sio rahisi kufikiwa. Mwandishi huyu katika kutafuta uhalisia anataka nchi kama hii. Nchi hii si rahisi kupatikana. Mambo ambayo Dzombo aliona ni tofauti kabisa na yale ya jehanamu. Huko jehanamu kuna kila aina ya matatizo na shida. Kwa mfano waombaji wamejaa mjini, takataka ni tele na walio wachochole ni tele. Kuna malofa ambao hawana cha kufanya. Hawa malofa wakikosa cha kufanya hugeuka na kuwa wahalifu. Hapa nchini kwetu Kenya pamejaa haya matatizo na shida hizi ambazo mwandishi anazungumzia. Kwa

mfano majaa ya takataka, chokoraa, watu wasio na makao miongoni mwa mengine.

Shida hizi zote zinatokea kwa sababu ya uongozi mbaya, utabaka, ubinafsi na umilikaji wa mali za asili na watu wachache. Wazo hili linapatikana katika *hadithi za Wachuna*. Umilikaji wa mali ya asili na watu wachache huzua ubepari na unyonyaji wa Wachuna ambao hawana msamiati wa haki katika lugha yao.

Baada ya kwenda kwa miguu na kuona mandhari ya nchi, Dzombo aligundua kuwa njia za usafiri zilikuwa bora. Halafu waliabiri chombo cha kusafiri ambacho huitwa Trimi. Chombo hiki huenda kasi sana. Kwa mfano Trimi waliyoabiri ilisafiri muda wa siku kumi mwendo ambao ungechukua miaka kumi kwa kutumia sayari. Unaweza kuulinganisha usafiri huu wa Trimi na huu ulio hapa Kenya. Hapa nchini Kenya barabara zimeharibika mpaka magari hayawezi kwenda kasi. Pili, jambo hili limeongezewa kwa kuweka vidhibiti mwendo katika magari, kwa sababu wengi huendesha magari kwa kasi bila uangalifu na husababisha ajali. Vyombo (Trimi) hivi vilikuwa imara kwa safari. Dzombo aliajabia yale aliyoyaona walipokuwa safarini. Lakini alielewa kuwa haya yalitokana na juhudi za Walenisi. Mtu Dzombo alipigiwa hadithi na Mtu-

Wazo kwa kusema;

> Hapo zamani kulikuwa na watu waliokuwa wakikaa vile umekaa, nao hawakuwa wakiacha kumsifu Mungu kwa ziada zote walizojipatia kutokana na juhudi za wengine. (*ukurasa 52*)

Kisa hiki kinaonyesha unyonyaji na uzembe kwa sababu hawakuwa wakijishughulisha na lolote. Hawa watu walikuwa wamehitimu katika ulaghai. Kwa kutumia mbinu tofauti tofauti za ulaghai. Walihadaa wengi kwa karne nyingi. Dzombo alitaka kujua kama kulikuwepo na upinzani dhidi ya hawa walaghai lakini anaeleza;

> Haukukosekana. Lakini kwa kuwa wengi hawakuwa na kisomo, waliogopa kwa kirahisi na kudanganyika haraka. Na wale waliokuwa nacho walinunulika kipumbavu kwa minajili ya ubinafsi wao wa kupindukia. Kwa hivyo upinzani ulichukua muda mrefu, kuimarika kabla ya wao kutambua kuwa adui wao alikuwa mmoja, na hawakuwa na budi bali kufungamana kwenye nia moja na kuwa na lengo moja. - Baada ya kunyamaza kwa muda fulani, Dzombo aliuliza: "Waliitwaje watu hawa? "Wachuna". Walimwambia kwa pamoja.
> *(ukurasa 52)*

Lengo hili moja ni juhudi za kung'oa unyonyaji na ubepari. Pili umma ulizidi kuhamasishwa kuhusu adui wao. Wazo hili lilitendeka hivi majuzi hapa nchini Kenya wakati wanaharakati na wakereketwa wa siasa za vyama vingi walikuwa wakipiga serikali vita, wakitaka mfumo wa vyama vingi. Baadhi ya vyama hivi ni;- Liberal Democratic Party, Ford Kenya, Democratic Party, Ford Asili, National Democratic Party na Independent Party of Kenya, miongoni mwa

vyama vingine. Wengine walinunuliwa na serikali na kuhama vyama vyao ili wasiunge mkono harakati hizi za ukombozi. Jambo la tatu ni kuwa hawa wadhulumiwa hawakujua kuwa adui wao alikuwa mmoja, kwa hivyo ilihitajika wao kuungana ili kung'oa utawala huu mbaya. Wazo la mwisho katika maelezo ya kijana Mtu-Wazo ni kutahadharisha dhidi ya ubinafsi ambao huzua matabaka na ubepari. Mambo haya mawili ni adui mkubwa wa harakati za kuleta ujamaa. Huu ndio uliokuwa utawala wa Wachuna. Hadithi ya Wachuna itaelezwa baadaye. Licha ya hadithi iliyotolewa na kijana Mtu-Wazo, Dzombo bado alidhihirisha athari na kasumba za ubinafsi alizotoka nazo huko duniani (Jehanamu). Kwa mfano walipokuwa safarini walipatiwa maji ya kukonga roho, hakuwapatia wenzake ila alikunywa hadi akaanza kuteuka na mengine akajimwagia. Alifikiri amebahatika kupata maji.

Huu ni ulafi na ubinafsi. Dzombo alikuwa bado hajajua maana ya utu, -kushirikiana. Alipopewa mkate hakuwapatia wenzake. Aliteuka kwa shibe ilhali wenzake walikuwa na njaa. Kwa upande mwingine kijana Mtu-Wazo alipopewa miavuli aliwapatia hao wenzake kila mmoja mwavuli wake. Hili ni wazo la ujamaa lililo kinyume na ubinafasi wa Dzombo. Hata alipopewa mablanketi matatu kujistiri baridi kali hakuweza kuwagawia wenzake. Wenzake walihisi baridi kali, lakini Dzombo alisema kuwa alibahatika.

Kwa muhtasari ingawa safari ya utu ilikuwa na matatizo mengi, ilimfahamisha Dzombo ushirikiano, ujamaa na matumizi bora ya ardhi kwa manufaa ya wote, kumfahamisha njia bora za usafiri na kumfunza ngano za Walenisi ambazo zilikuwa na mafunzo kochokocho. Katika safari hii ya Utu Dzombo alikutana ana kwa ana na utu lakini yeye akaubinafsisha na kuwanyima mavuno ya safari.

Baada ya safari walikaribishwa kwa mlo na wenyeji wake. Meza iliandaliwa. Mwandishi anasema;

> Meza yenyewe haikuwa kama hizi za kitabaka, ya urefu na mapana yasiyolingana na yenye viti vya maumbo tofauti ili kuonyesha tofauti za kijamii kati ya binadamu... licha ya meza hii kuwa mviringo hakukuwa na kiti ama mahali maalum kwa mtu fulani kuketi. Mtu alikaa mahali alipopenda. Desturi hii haikuwa kwa nyumba hii pekee yake, bali ndiyo iliyokuwa itikadi katika kila nyumba katika ulimwengu huu mpya. *(ukurasa 67)*

Maelezo haya ya Mkangi yanatuelekeza kwa ujamaa. Mfumo huu ulimwathiri Mkangi sana; hasa aliponiambia (mtafiti) kuwa baadhi ya watu waliomwathiri ni Mwalimu Nyerere, Karl Marx, Yesu Kristo, Mao Tse Tung' na Fidel Castro wa Cuba miongoni mwa wengine. Hawa ni wanamapinduzi waliosisitiza mfumo wa ujamaa. Mfumo huu unaenda sambamba na mihimili ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa – kuleta usawa na umoja katika jamii. Katika nchi ya Walenisi

maisha ni sawa kwa raia wote. Hakukuwa na ubaguzi katika jamii hii baina ya wanawake na wanaume. Watu wote ni sawa.

Safari hii ya utu ndiyo iliyotoa hadithi za Mabavu, Moto, Mapacha na Mchawi baada ya Dzombo kufanya utafiti katika maktaba kuu ya Walenisi. Pili, baada ya safari alikuwa na mawazo, kumbukumbu ya Maskini Jeuri rafiki yake aliyebaki kule jehanamu. Dzombo alijifunza mambo mengi huko Walenisi. Aliweza kujua kazi ya mapenzoni. Mwandishi anasema;

> Kwanza ni kueneza mapenzi halisi ambayo yameshinikizwa kikiki katika uchumi wa kitu. Pili, ni kupongezana, kushauriana na kutiana shime. Na tatu kuondoa ufyanduzi na kuupinga usirudi.... Sisi Wawalenisi tunajitawala, na ajitawalaye hashurutishwi wala kuambiwa – hujiambia... *Wawalenisi* wako huru, na watu huru hawashindwi kamwe kutatua mafarakano na matatizo kati yao. Hii ni kwa sababu uhuru ni kujijua na kujifahamu ili kuweza kujitawala vilivyo katika kila jambo pasipo kushurutishwa ama kuogofya na yeyote ama na chochote. (*ukurasa 203 - 204*

Katika dondoo hili Dzombo ana mambo mengi aliyojifunza. Mapenzoni ni namna ya Bunge au Baraza kuu la *Walenisi*.

Dzombo pia alijifunza kujitambulisha na maskini, lazima kupigania haki za kila binadamu, kuwainua wanyonge, kukomesha kila aina ya mateso kama ya wale walio magerezani, lazima pawe na viongozi wa kuona, kusikia na kusema kwa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

minajili ya wale walio mabubu na waoga. Alijifunza maana ya mapenzi ambayo yanatokana na vitendo halisi. Haya mapenzi yalihusu migawano iliyo bora. Mwisho akajifunza kuwa si dhambi kuwatetea wanaonyanyaswa na kupiga uchuna marufuku. Baada ya maajabu haya, ambayo Dzombo aliona katika safari ya utu, alifikiria kwao. Wakati huo Dzombo alifunga ndoa na Mtu-Bint Fikirini. Mawazo ya kurudi kwao Jehanamu yalimsumbua Dzombo. Moyo ulishikwa na simanzi kwa sababu ya ufahamu wa kiutu ambao sasa amejifunza. Dzombo anamweleza Mtu Bint Fikirini;

> Ufahamu wa kiutu umenifanya kuwafikiria wenzangu huko jehanamu – vile wateswavyo, wanyanyaswavyo, waumizwavyo, wapumbazwavyo na kwa jumla, kuishi katika hali ya uzima – Mauti ya ukweli uongo wanaopewa na Wachuna wa huko.... Ni fikira hizi ndizo zinitiazo simanzi sana mara kwa mara...
> Waonaje sasa? Mkewe akamwuliza. "Uhuru wa mtu mmoja, ama kushiba kwa mtu mmoja, hakuna maana ikiwa wengi wako utumwani ama wangali wanakufa kwa njaa.... Kwa hivyo nimefikiria kurudi kwetu Jehanamu". Bibiye akimkatiza akamwuliza, Ukawazindue? *(ukurasa 216 - 217)*

Safari ya utu ilimfunza Dzombo mambo mengi ambayo yangesaidia maendeleo ya huko kwao (Jehanamu). Pili, alijifunza kuwa wanadamu lazima wafanye bidii katika kupambana na udhalimu. Walio waoga na wasioweza kudai haki zao lazima waongozwe. Uongozi huu ndio Dzombo anaenda kutoa. Angelitoa uzinduzi kwa kuwaeleza haki zao, kuonyesha udhalimu na mbinu za ukombozi.

Mwisho mwandishi anatueleza kuwa Dzombo na mkewe mjamzito walifunga safari kurudi duniani mahali ambapo watu huteswa na kunyanyaswa na wengine hasa watawala. Watawala huwanyanyasa na kuwadhulumu watawaliwa. Haya yalikuwa mateso ya Wachuna. Kurudi kwake Jehanamu ni njia ya ukombozi. Dzombo ndiye atakayeongoza mapinduzi. Haya yatafanyika kama yalivyofanyika katika nchi ya Walenisi. Kama ilivyo kawaida mapinduzi ya aina yoyote huhitaji uongozi bora kama anavyosema Al-Amin Mazrui (1984).

### 4.1.8. HITIMISHO

Katika kutoa muhtasari tumeona hadithi kadha katika riwaya hii ambazo zina maudhui mazito ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika baadhi ya hadithi hizi mwandishi ametumia muktadha wa kihistoria. Wamitila (2003:136) anasema;

> Mwandishi wa *Walenisi* anatumia basi muktadha wa kihistoria, kama nyenzo ya kumulika masuala mapana yanayoihusu jamii yake na jamii pana ya ulimwengu na kwa njia hii kuhimiza na kumjasirisha msomaji wake kuyafungua macho kuyaangalia mazingira yake (Ya kisiasa, kiuchumi na kijamii) kwa jicho la ndani. Msomaji wa riwaya hii anapaswa basi katika kusoma kwake, kujihusisha na kile kinachojulikana katika uhakiki kama 'hemenitiki za kituhuma' (hermaeneutics of Suspicion) yaani pana umuhimu wa kuyatilia maanani mambo ambayo riwaya hii haisemi waziwazi --- ambapo yasemwayo na yasiyosemwa yana uzito sawa.

Kuna mambo mengi ambayo yamejikita katika hadithi za Mkangi. Kwa mfano hadithi ya Mapacha. Hadithi hii inaonyesha hali ya jamii hasa kwa upande wa

matibabu na masuala mengine ya kijamii. Maelezo ya kihistoria na masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yaliyo katika hadithi hizi yamejikita katika nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Katika kuangalia mihimili ya nadharia hii tuliona kuwa historia na siasa haziwezi kutenganishwa kwa sababu fasihi haiwezi kujitenga na masuala ya kijamii. Pili Mkangi anapendekeza jamii isiyo na dosari. Jambo hili linadhihirika katika hadithi kuu ya Dzombo alipokuwa katika nchi ya *Walenisi* na kule Jehanamu. Mawazo haya yanapingana kuonyesha uzuri na ubaya. Huu ni ulinganifu wa jamii mbili. Tunaweza kusema kuwa hii ni athari aliyopata kutoka kwa Shabaan Robert (1951). Mwisho wema hushinda. Tunaona Wachuna waking'olewa na nchi hii inarudi kwa wenyeji Wawalenisi ambao mwito wao unakuwa;

> SHIME twende mbele; UBINAFSI tuushinde; USHINDANI tuuzike; Uchuna UPINGIKE ufyanduzi USIZUKE na Uwalenisi ni MAPINDUZI... (*ukurasa 214*)

Huu ndio uliokuwa mwito wa Walenisi. Mwito huu ni nguzo ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa, kwa sababu nadharia hii inasisitiza mapambano katika jamii ili kung'oa uozo uliopo na kuufanya ulimwengu mahali bora pa kuishi. Hali kadhalika historia ya mwanadamu imeonyesha kuwepo kwa harakati za mapambano baina ya matabaka kwa mfano katika *hadithi ya Mapacha*, *hadithi ya Mabavu* miongoni mwa hadithi zingine.

Tatu, katika kutongoa hadithi zake, Mkangi anaeleza kuwa anataka jamii

ambayo haina serikali, anasema "serikali ni chombo cha kulinda na kuendeleza maslahi ya tabaka fulani tu pekee, huku wakidai kuwa ni watumishi kwa wote. Ingawa Mkangi mwenyewe pia anatambua kuwa serikali ni chombo muhimu na hakiwezi kukosekana katika jamii yoyote ijionayo inaendelea kustaarabika. Anataka pasiwe na walinda usalama. Mzee Mtu Mwenzio anamweleza Dzombo kuwa;

> Lakini kwa kuwa sisi jukumu letu ni kuona usawa kati yetu, nadhani ushaona Mtu Dzombo kuwa hapa Walenisi hatuna askari wa namna yeyote, wala magereza. Tuna mahakama ... lakini si ya kitabaka namna ya zilivyokuwa wakati wa Fyanduzi za Wachuna. (*ukurasa 203*)

Chombo cha utawala lazima kiwepo. Kutokuwepo kwa magereza ni ishara kuwa hakuna wahalifu. Mawazo haya ni mawazo ya kiutopia. Mawazo yasiyopatikana katika uhalisia wa mwanadamu. Kwa upande mwingine serikali ni chombo cha ugandamizi. Katika *hadithi ya Maskini Jeuri* tunaona ufisadi na umaskini ukiwa katika mstari wa mbele na hatuoni serikali ikifanya lolote ili kuwakwamua waliozama katika lindi la umaskini au walala hoi. Jamii isiyo na dosari ndiyo jamii ambayo Mkangi anaipigania. Wazo hili linafungamana na mawazo ya kimarx ambayo yanapigania kuwepo na jamii isiyo na matabaka ya aina yoyote.

Baada ya kuona yale yote aliyoyaona Dzombo anahiari kurudi kwao Jehanamu ili kuwazindua aliowaacha huko. Hili linachukuana sambamba na maoni ya Arvon H. (1973;87) 'ya kuacha umma na matumaini'. Pia mtazamo wa nadharia hii hupinga ubepari na ubwanyenye na kuhimiza ujenzi wa ujamaa. Haya ni mambo ambayo Mkangi amedhihirisha waziwazi katika hadithi zake. Mbughuni (1978:12) anasema kuwa binadamu ana uwezo wa kusema juu ya hatima yake, anaweza kuhiari uzuri au ubaya, haki au dhuluma na katika kufanya hivyo huwa anashiriki katika umbuji wa historia. Historia ni msingi wa matukio ya wanadamu, hadithi hizi kama tulivyosema zimejikita katika misingi ya kihistoria.

Kama alivyosema Plekhanov *katika Marxist Esthetics* (1973:12), Mkangi ametumia sanaa kueleza matukio yaliyo katika jamii yake na jamii ambayo angelipenda wanajamii kuwa nayo. Matukio yaliyo katika sura ya nne yamefungamana na mihimili ya nadharia ya uhalisia wa kijamaa. Kurudi kwa Dzombo kutoka nchi ya wawalenisi ni mbinu mpya ya kuleta mabadiliko katika jamii. Matumizi ya hadithi kama nyenzo ya kutolea maudhui katika riwaya hii yanachukuana na mbinu na misingi halisi za umarxi kama anavyotueleza. Ngara E. (1985:75) aliposema "sanaa ya nchi tofauti za ujamaa yana ujamaa katika urithi wake, ingawa kila moja ina sura yake tofauti kulingana na utaifa". Katika kukunja jamvi, sura hii imechunguza hadithi tofauti na maudhui tofauti yaliyojikita ndani. Mtindo wa usimulizi utajadiliwa katika sehemu inayofuata.

**Utangulizi:**

Mtindo ni nyenzo muhimu katika uandishi wa kubuni. Mtindo ndio unaoweza kutofautisha maandishi ya mwandishi fulani kutoka kwa mwingine. Kazi za Mkangi ni miongoni mwa maandishi yaliyochukua mtindo tofauti ili kutoa maudhui yake mazito. Katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi* Mkangi ametumia mtindo wa fasihi simulizi kuyaendeleza maudhui yake. Tamthilia ya Ebrahim Hussein (1976) pia imetumia mtindo huu wa kijadi. Wamitila (2003:57a) anasema haya kuhusu riwaya ya *Mafuta*;

> "hii ni riwaya inayochunguza maisha na mivutano ya kitabaka katika jamii ya kikoloni – Mambo leo. --- jamii ambayo Michel Foucault katika kitabu chake *Discipline and Punish* anaieleza kama 'jamii ya kigereza'. Ni jamii inayodhibitiwa kwa kila njia, inachungwa katika matendo yake yote na inatengwa na kuonekana kama kundi la wahalifu na tabaka ndogo la matajiri".

Dhamira hii iliathiri mtindo wa uandishi kwa kutumia mafumbo kama asemavyo Chacha (2003:47). Pili mfumo wa watawala uliweza kuathiri uandishi huu wa riwaya ya *Mafuta*:

Uteuzi wa maneno ya Mkangi katika riwaya zake *Mafuta* na *Walenisi* unaonyesha toni ya uchungu na ukali, kwa kuchukulia kuwa wakati mmoja Mkangi alitiwa mbaroni na kuzuiliwa kwa muda wa miaka miwili. Mtindo wake umetokea kuchamba serikali.

### 4.2.1 MTINDO WA USIMULIZI

Uchanganuzi wa maudhui katika *Mafuta (*1984) na *Walenisi* (1995) ulishirikisha pia uchanganuzi wa mbinu za usimulizi zilizotumiwa. Miongoni mwa mitindo ambayo Mkangi ametumia ni masimulizi ya kinafsia, ndoto, tawasifu, mazungumzo, mafumbo, kumbukumbu, taswira ya safari, nafsi tofauti za usimulizi hasa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu, mazungumzo ya mtu na nafsi yake na matukio ya kihistoria miongoni mwa mengine. Mbinu za uzimulizi zimejadiliwa katika sehemu hii na kutolewa mifano ya kudhihirisha. Kwanza kabisa Mkangi anatumia masimulizi ya kinafsia. Usimulizi wa namna hii huchukua wahusika wengi ambao hutoa maelezo kuhusu tukio au mambo. Katika masimulizi haya, nafasi ya nguli huwa haitawaliwi na mhusika mmoja. Ngara (1985:71) akizungumzia juu ya riwaya ya Ousmane *Gods Bits of Wood* (1976) anasema,

> Muundo wa riwaya unafanana na aina fulani ya hadithi za kale. Kuna hadithi kadha zinazotokea mahali tofauti. Riwaya hii si juu ya mhusika mmoja mkuu au wawili, ambayo ni mbinu ya kawaida. Riwaya ya Ousmane ni juu ya jamii nzima ya wafanyakazi na wakulima. Mtazamo wa aina hii huafikiana na dhana ya ujamaa wa Mwafrika na kuonyesha siasa ya ujamaa ambayo hulenga juu ya watu (wahusika) na sio mtu (mhusika) binafsi. Kwa kutumia mbinu hii Ousmane haafikiani sana na riwaya za kibwanyenye na kibepari ambazo husisitiza nguli. Ingawa watu lazima wawe na kiongozi, mapambano lazima yawe na siasa maalum.

Maneno haya ya Ngara yanatoa sifa ya matumizi ya hadithi katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi.* Kuna wahusika na hadithi tofauti zinazotolewa mahali tofauti lakini zote zilidhamiria kutekeleza wazo moja la mapinduzi ya

kuwaondoa wanyonyaji, wadhalimu na hali ya utabaka. Katika riwaya ya *Mafuta* mwandishi anasema,

> ... Usoni pake kulisimama akina msati, Ti, Matope, Gweni, Mbeyu, Jasho, Pakacha, Nyepi ... na wengine wengi. Wote wakiwa na tabasamu nyusoni. Twende, waliwaambia, "kwani maji tumeyakomboa, na kuwakaanga na mafuta yao wenyewe. *(ukurasa 89)*

Maelezo ya mwandishi yanaonyesha ushirikiano wa pamoja katika kukabiliana na udhalimu. Wahusika wako pamoja. Katika riwaya ya *Walenisi* tunaona Dzombo na mkewe Mtu Bint Fikirini akiwa mja mzito wakirudi huko jehanamu ili kuwazindua watu wa huko kwa sababu uhuru wa mtu mmoja au shibe ya mtu mmoja haina maana iwapo wengi wanaishi katika utumwa au kufa kwa njaa, kuteswa na kunyanyaswa. Hii inaonyesha hali ya ujamaa. Wahusika wote wanajitokeza pamoja na wengine wengi. Wazo hili pia lilionyesha kuwa ukombozi unatekelezwa na wote. Matumizi ya mbinu hii ya kijadi na kisasa inaashiria uhalisia wa kanuni za mbinu za Ki-Marx namna inavyoelezwa na Ngara (1985:73) kwamba sanaa ya uandishi ya nchi tofauti ya kijamaa ina ujamaa kama yaliyomo, ingawa yana sura yake tofauti ya kitaifa.

Sura ya kitaifa katika kazi za Mkangi *Mafuta* na *Walenisi* ni kuzindua wachochole kupitia kwa hadithi zinazotolewa katika riwaya hizi (Tazama hadithi hizo). Hatima ya hadithi zilizotolewa katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* ni kuasi dhidi ya mfumo wa ugandamizaji, utabaka na unyonyaji katika riwaya

zote mbili. Riwaya ya Ngugi *Matigari* (1987), Mohamed S.A. *Dunia Mti Mkavu* (1980) ni mifano ya baadhi ya maandishi ambayo yametumia usimulizi nafsia. Jambo hili ndilo lililotumiwa na Mkangi katika *Mafuta*.

Mbinu nyingine ambayo imetumiwa katika riwaya hizi ni ile ya tawasifu. Mhusika huweza kutoa historia yake na maendeleo. Mbinu hii inapatikana katika hadithi ya Mama Fofi na mumewe Sifa. Hadithi ya Matope inasimulia shida alizozipata hadi akatiwa mbaroni. Katika riwaya ya *Walenisi* maelezo ya Dzombo kujitambulisha kama inavyoonekana katika dondoo ya ukurasa 134 (riwaya ya *Walenisi*) yanatumia mbinu ya tawasifu. Mbinu hii pia ilitumiwa katika riwaya ya Gorky *The Mother* (1906) na *My Universities* (1979). Riwaya hizi mbili zimesheheni maudhui ya uhalisia wa kijamaa. Hadithi hizi ni uzinduzi wa kuweka masaibu ya jamii wazi. Jambo ambalo Mkangi pia amelitumia katika riwaya zake.

Hadithi ya *Mafuta* inaanza kwa mtindo wa kipekee. Labda huu mtindo ndio uliomfanya Kibwana katika *Weekly Review Septemba 20, 1985* kusema kuwa riwaya hii ni ngumu. (Tazama nukuu katika uk. 71). Pia Mkangi mwenyewe katika mahojiano yake na Chacha (2003) ameungama kuwa aliweka mafumbo magumu (Tazama uk. 71) ili kuchamba utawala wa wakati huo na pia wachapishaji wasielewe maana iliyo katika Mafuta kwa sababu wakielewa yaliyomo hawangekichapisha kitabu hiki. Hadithi hii iliandikwa na Jali. Lakini

alipotuhumiwa kuwa mwizi na mzee mwenye mkunazi, Jali alichopoka mikononi mwa walofa waliotaka kumwua na kuacha koti lake. aliacha koti lake. Ndani ya koti hili kulikuwa na makaratasi ambayo tayari yalikuwa na maandishi ya hadithi za *Mafuta.* Mwandishi anasema;

> Macho yalimng'ara kwa furaha na akakitoa kwa hamaki. Kitu chenyewe kilikuwa kimekaa kama kibunda. Alianza kukifungua kwa haraka huku moyo ukimpuma. Kibunda chenyewe kilikuwa kimefungwa kwa ustadi kama vile bumba la tumbako. Kuisha kukifungua, akaona makaratasi mengi ndani ambayo yalikuwa na maandishi. Hakujua kusoma. Kwa hivyo maandishi yakawa ni 'nzora' tu kwake ... hakuacha kuyachakurachakura himahima. Alifika mwisho bila kuona kile alichokuwa akidhani yalikuwa yameficha ... akimwambia zuka makaratasi huliwa? Walipoona upepo umeanza kuyapeperusha, Zuka alimwuliza ikiwa angewaruhusu wayachukue. 'Yaondoeni hapa kwani sitaki hata kuyaona na myachomelee mbali' ... watoto hawa sasa waliingia kazi ya kuyakusanya na kuyapanga vizuri kwa ukurasa mmoja ukifuatiwa na mwingine. Baada ya kufanya hivi waliacha kucheza kamari. Badala yake walienda pahali fulani faragha na kuanza kuyasoma ... *(ukurasa 6-7)*

Mandishi ya Jali ndiyo hizi hadithi zinazosimuliwa katika riwaya ya *Mafuta.* Uandishi wa Mkangi wa riwaya hii ni 'unukuzi' wa hadithi za Jali ambazo ziliwekwa pamoja na Zuka na Kazamoyo. Huu ni mtindo wa kipekee, na wa hali ya juu unaodhihirisha hali ya ujamaa kwa sababu hadithi kama fasihi simulizi ilikuwa mali bia. Riwaya ya *Mafuta* imepitia katika hatua tatu muhimu. Kwanza iliandikwa na Jali. Pili ilisomwa na Zuka na Kazamoyo. Tatu 'iliandikwa' na Mkangi. Ufundi huu wa kuhusisha watu watatu ni ile hali ya kutaka kuwa sifa isionekane ikimwendea 'mwandishi' wa tatu, ambaye ndiye mwandishi kamili wa riwaya ya *Mafuta.* Huu mtindo unaofanya utangulizi ndio

uliotufunulia hadithi ya *Mafuta* kama ilivyoandikwa na Mkangi. Kwa upande mwingine, hadithi za riwaya ya *Walenisi* zinatumia mbinu rejeshi. Kwa mfano mashtaka ya Dzombo yanatokea ndipo tunaelezwa makosa yake. Hadithi ya mapacha pia inachukua mtindo huu wa mbinu rejeshi. Pia hadithi za *Walenisi* zilipatikana baada ya utafiti katika maktaba kuu ya *Walenisi*. Hadithi za Moto, Mabavu, Mapacha, Mchawi na Wachuna ni kama kumbukumbu. Tayari hizi hadithi zilikuwa zimeandikwa na kuwekwa katika maktaba. Hiyo ndiyo sura anayotutolea mwandishi kuhusu hadithi hizi.

Mtindo mwingine ambao Mkangi alitumia unahusu mazungumzo katika maelezo yake. Hadithi za riwaya ya *Mafuta* ni kama tamthilia. Kwa mfano Mazungumzo baina ya Ti na wanamkahawa.

> Basi mbona wimawima hivi? Akauliza, 'Si tukae na tuzungumze kwa taratibu – ama wasemaje? Swali hili akalielekeza kwa mwenye mkahawa. "Mimi kwangu sawa – sijui hao wengine" akasema. Tutakusikiliza kwa kuwa ni wadhalimu na watu wenye mawazo ya kinyumenyume tu ndio huwanyima wengine haki zao za kusikilizwa." Mmoja wao akanena wenzake huku wakikaa.
> "Nashukuru". Ti alisema ... kwa furaha.
> "Sasa ni zamu yetu ya kukununulia wewe Chai", mwingine akamwambia.
> "Nyoteni chai juu yangu" mwenye mkahawa akajitolea.
> "Biashara haigombi yakhe," na mwingine akamwonya.
> Mabishano haya ya kirafiki juu ya nani angemnunulia chai yupi, yalimvutia sana Ti.
> Ni baada ya kukubaliana kuwa wangegawana gharama sawa ndipo ubishi ulikoma. *(ukurasa 57).*

Katika dondoo hii, ingawa ni mandishi ya nadhari lakini yanachukua sura ya mazungumzo. Pili, kusisitiza suala la ujamaa, wanagawana gharama ya chai sawa. Hivi ndivyo wangependa malighafi yanayopatikana katika nchi yagawanywe sawa. Tatu, wanaona ni sawa kila mtu kuwa na uhuru wa kuzungumza. Mambo haya yanapozingatiwa hutia jamii furaha. Kuwa na furaha ni mojawapo wa mihimili ya nadharia ya utafiti huu. Sehemu nyingine zinazochukua mazungumzo ni Mfalme na Mshonaji nguo *(ukurasa 71)*, mazungumzo baina ya wanajamii wanapotamba hadithi (*kurasa 64-65)* miongoni mwa nyingine.

Kivutha Kibwana katika kuchangia makala ya uandishi katika *Weekly Review Septemba 20*, 1985 aliyaita maandishi ya Mkangi '*No see Through Literature*' na anasema;

> Mazungumzo ya Mkangi ni halisi ya kuchangamsha.
> Mazungumzo haya ni magumu kidogo,
> Yanachangamsha na bado yanafaa ... kwa maoni
> Yangu hizi hadithi ni jazanda.

Maoni ya Kibwana yanachukuana na mojawapo wa sababu ya hadithi, kuburudisha na kuchangamsha. Hili ni jambo muhimu la kufanya jamii iwe na furaha. Pili kama ni jazanda zina mafumbo yaliyofumbikwa ndani. Jambo hili linadhihirika katika mahojiano ya Chacha na mwandishi (2003:47) na mtafiti

na mwandishi mwenyewe anaposema;

> Niliandika *Mafuta* mwaka wa 1984 wakati wa serikali ya ugandamizaji. Niliandika kuonyesha udhalimu mkubwa uliokuwepo wakati huo. Nilikuwa katika mapambano ya kuona kuwa nchi yetu inajitoa katika hali iliyokuwepo – (ugandamizaji udhalimu, ukatili na idhilali ya kila aina) ilinibidi niandike *Mafuta* kimafumbofumbo. Kitabu chenyewe ni kigumu.

Matumizi ya mafumbo yanafanya kitabu chenyewe kuwa kigumu. Pili, matumizi ya mafumbo yalifanya wachapishi kuipiga chapa riwaya hii kwa urahisi kwa sababu hawakuelewa yaliyoandikwa ndani. Matumizi ya mafumbo yanachukuana na lengo la utafiti huu – kuchanganua hadithi hizi.

Riwaya ya *Walenisi* pia inatumia mazungumzo kwa mfano mazungumzo baina ya daktari na mamake Metabu, na daktari na mwuguzi. Katika vikao tofauti kuna mazungumzo baina ya Dzombo na wenyeji wake. Lugha ya mazungumzo inapotumiwa huleta uchangamfu na udadisi. Katika mazungumzo haya Dzombo anasema,

> Eti wasema Trimi yangu ni ile ya mbele?
> "Ndio, Mtu-Dzombo"
> "Lakini sijui twende wapi?"
> Trimi yajua, Mtu-Bint Fikirini akamwambia.
> Wacha wee ... ! Mwan'tania? Akawauliza.
> Si utani Mtu-Dzombo. Utajionea mwenyewe punde tu
> uipweyapo, Mtu-Bint Fikirini akazidi kumhakikishia.
> *(ukurasa 51)*

Maelezo haya yanaonyesha mtindo wa mazungumzo katika riwaya zote mbili. Hadithi hizi zina utangulizi tofautitofauti. Senkoro (1982:77) na Wamitila (2003a:28-29) anatoa mianzo tofauti ya hadithi na jinsi hadithi huisha. Mtindo huu pia unadhihirika katika riwaya ya *Mafuta*. Kwa mfano hadithi ya Gweni inaanza hivi;

> Hapo si zamani sana ... kulikuwa na jamii moja ... Na hadithi yangu ikaishia hapo."
> Mbeyu akawaambia wasikilizaji. *(ukurasa 70)*

Huu ni mtindo ambao mwandishi ametumia ili kuhusisha kazi yake na mambo ya kijadi. Katika riwaya ya *Walenisi* hadithi hizi, za mapacha, Moto, Uchawi, Wachuna na Mabavu zilipatikana baada ya Dzombo kufanya utafiti katika Maktaba kuu ya Walenisi. Mtindo huu karibu ushabihiane na mtindo ulioko katika riwaya ya *Mafuta* kwa sababu hadithi hizi zilikuwa 'zimeandikwa' na Jali. Katika *Walenisi* hadithi zinapatikana baada ya utafiti sana katika maktaba kuu ya Walenisi.

Masimulizi mengine katika riwaya hii yanafanywa na mwandishi, kwa mfano (ukurasa 88-89). Hali kadhalika kuna mjadala nafsia katika hadithi hizi kwa mfano Mtue anasema,

> Ndio mwisho wangu leo, wazo moja lilimjia. Na jingine watanitia kitanzi, kunipiga marungu ama kunilipua kwa risasi? Hatua hivi, jingine likamjia. Hata kamwe, nadhani wanaenda kunitesa tu. Mmm u! Nitavumilia kweli mimi ...? Mtue alikuwa anawaza juu ya mateso ambayo angepata.
> *(ukurasa 83)*

Haya ni mazungumzo ya Mtue na nafsia yake. Mtue anatafakari hatima yake kabla hajachukuliwa na watesi wake.

Katika riwaya ya *Walenisi* Dzombo anaota. Matumizi ya ndoto yanatoa mawazo ya mhusika huyu akiwa ndotoni yanapatikana katika ukurasa 116-117. Mwisho Dzombo alishtuliwa na Mtu Bint Fikirini aliposema,

> "Mtu-Dzombo, umekuwa ukiota? Kwa nini?
> Akauliza huko akipokea kifungua kinywa.
> "Kwa sababu nilikusikia ukiuliza 'Utu ni nini?
> Nilipokuwa nimefika hapo mlangoni"
> Ala! Kumbe! ... kulikuwa kumekucha na kumbe
> alikuwa akiota usiku mzima !"
> (ukurasa 137)

Alipokuwa ndotoni mawazo ya Dzombo yaliranda hadi kwao Jehanamu. Matumizi ya ndoto ni njia moja ya kujieleza. Hii ni mbinu ambayo mkangi ametumia katika kututolea maudhui yake. Katika hali ya kawaida, ndoto huwa na mambo ambayo mhusika amekuwa akiyawaza wakati fulani.

Uandishi wa Mkangi una athari aliyorithi kutoka kwa marehemu Sheikh Shabaan Robert. Shabaan Robert aliandika riwaya ya *Kusadikika* (1951) wakati wa ukoloni. Kwa hivyo hangeweza kuandika mambo maovu waziwazi yaliyokuwa yakifanywa na wakoloni. Haki ya sheria ilikuwa imedunishwa na baadhi ya wajumbe walitiwa kizuizini bila kufanyiwa mashtaka. Mashtaka pia katika riwaya ya *Mafuta* hayakuendeshwa kwa njia nzuri, yaliendeshwa na

kigaro cha wadhalimu wachache. Wajumbe hao waliporudi kutoka safarani walidhulumiwa na kutupwa mbaroni. Kwa upande wake Mkangi ametumia pia taswira ya safari katika *Mafuta* na *Walenisi*. Senkoro (1982:57) anasema kuwa: "taswira ya safari ni mojawapo wa mbinu kuu za fani katika fasihi ya ulimwengu."

Katika riwaya ya Mohamed Suleiman Mohamed *Nyota ya Rehema* (1976), mwandishi anatuonyesha Rehema akikimbia kutoka kwao – kwa Fuad, mwendo wa maili kumi kwa miguu hadi akajikuta katika mikono ya Sulubu. Senkoro (1982:58) anasema,

> Taswira ya safari inakamilika katika *Nyota ya Rehema* kwa ndoa baina ya Rehema na Sulubu; ndoa ambayo yenyewe ni ishara ya muungano wa wanyonge. Muungano huu ndio ulioleta ushindi wa hao wanyonge baada ya safari ndefu, mwishoni mwa riwaya.

Hali kadhalika riwaya ya Shabaan Robert *Kusadikika* (1951) *na Adili na Nduguze* (1952) zimejengwa katika taswira ya safari. Hivi ndivyo mambo yalivyo katika riwaya za *Mafuta* na *Walenisi*. Ti anafanya safari ndefu akitafuta kwa Msati, kiongozi wa kundi la siri ili amjulishe yaliyompata Mtue. Safari yake Ti inaleta muungano wa wanyonge wanaonyanyaswa na hatima yake ni ukombozi. Taswira ya namna hii inaonekana ikiwa imejengwa juu ya misingi ya fasihi simulizi hasa ngano. Wamitila (2003:131) anasema,

> Safari inachukua nafasi hii kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Safari humbadilisha mtu, jinsi alivyokuwa aanzapo safari sivyo safari hiyo humalizika. Umuhimu wa safari unaeleweka vizuri hata tunapochunguza misingi ya imani nyingi za kidini na tamaduni zetu, safari inachukua nafasi kubwa sana ... safari inapotumiwa huashiria mabadiliko fulani.

Mwanzoni mwa sura hii tumeonyesha baadhi ya riwaya zilizotumia taswira ya safari. Hali kadhalika katika *Walenisi* kuna taswira ya safari ya Dzombo. Safari zake zilimpeleka mahali kwingi katika nchi ya Walenisi. Kutokana na ziara hizi za kumfahamisha na kumwonyesha yaliyokuwa yakitendeka katika nchi ya Walenisi, Dzombo alijifunza mengi aliweza kufanya utafiti katika maktaba kuu na kugundua mambo mengi. Taswira ya safari imekuwa msingi wa mabadiliko. Mwisho tunaona ikiishia kwa ndoa baina ya Dzombo na Mtu Binti-Fikirini. Pia Dzombo anabadilisha jina lake kuwa Mtu-Bedzombo ambaye anaamua kurudi kwao kuwazindua aliowaacha huko. Hapa alikuwa amejihami vilivyo ili kwenda kutatua matatizo ya huko. Waliandamana na mkewe Mtu Binti-Fikirini akiwa mjamzito.

Pia usimulizi wa *Mafuta* unachukua nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu, kwa mfano Hadithi ya 'Mama Fofi' na 'Matope'. Tazama hadithi ya 'Matope' iliyo

katika nafsi ya tatu ambako mwandishi anasema;

> Kuingia kwake kwa ghafula, kulikomesha kuteswa, kupigwa na kudharauliwa kwa Matope. Umati wote ulisinyaa na kumatamata kule kumwona ... Kimoyomoyo alimshukuru mfadhili wake. Ni weli alikuwa ameshasikia sifa za mtu kama huyu, lakini leo hii, ilikuwa ni mwanzo kumpasha moto. Kwa kufuatia tabia za wasulubishi wake, kutisha kwa jibaba hili hakukuweza kufichika. Ikiwa walionyesha ishara yoyote ya kumheshimu, basi ilikuwa ni kwa shauri ya uwoga bali si kwa kuwa eti walikuwa wakimpenda sana. *(ukurasa 43)*

Katika riwaya ya *Walenisi* Mkangi ametumia pia usimulizi katika nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu kuhusu jambo hili la usimulizi katika riwaya hii Wamitila (2003:92) anasema,

> Riwaya hii inapoanza inasimuliwa kwa nafsi ya tatu. Hata hivyo, kuna sehemu inayosimuliwa katika nafsi ya kwanza. Hii ni sehemu inayohusu matokeo ya utafiti wa Dzombo nchini Walenisi. Dzombo anapoandika matokeo ya utafiti wake wa historia ya Walenisi anaanza usimulizi wake kwa nafsi ya kwanza (hii hutambulishwa na matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza 'ni' na 'mimi').

Usimulizi wa Mkangi katika riwaya ya *Walenisi* umeingiliana baina ya usimulizi wa nafsi ya kwanza na usimulizi wa nafsi ya tatu. Sehemu hizi mbili za dondoo zinaonyesha masimulizi katika nafsi tofauti.

Nafsi ya kwanza:

> Mimi Dzombo wa Bedzombo, niliyehukumiwa kifo kwetu Jehanamu kwa kutaka kumalizika ubaradhuli na upopo huko, nataka ijulikane kuwa bado sijafa. Nilinusurika na nikajikuta katika Ulimwengu mwingine ambao katika upeo wangu wa kuelewa nilikudhania ni Mbinguni kwa Mwenyezi Mungu. Ni baadaye nilipokuja kujua niko wapi na kwamba sikuwa nikitoka Duniani. *(ukurasa 153)*

Matumizi ya 'ni' yanaonyesha nafsi ya kwanza. Masimulizi ya matokeo ya utafiti yamejikita katika nafsi ya tatu Mwandishi anasema,

> Dzombo aligusa mengi ndani ya daftari lake. Yale yote aliyoyaona kuhusu elimu isiyo na usawa, sheria zisizo na haki, uchumi usio na mapenzi--- kisha akaendelea kuandika. *(ukurasa 187)*

Huu ni usimulizi katika nafsi ya tatu.

Riwaya zote zimetumia mbinu ya fasihi simulizi hasa hadithi kutoa maudhui. Kuusu jambo hili la matumizi ya fasihi simulizi katika riwaya ya *Walenisi,* Wamitila (2003: 129) anasema;

> Sifa moja inayopatikana katika riwaya ya *Walenisi* ni matumizi ya mbinu za usimulizi zinazohusishwa na fasihi simulizi. Tunapoisoma riwaya hii, tunajiwa na hisia za kusikiliza ngoma au simulizi ya fasihi simulizi. Historia ya jamii ya Wachuna imewasilishwa kwetu kwa mtindo wa fasihi simulizi... Pana matumizi ya hadithi zenye muundo wa ngano kama kisa cha Moto, kisa cha Mchawi, na kisa cha Mapacha.

Hizi ni hadithi zinazoeleza asili au chanzo cha kitu fulani. Kwa mfano chanzo cha Moto, ni kisasili – hadithi inayoeleza historia fulani. Kwa mfano historia ya Wachuna na pia hadithi ya Mapacha ni ngano au hadithi za fasihi simulizi. Sifa hii pia inapatikana katika riwaya ya *Mafuta*. Hadithi ya 'Mfalme aliyeenda uchi' ni kisasili. Hadithi ya 'Nyani na Chui' ni hurafa; miongoni mwa hadithi zingine. Hadithi hizi zinaashiria matukio katika jamii kupitia kwa hadithi za kale. Okpewho (1983:155) katika kongamano la wanahistoria la Kenya lililofanyika

mjini Nairobi mwaka 1968, akimnukuu Ngugi wa Thiong'o anasema "Nataka kuzungumza juu ya mambo ya kale kama mbinu ya kuzungumza juu ya mambo ya siku hizi". Maneno ya Okpewho ndiyo yanayochukua hadithi za *Mafuta* na *Walenisi*. Hadithi hizi zinadhamiria kutoa maudhui ya kileo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Katika riwaya ya *Walenisi* mwandishi anatumia kejeli. Mtindo huu unajitokeza wakati Dzombo aliposema;

> Ala, mbona mu wanyonge hivi? Akawashtukia?
> Baridi imetumaliza wakamweleza.
> Kwani hamkubahatika na mablanketi? Akawauliza.
> Hatungekuwa hivi. Wakamwambia huku wakitweta.
> Lo! Poleni sana. Kweli hamna bahati. Mimi nami karibu inimalize kama haingekuwa kwa bahati nzuri, akajieleza.
> "Wewe U mtu wa bahati" wakadokeza.. 'Tena sana' akakubaliana nao. *(ukurasa 60)*

Hii ni kejeli kwa sababu alipopewa maji na punde mkate, alisema kwamba alikuwa na bahati, na sasa baada ya kupata blanketi tatu alisema vivyo hivyo. Lakini wao walipopewa miavuli walimpatia mmoja. Hapa mwandishi alitaka kuonyesha jinsi Dzombo bado alikuwa na ubinafsi. Mbinu ya namna hii ya kejeli pia imetumika katika riwaya ya *Mafuta* hasa Mtue anapotaka kujua ukweli wa Mafuta na jibu alilopewa.

Mbinu nyingine ambayo mwandishi anatumia ni kumbukumbu. Hii inajitokeza katika riwaya ya *Walenisi* hasa pale ambapo Dzombo alifikiria hadithi ya 'Maskini Jeuri' na 'Mzee Matingasi'. Matingasi na Maskini Jeuri walikuwa rafikize

walioshirikiana na Dzombo katika 'kuwasha taa'. Matumizi haya yanajitokeza wakati Dzombo walipokuwa wametoka safarini. Kumbukumbu ni mojawapo wa kipera cha hadithi za historia. (Tazama Kiambatanisho A).

Walikuwa wameandaliwa vinywaji vya kila aina. Dzombo hakujua achukue kinywaji kipi, ndipo mwandishi anasema;

> Hakutaka kubahatisha kwa kufuatisha rangi ama maumbo yaliyokuwemo. Hakufanya hivyo kwa kukumbuka jinsi siku moja alivyochezewa shere na rafiki yake aliyejiita 'Maskini Jeuri'. *(ukurasa 69)*

Jambo lingine ni kuwa usimulizi wa riwaya ya *Mafuta* yaonekana kama kwamba ulichukua muda mfupi hasa wanaposema (Zuka na Kazamoyo) 'wacha turejee huko kwa mkunazi ili kujua yaliyompata Jasho'. Wanarejea kwa mwenye mkunazi na kumsaili juu ya Jasho.

Mwisho Mkangi ametumia ndoto kuonyesha jinsi fikira zake zilivyokuwa kwao jehenamu alikotoka. Hasa anapoota mambo ya nyumbani kwao kuhusu watoto wake na mkewe. Kwa kutoa Muhtasari, Mkangi ametumia usanii wa hali ya juu kututolea mawazo yake na kusawiri maisha ya jamii kwa kutumia mtindo tofauti ya usimulizi.

# SURA YA 5

## 5.0 HITIMISHO

## 5.1 UTANGULIZI

Tumechanganua kwa makini hadithi zilizo katika riwaya mbili za Katama Mkangi, *Mafuta* na *Walenisi.* Mkangi ametumia hadithi tofauti katika riwaya hizi mbili ili kutoa maudhui yake. Kwa kufanya hivyo ametumia mitindo tofauti ili kushika hisia za wasomaji wake. Jambo ambalo linafanya hisia za wasomaji wake kuwa naye pamoja au wasiweze kuchoka.

Tumeonyesha kuwa hadithi hizi zimefungamana na vigezo vya nadharia yetu ya uhalisia wa kijamaa kwa kutongoa na kueleza muumano wa hadithi, maudhui na uhalisia katika jamii ya mwandishi. Tumeweza kuonyesha kuwa hadithi hizi ni mafumbo ambayo yamebeba maudhui mazito kama asemavyo Senkoro (1982:116);

> ...visa vinavyosimuliwa vina uchangamfu wa juu ambavyo chini yake kunatokota maana nzito zenye kukabili masuala mbalimbali ya kisiasa, kitamaduni na kiuchumi

Kwa mujibu huu maudhui ambayo yamejikita katika hadithi hizi ni mafumbo ambayo yanahitaji ufumbuzi. Utafiti huu umefumbua mafumbo yaliyo katika hadithi hizi.

Pia tumeonyesha kuwa baada ya udhalimu huu uliotendewa wanajamii, Mkangi anatoa kauli kuwa njia ya pekee ya kuboresha mambo ni kupitia kwa mapinduzi.

Haya yatakuwa mapinduzi ya mfumo wa kisiasa, kiuchumi na sera ya jamii kuhusu masuala ya kijamii. Mapinduzi haya yataleta usawa katika ugawanyaji wa rasilimali za nchi, haki katika mahakama, usawa katika huduma za afya, miongoni mwa mengine. Hadithi ya Mabavu, Moto na Mchawi zinaonyesha chanzo cha ukabaila katika jamii. Hadithi ya Mwenye mkunazi inaonyesha ubepari. Kupitia kwa hadithi hizi tumeonyesha kuwa Katama Mkangi alitaka jamii ambayo wananchi wake na watawala wanawajibika.

Utafiti huu umeonyesha watu walioathiri maisha yake hasa kuelekea kwa siasa za ujamaa. Watu hawa ni kama Mwalimu Julius Nyerere Karl Marx, na Frantz Fanon miongoni mwa wengine. Mkangi aliwahusudu sana waandishi kama Shaaban Robert. Uandishi wa Shabaan Robert umeathiri mtindo wake hasa kutumia hadithi zilizojikita katika safari. Kupitia kwa hadithi hizi Katama Mkangi ametupitisha katika jamii ambayo angelitaka. Hili ameeleza kwa njia ya ulinganifu kwa mfano kupitia kwa *hadithi ya Mapacha* na *Utawala wa Wachuna na Walenisi.* Mkangi pia aliathiriwa na siasa za mahali ambako alisomea hasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam baina ya mwaka wa 1967-1971.

Safari anayotutolea katika riwaya hizi ni nyenzo ya kuleta mabadiliko. Wahusika wote wakuu wanashirikishwa katika safari. Lakini mwisho anashikilia mawazo yaliyo tofauti na masimulizi ya kawaida ambapo nguli hujitokeza, ambalo huwa si kundi la watu. Kwa mfano katika riwaya ya *Mafuta,* hatima yake ni kundi la watu

na katika riwaya ya *Walenisi* Dzombo na mkewe mjamzito wanajitokeza. Njia hii inashikirisha wengine katika mapinduzi. Kwa kufanya hivi alionyesha mawazo yake ya kijamaa ambayo huhitaji ushirikiano wa wote. Ngara (1985:71) anasema mtazamo wa namna hii unaafikiana na dhana ya ujamaa wa Mwafrika na kuonyesha siasa ya ujamaa ambayo hulenga juu ya watu (wahusika) na sio mtu (mhusika) binafsi. Hali kadhalika kama tulivyoeleza katika sura ya pili hadithi ni mali bia. Katama Mkangi amebuni hadithi hizi ili kutoa uhalisia wa mambo katika jamii kwa kueleza leo akitumia jadi.

Pia tumeona jinsi alivyoonyesha nafasi za wahusika katika hadithi hizi, wakieleza au kuuliza swali au wakitaka kujua zaidi juu ya hadithi au kuwa na mshawasha wa kutaka kujua jambo hili au lile. Mambo kama haya yanatoka katika tendohisia la hadhira. Huu ndio uhalisia wa utambaji wa hadithi kama anavyosema Okpewho (1983:162), kwa muktadha huu wa tendohisia, hadithi za *Mafuta* zinaonekana kama maigizo. Mbinu hii inatia uhai katika usimulizi kwa hadhira pamoja na mtambaji.

Matumizi ya matukio ya kihistoria katika hadithi hizi yamesaidia kutoa maudhui. Historia ya jamii hujengeka kutokana na matendo ya jamii hiyo ambayo huwa yametendeka kutegemea wakati, mahali na mazingira. Historia ni kipengele muhimu cha nadharia ya utafiti kwa sababu matukio huhifadhiwa katika historia. Kwa mfano h*adithi ya Wachuna,* au *hadithi ya Mama Fofi*, au M*oto* na *Mchawi.*

Kwa kutumia utafiti huu tumeweza kuonyesha jinsi hadithi hizi zinavyohusishwa na matukio ya kihistoria na uhalisia wa kijamaa katika nchi za Kiafrika. Matukio ya kihistoria yameweza kuonyesha kuibuka kwa maudhui ya ubwanyenye, ubepari, istiimari za Waingereza na Wamerika, na Ukoloni mamboleo uliolikumba bara la Afrika. Kwa njia hii, uchanganuzi huu umeonyesha jinsi hadithi za kijadi zilivyo na utajiri mwingi wa kutoa maudhui ya kisasa, kukuza lugha na kufunza maadili.

Hadithi zinazojitokeza katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi* ni hadithi ambazo Katama Mkangi aliweza kuzitunga ili kutoa maudhui tofauti kama alivyofanya katika riwaya hizi. Katika mahojiano kati yangu naye ya tarehe 6-08-03 katika ofisi yake alikokuwa anafanya kazi huko USIU alinitolea kijihadithi hiki:

> Kulikuwepo na jitu lililokuwa likiwala watu. Wenyeji walienda kwa mganga ambaye aliwaambia jinsi ya kufanya kwa kuliwinda hili jitu na kuliua. Baada ya kuuwawa kwa jitu hili wangelilichoma baadaye wangelichukua fimbo ya aina fulani na kupiga kwenye jivu hilo na kuita jina la mtu aliyeliwa na jitu hilo. Mtu huyu angelifufuka na kujiunga na wengine ambao walikuwa wakiimba nyimbo za ushindi.

Hadithi hii ilibuniwa na kutoa maudhui ya jamii mpya. Hiki kisakale kinatoa maudhui ya kisasa. Kwa mfano maarifa yatafutwe jinsi ya kupambana na udhalimu na namna ya kuleta mapinduzi. Wazo hili hapa linatuonyesha ubunifu wa Katama Mkangi katika kutumia hadithi kutolea maudhui tofauti yaliyojikita katika nadharia ya uhalisia wa kijamaa.

Uchunguzi wa hadithi hizi umeonyesha kuwa licha ya hadithi hizi kuwa visakale, kumbukumbu, hurafa na kadhalika hadithi za kubuni zina maudhui mazito. Watambaji wa hadithi wamepata njia mpya ya kutoa maudhui yao kwa kutumia hadithi za kale kama asemavyo Okpewho (1983:155) alipomnukuu Ngugi wa Thiong'o kama tulivyoona hapo awali.

Katama Mkangi ametumia mbinu hii ya kijadi kutoa maudhui yake na hali kadhalika kuhifadhi ukale wa Mwafrika. Sambamba na wazo hili utafiti huu umejaribu kuonyesha umuhimu wa masimulizi ya hadithi katika jamii za Kiafrika kama njia ya kuficha ukweli wa maudhui na kufundisha jamii.

### 5.1.2 MAATHIRIANO YA FASIHI ANDISHI NA FASIHI SIMULIZI

Fasihi simulizi na fasihi andishi ni kazi za sanaa zinazotumia lugha kutoa maudhui yake. Kazi hizi zimeathiriana kwa njia tofauti ndiposa utafiti huu ukaonelea ni jambo lenye hadhi kutazama mwathiriano huu wa tanzu hizi mbili za fasihi.

Hapo zamani za kale kabla kwa kuwepo na maandishi, fasihi simulizi ndiyo iliyokuwa njia ya pekee iliyotumiwa kupitisha maadili, historia ya jamii, kuadibu, kuonya na kuelimisha. Maadili haya yalikuwa yakipitishwa kwa njia ya mdomo. Maelezo haya yalikuwa muhimu kwa sababu yaliweza kupitishwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Hadithi, semi, methali, nahau na vitendawili ni fasihi

simulizi iliyokuwa ikitambwa na kupitishwa kwa njia ya mdomo. Utambaji huu ulitumia mbinu mbalimbali za sauti kama anavyosema Matteru (2003:26);

> ... hutumia pia mbinu mbalimbali za sauti ya binadamu zisizokuwa maneno wala mazungumzo kama vile miguno, toni, vituo katika sauti, miliolio, kiimbo na kadhalika.

Mbinu hizi zilitumika katika jamii hizi za jadi. Matumizi ya mbinu hizi tofauti yalifanya masimulizi ya hadithi semi, methali, nahau na vitendawili yasiwachoshe wasikilizaji na kila mara kuonyesha kama ni jambo jipya linaposimuliwa na watambaji tofauti kwa nyakati tofauti. Mara nyingi mambo haya yalifanywa jioni hasa baada ya kazi ya siku kutwa. Ilikuwa njia ya kujiburudisha. Hali kadhalika wengine walifunzwa mambo ya jandoni kwa njia ya namna hii. Fasihi hii ilichukua maelezo ya nathari ambamo mlijikita hadithi, kwa mfano ngano, hadithi za kihistoria (Misendu) na visasili (tanye), hurafa na hekaya. Utafiti huu umeweza kutumia aina hii ya utanzu. Tanzu zingine ni ushairi na tanzu zinazochukua maumbo ya kisemi. Tanzu hizi zote huingiliana. Kwa mfano semi nyingi huwa na mapigo ya kishairi yenye urari na mpangilio usio wa kawaida wa maneno kwa mujibu wa Matteru (2003:28). Utangulizi wa hadithi huwa na ladha ya kishairi kwa mfano:

> Msimulizi : Hadithi, hadithi
> Mskilizaji : hadithi njoo

Mambo haya ya jadi sasa yamewekwa katika uandishi. Hii ni njia mojawapo ya kuhifadhi hii tunu ya jamii. Lakini kwa kufanya hivi, fasihi simulizi inakuwa mali ya mtu binafsi yenye hati miliki. Haiwi tena mali bia. Baadhi ya wasanii kama



KENYA ... LIBRARY

Katama Mkangi na Ebrahim Hussein wametumia hadithi hizi za kijadi kusawiri maisha katika jamii zao. Hadithi hizi zimekuwa maandishi, sio tena hadithi za kutambwa.

Matteru (2003:31) ameonyesha kuwa taaluma kama elimu jamii, elimu utamaduni na hata historia zimenufaika kutokana na fasihi simulizi. Rekodi na data za historia zimewekwa sawa na kujengwa kwa kutumia fasihi simulizi. Jambo hili pia limesisitizwa na Jan Vansina (1995). Haya ni maingiliano ya sanaa hii ya fasihi simulizi na taaluma hizi zilizowekwa katika maandishi. Fasihi simulizi inachangia taaluma hizi.

Athari nyingine inapatikana katika isimu na taaluma za lugha. Kwa kutumia miundo mbalimbali inayojitokeza katika fasihi simulizi wanaisimu wanaweza kuelewa lugha na mabadiliko yake hasa katika misemo, vitendawili, nahau na methali miongoni mwa zingine kwa sababu lugha hukua na hubadilika na wakati. Pia kwa kutumia lugha wanaweza kuelewa mshikamano wa lugha na jamii inayotumia lugha hiyo.

Fasihi simulizi inatakikana kuchunguzwa, kuchambuliwa na kuainishwa ili vitabu viandikwe. Kwa kufanya hivyo data ya fasihi simulizi huwa imebadilika. Njia hii itahifadhi fasihi simulizi. Maandishi yakitumiwa sana yatafisha fasihi simulizi na hata kupunguza hadhi yake katika jamii. Fasihi andishi imenufaika kifani kutoka

kwa fasihi simulizi. Hadithi za kijadi kama kazi za Shabaan Robert (1951) na (1946), zina mtiririko kama ngano za kiasili zinazotumia "paukwa... wakaishi raha mstarehe." Katika hizo hadithi maudhui yamefumbwa ndani. Matteru (2003:35) anasema;

> amezifanya (Shaaban Robert) hadithi zake ziachane na wakati wa kuzifanya ni za kale wakati zinapojadili mambo ya wakati uliopo. Hii ni hali iliyomo katika fasihi simulizi.

Wengine waliotumia mtindo huu ni Ebrahim Hussein na Katama Mkangi kama tulivyoeleza hapo awali, halafu Mathias Mnyampala katika *Ngonjera za Ukuta* ambako anatumia mtindo wa 'kufunga nyama'. Mtindo huu huwa wa kufumba na kufumbua fumbo.

Aidha fasihi simulizi imesaidia kuimarisha na kutajirisha uandishi wa Kiswahili kwa kufanya utafiti katika fasihi ambazo zimelala (za Jadi) kwa kuzitumia katika uasili wake wa kutia ladha katika kazi za fasihi andishi. Jambo hili huipa fasihi andishi ya Kiswahili upekee wake. Matumizi ya tamathali za lugha, semi, methali na vitendawili hurutubisha fasihi andishi ya Kiswahili. Kwa upande mwingine fasihi andishi imetumika kuhifadhi fasihi simulizi. Hata hivyo Matteru (2003:33) akimnukuu Obiechina anasema:

> Hakuna watu, wowote, ambao wanajulikana kuwa wamepoteza kabisa hadithi ya usimulizi katika utamaduni wao. Hii ni kweli hata katika jamii ambazo zimeingiliwa sana na maandishi.

Kwa mujibu huu maandishi hayawezi kusema kila kitu na kwenda sambamba na mageuko ya wakati kwa kiasi hicho, na hata watu wakihamia mjini bado kutakuwa na mahitaji ya kutumia 'mdomo' katika mawasiliano ya ana kwa ana. Pili suala la fasihi simulizi kupisha fasihi andishi halipo. Fasihi hizi zitaingiliana na kuwepo pamoja.

Wazo lingine ni kuwa fasihi simulizi inapowekwa katika maandishi huwa inapoteza ladha au 'hisia' ya aina fulani kwa kutoshirikisha wasikilizaji na mtambaji. Okpewho (1983:162) anasema;

> Yeyote ambaye ameona utambaji wa hadithi katika vijiji vya kienyeji, ameshashuhudia jinsi wasikilizaji au msikilizaji anavyoingiliana kwa kumkatiza mtambaji na maelezo, kwa kuuliza swali au kuongeza jambo, kama jambo la busara au tukio la tendohisia. Au wengine (watambaji) huweza kuteua mmoja kutoka kwa hadhira ambaye atajibu maswali yake katika usimulizi.

Wazo hili pia limezumgumziwa na Ruth Finnegan (1976:67-8) kuhusu jamii ya Limba. Mkangi ametumia mbinu hii katika riwaya yake ya *Mafuta*. Okpewho (1983:156) anasema kuwa sifa hizi za tendohisia huwa zimetolewa katika fasihi simulizi inapowekwa katika uandishi. Mara nyingi hadhira hubadilika. Huwa tunatumia macho badala ya masikio. Utapata kuwa jambo ambalo lingefurahisha masikio linapowekwa katika maandishi huchosha macho. Kwa mfano muziki utateka masikio lakini unapowekwa katika maandishi huchosha macho. Ukariri wa mashairi huwa na ladha kwa masikio lakini huchosha macho kwa kusoma.

Hali kadhalika hadithi ikitambwa huteka hadhira kuliko kuisoma. Matumizi ya ishara za mwili na tendohisia kama kicheko hupotea wakati fasihi simulizi inapowekwa katika maandishi.

Hadithi zingine zinaweza kuelezwa mara nyingi katika jamii na mabadiliko tofauti. Hadhira haiwezi kusinywa au kuchoshwa na maelezo hayo kwa sababu kuna mambo mageni yanayoingizwa ndani ili kutia ladha kazi hii. Au mtindo wa usimulizi huweza kugeuzwa. Lakini maandishi hayatabadilika, yakishaandikwa huwa vivyo hivyo. Hata hivyo mabadiliko kutoka kwa fasihi simulizi hadi fasihi andishi yameonyesha mabadiliko katika sanaa hii inayotumia lugha.

Uandishi wakati mwingine huweza kutumia istilahi au semi zingine ambazo hazifungamani na jamii za Kiafrika au jamii husika. Kwa mfano Taban Lo Liyong (1969) anapoeleza hadithi ya '*The Old man of Usumbura and His Misery*' Hadithi hii ni ya kusisimua lakini inapoandikwa inapoteza ladha, na lugha ya mtambaji inatoka katika masimulizi ya kiasili kwa mfano matumizi ya maneno ya Kiingereza. Maneno kama "Blacksheep," "in the snow – whitehome." Theluji katika Afrika ni nadra kupatikana. Pili kondoo mweusi (black sheep) hazitoi maana iliyokusudiwa. Kwa mujibu wa Okpewho (1983) anaonyesha kuwa uandishi hudunisha sifa ya usimulizi.

Pia katika usimulizi mtambaji huhitaji kutumia maigizo na ishara mbalimbali za mwili kama mikono na uso. Matumizi ya ishara hizi hayako katika uandishi. Ishara hizi hutomelea ujumbe uliokusudiwa. Kutokuwa na ishara hizi hufanya uandishi kukosa ule uhondo wa asili ambao hadhira hupata katika fasihi simulizi.

Kwa kuhitimisha, fasihi simulizi na fasihi andishi haziwezi kutalakiana. Mara nyingi zina mwingiliano wa hapa na pale.

### 5.1.3 MAPENDEKEZO

Baada ya kutazama mambo tofauti katika riwaya hizi mbili, tungependa kupendekeza yafuatayo; kwanza kabisa riwaya hizi zote zinakaribiana kwa njia ya maudhui na mtindo. Tungependekeza utafiti ufanywe wa kina kuhusu mtindo wa Katama Mkangi katika riwaya zake *Mafuta* na *Walenisi*. Pili utafiti zaidi unaweza kufanywa ili kutazama nafasi ya mwanamke kwa sababu mwandishi huyu (Mkangi) amelipatia suala hili nafasi muhimu katika riwaya hizi mbili. Utafiti zaidi unaweza kulishughulikia suala hili kwa kina ama kwa kutoa mlinganisho au kushughulikia suala hili moja kwa moja katika riwaya zote mbili. Mtafiti anaweza kushughulikia nafasi ya mwanamke katika hali ya utaifa kwa kutetea mapinduzi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Tatu watafiti wengine wanaotaka kutafiti wanaweza kuchunguza matumizi ya lugha na fani katika kutoa msukumo wa hadithi au maudhui. Kama ilivyo

kawaida lugha ni chombo muhimu kwa mwanadamu. Lugha ndiyo nyenzo ya kutolea mawazo yetu. Utafiti wa kina kuhusu lugha iliyotumika katika riwaya hizi mbili utasaidia kutoa picha nzuri zaidi kuhusu maudhui ya mwandishi.

Sehemu nyingine ambayo inaweza kushughulikiwa na utafiti wa baadaye inaweza kuwa maathiriano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi kwa muktadha wa riwaya hizi mbili kwa kutazama kwa nini kumetokea ukiukaji wa mambo kutoka fasihi simulizi hadi fasihi andishi. Jawabu rahisi likiwa, jamii inabadilika. Je, hata kama tuna hayo mabadiliko, tutupe 'chungu cha zamani?' Utafiti wa kina katika suala hili utasaidia kutoa mwangaza zaidi juu ya maathiriano haya.

Pia suala la ukombozi dhidi ya istiimari katika riwaya zote mbili. Suala hili linaweza kufungamanishwa na matukio ya Kihistoria yanayojitokeza katika riwaya ya *Mafuta* na riwaya ya *Walenisi.* Utafiti wa namna hii unaweza kulenga nafasi ya Historia katika kukaza maudhui ya ukombozi.

Matumizi ya mbinu ya ubunilizi wa kisayansi pia yanaweza kufanyiwa utafiti kwa muktadha wa riwaya ya *Walenisi.* Dzombo alitakikana kufa kupitia kwa njia ya chombo cha sayari. Je, huu ubunilizi wa kisayansi una sifa gani, kwa nini mwandishi aliitumia? Haya ni baadhi ya masuala yanayoweza kusaidia utafiti wa namna hii.


Licha ya hayo utafiti huu umeangalia hadithi katika hadithi kama chombo cha kutolea maudhui kwa kutumia nadharia ya uhalisia wa kijamaa Utafiti huu umeonyesha mwumano uliopo baina ya matukio ya hadithi hizo na uhalisia au ukweli wa mambo yanavyojitokeza. Jambo linalofanya kazi hii ya sanaa kuwa kioo cha jamii ya mwandishi. Kwa misingi ya utafiti huu hadithi za kijadi zimetumika kama nyenzo ya kutolea maudhui.

Kwa kuhitimisha, bila shaka Katama Mkangi ametuachia mambo matatu muhimu, kwanza kabisa ni matumizi ya hadithi za kale kutoa maudhui. Hapa ni matumizi ya ukale kuelezea mambo ya kisasa. Pili uandishi wake ni wa kipekee hasa mtindo aliotumia kutanguliza na kuendeleza kazi zake. Kwa kufanya hivyo Mkangi ametuachia urithi usio kifani kupitia kwa mtindo wake wa uandishi. Jambo la tatu ameonyesha jinsi ya kuhifadhi ukale wa Mwafrika kupitia kwa hadithi zenye maudhui mazito alizotoa. Ameonyesha umuhimu wa fasihi simulizi na jinsi fasihi simulizi ilivyoathiriwa.

## KIAMBATANISHO (A)

**VIPERA VYA HADITHI**

Utanzu wa Fasihi simulizi umesheheni vipengele kadha. Kwa mfano Hadithi, maigizo, ushairi na semi. Mchoro huu unaonyesha vipengele vya Hadithi ambavyo huchukua hadithi za kubuni na Hadithi za kihistoria. Hadithi hizi zina vipengele vidogovidogo vilivyojikita katika kila kipengele kikuu (Tazama mchoro).




Kwa mujibu wa Wamitila (2003:26b) hadithi za kubuni zina ngano, mbazi, istiara, soga na mchapo. Ngano nazo zina hekaya, hurafa na ngano za mazimwi. Licha ya haya Hadithi za kubuni zina vipera vilivyoonyeshwa na Hadithi za kihistoria pia zina vipera vyake.

**KIAMBATANISHO (B)**

**MAELEZO KUHUSU MWANDISHI WA RIWAYA ZA *MAFUTA* NA *WALENISI* MAHOJIANO YA MTAFITI NA MWANDISHI (GEORGE KATAMA MKANGI) TAREHE 6-08-03 KATIKA OFISI YAKE – USIU**

**Kuzaliwa:**

George Katama Mkangi alizaliwa miaka sitini iliyopita huko Ribe Mkoa wa Pwani.

**Kisomo**

Alianza shule katika shule moja ya Kiarabu ambapo alifanya mtihani wa C.E.E. (common Entrance Examination). Baada ya kuupita mtihani huu alijiunga na Mariakani Primary School katika darasa la tano na sita. Huu ulikuwa mwaka wa 1956 na 1957. Baadaye aliendà St. Michael Giriama, akasoma huko mwaka wa 1958 na 1959. Alifanya Mtihani wa KAPE. Hapa alifaulu na kujiunga na St. Georges Giriama mwaka wa 1960 – 1963.

Alifanya mtihani wa kidato cha nne uliojulikana kwa jina Cambridge Examination. Alipita katika daraja la kwanza (1st Division). Akajiunga na Strathmore School mwaka wa 1964 katika kidato cha tanona kufanya mtihani wa kidato cha sita mwaka wa 1965. Baada ya mtihani huu uliojulikana kama Cambridge Higher Examination alifaulu na kujiunga na Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki huko Dar-es-Salaam (sasa University of Dar-es-Salaam). Huko alisoma Historia, Jiografia, Isimu, Elimu Jamii, Elimu na Kiswahili. Kiswahili hakikuwa miongoni mwa

masomo yake muhimu. Alihitimu na shahada ya B.A pamoja na Stashahada ya Ualimu.

Katika mwaka wa 1972-73 alijiunga na Chuo Kikuu cha Sussex huko Uingereza ambako alipata shahada ya Uzamili katika somo la Elimu mipango na Maendeleo (Education development and Development). Katika mwaka wa 1978 alipata shahada ya Udaktari katika Elimu Jamii.

**Kazi**

Baada ya mtihani wa kidato cha sita, Mkangi alifanya kazi na East African Harbours mjini Mombasa, kabla ya kijiunga na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Huu ulikuwa mwaka wa 1967. Baada ya kumaliza masomo ya chuo kikuu alifunza katika shule ya upili ya Ribe. Masomo aliyofunza ni Jiegrafia, Historia na Kiswahili. Huu ulikuwa mwaka wa 1971. Mwaka wa 1972 alipandishwa cheo na kuwa mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Dr. Aggrey. Hapa alikaa kwa muda wa miezi sita na akapata udhamini kwenda kusomea shahada ya Uzamili (masters degree) huko Uingereza. Alipotoka shule ya Upili ya Dr. Aggrey, Ali Mwakwere akawa sasa ndiye Mwalimu Mkuu. Mwakwere akawa ni Waziri wa Leba nchini baada ya Uchaguzi Mkuu 2002.

**Uandishi Wake**

Uandishi wake ulianza akiwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Akiwa huko aliandika *Ukiwa* (1975). Hapo alitiwa hima kuandika na mwalimu wake Profesa George Mhina. Alipokuwa huko hakusomea Kiswahili lakini alipenda Kiswahili kwa sababu:

(a) Ya uzalendo wake na kukuza utamaduni.

(b) Hakuna lugha iliyo bora kuliko nyingine. Alijaribu kuandika kwa Kiingereza lakini akashindwa, hivyo basi akahiari kuandika kwa Kiswahili.

(c) Uandishi lilikuwa kama jambo la ziada la kupitisha wakati.

(d) Lugha zetu hutoa mawazo yetu sawa au bora zaidi kuliko Kiingereza. Jambo hili ni dhahiri shahiri kwa sababu lugha ya Kiswahili ina sifa nyingi za kutumia kutoa maelezo ya kitu.

(e) Rais Nyerere alikuwa anatumia Kiswahili kwa usahihi sana. Jambo hili pia lilimtia motisha.

Kuna mambo kadha yaliyomtia motisha kuandika *Ukiwa* (1975). *Ukiwa* ni tawasifu yake.

Ingawa anaeleza kuwa hakuna mwandishi aliyemtia motisha katika kuandika anaeleza kuwa;

(a) Maandishi ya Shabaan Robert, mawazo na sera yake, yalimuathiri alipokuwa katika kidato cha tano na sita.

(b) Mwalimu Julius Nyerere alikuwa fanani yake katika matumizi ya Kiswahuili. Hili limtia Mkangi mwoyo alipokuwa katika kidato cha tano na sita.

(c) Alikuwa anaandika matukio yake mwenyewe ya ujana.

(d) Kama mzalendo alipenda lugha yake. Ingawa watu wengi waliosoma hawapendi lugha ya Kiswahili lakini yeye anapenda Kiswahili.

**Waandishi Waliomwathiri**

Mawazo ya mwanasanaa huyu aliyetuama yaliathiriwa na watu wafuatao: Mwalimu Nyerere, Karl Marx, Paul Frere, Walter Rodney, Fidel Castro, Sheikh Vera, Shaaban Robert na Yesu Kristo hasa mafunzo yake. Ikumbukwe kwamba Mwokozi Yesu Kristo alitoa mafunzo yake kwa njia ya ngano.

Wengine waliomwathiri ni wanamapinduzi kama Mao Tse Tung, Augustino Neto (wa Angola), Kwame Nkurumah wa Ghana, Nelson Mandela aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, aliyekuwa wakati mmoja rais wa Burkina Faso, Thomas Sankara, Patrice Lumumba wa Congo na Muamar Gadhafi wa Libya. Wengi wa waandishi hawa na viongozi hawa ni watu wanaoshikilia mawazo ya mrengo wa kushoto. Siasa zao ziliegemea katika ujamaa. Bila shaka siasa za Mkangi kama mwandishi zimeathiriwa na watu hawa. Ingawa mwenyewe anasema kuwa alitaka kuchukua mtindo ulio tofauti kabisa kwa kutumia hadithi za kale.

Maandishi ya *Mafuta* na *Walenisi* ni masimulizi na ngano za kale kuonyesha jinsi lugha hii ina utajiri usio na kifani. Hadithi alizotumia katika usanii wake aliweza kuzitunga yeye mwenyewe; kwa mfano hadithi ya majini aliyomtolea mtafiti, ambayo ipo katika sura ya nne kama mfano.

Uandishi wake wa riwaya ya *Mafuta* ulichochewa na jinsi mambo yalivyokuwa mabaya hapa nchini. Siasa zilikuwa mbaya sana. Riwaya hii inachamba serikali kwa vitendo vyake. Alitumia jazanda katika kuelezea ukweli wa mambo kupitia kwa hadithi alizotoa katika riwaya ya *Mafuta* na *Walenisi.*

George Katama Mkangi aliweza kuwekwa kizuizini kwa muda wa miaka miwili 1986 – 1988 huko Naivasha Maximum Prison. Kabla ya kuwekwa kizuizini alihojiwa kwa muda wa siku sabini na tano (75). Alihitajika kukiri kuwa ametubu. Mahojiano haya yaliongozwa na aliyekuwa Mkuu wa Polisi Marehemu Bwana Kilonzo. Alipokuwa huko ndipo alipoandika riwaya yake ya *Walenisi.* Alinileza kuwa, "unapokuwa kizuizini huwa upo katika ulimwengu mwingine," ndipo aliweza kutumia taswira ya safari na nchi ya Walenisi na utawala wa Wachuna. Alieleza mateso ya wafungwa wa kisiasa, tazama riwaya ya *Mafuta* (ukurasa 41). Kwa muhtasari dhuluma zilizokuwa nchini na kuzuiliwa kwake vimechangia katika uandishi wake.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**Kazi zake zingine ambazo hazijachapishwa**

1. MLO - (Maskini Liberation Organization).
2. *Hadithi za Mfalme Tapwaratapwara.* (Hii ni hadithi fupi).
3. Mswada wa *Ningekuwa Mungu.* (Hii ni tamthilia).
4. *Mazingaombwe.*
5. *Matunda sita mtini.* (Hadithi za watoto).

Msanii huyu alikuwa na furaha kutaka kunieleza maswala niliyomwuliza. Niliahidi kukutana naye tena kadiri kazi ya tasnifu yangu ilipoendelea. Lakini alituama ghafla kutokana na ajali ya barabarani. Mungu amrehemu.

## Marejeleo


Abdilatif, A. (1973). Sauti ya Dhiki. Nairobi: Oxford University Press.

Arvon, H. (1973). Marxism and Esthetics. London: Cornell University Press.

Bolt, R. (1960). A Man for All Seasons. London: Heinemann.

Cantalupo, C. (Editor) (1995). The World of Ngugi wa Thiong'o. Trenton New Jersey: Africa World Press Inc.

Chacha, L.M. (2003). Mwongozo wa Walenisi. Nairobi: Africawide Network.

Chacha, N.C. (1987). Meaning and Interpretation of Swahili Poetry. *A Potrayal of a Changing Society*. Ph.D Dissertation. Yale University: U.S.A.

Coombes, J. (1953). Literature and Criticism. Middlesex: Chatto and Windus.

Dickinson, M. (Editor) (1972). When Bullets begin to Flower. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Eagleton, T. (1983). Literary Theory. England: Basil Blackwell Publishers Ltd.

Fanon, F. (1977). The Wretched of the Earth. New York: Grove Press Inc.

Foster, E.M. (1927). Aspects of the Novel. Harmondsworth: Penguin Books Ltd.

Finnegan, R. (1970). Oral Literature in Africa. Nairobi: Oxford University Press.

---------------- (1970). Oral Poetry. London: Cambridge University Press.

Gibbe, A.G. na Mvungi, T.A. (1987). Fasihi Simulizi kwa Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: Standard Publishing Company.

Gombes, H. (1963). Literature and Criticism. London: Penguin Books Middlesex.

Hugo, V. (1862). Les Miserables. London: Penguin Books.

Hussein, E. (1976). Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi. Nairobi: Oxford University Press.

-------------- (1973). Mashetani. Nairobi: Oxford University Press.

----------------(1969). Kinjekitile. Dar-es-Salaam: Oxford University Press.

Kamera, D.S. (2003). *'Fasihi simulizi na uandishi katika shule za Msingi'.* Katika makala ya semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili III. Fasihi. Dar-es-Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kibwana, K. (1985, Septemba 20). *No 'See –Through' Literature Here.* The Weekly Review p. 120: Nairobi.

King'ei, G.K. (2002). *Swala la Uana katika Fasihi ya Kiswahili.* Eldoret, Uhakiki wa Utafiti kutoka Kenya katika Simala, I.k. Mhariri Utafiti wa Kiswahili. Chakita, Moi University Press. Moi University.

---------------------(1996 Mei 10) *The Ethics of Socialism.* The Weekly Review p. 100: Nairobi.

Kirumbi, P.S. (1975). Misingi ya Fasihi Simulizi. Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.

Lukac's, G. (1972). The Meaning of Contemporary Realism. London: Merlin Press.

Liyong', T. (1969). Fixions and other Stories. London: Heinemann Ltd.

Mc Ewan, N. (1983). Africa and the Novel. London: Macmillan press Ltd.

Mandel, E. (1968). Marxist Economic Theory. London: Merlin Press.

Matteru, M.L. (1987). *Tanzu na Fani za Faishi Simulizi* katika Mulika 19. Dar es Salaam: TUKI.

-----------------(2003 ) *'Fasihi simulizi na Uandishi wa Kiswahili'*, katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mazrui, A. (1984). Uchambuzi wa *Dunia Mti Mkavu* katika Juzuu 51/1 & 51/2, 1984. Kiswahili. Jarida la TUKI Chuo Kikuu Dar-es-Salaam.

--------------- (1981). Kilio cha Haki. Nairobi: Longhorn.

---------------- (1988). Chembe cha Moyo. Nairobi: Heinemann.

Mazrui Almin na(1992). Uchambuzi wa Fasihi. Nairobi: East African
Syambo, B. Educational Publishers Ltd.

Mazigwa, S.A. (1991). Fasihi ya Kiswahili. Dar es Salaam: Benedictive Publication Ndanda.

Mbiti, J.S. (1966). Akamba Stories. London: Oxford University Press.

Mbughuni, P. (1978) *The Theme of A new Society in Kiswahili Prose Tradition* katika Vol. 48/2 Septemba, 1978. Kiswahili. Jarida la TUKI Chuo Kikuu Dar-es-Salaam.

Miliband, R. (1976). Marxism and Politics. London: Oxford University Press.

Miruka, O. (1997) Encounter with Oral Literature. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mkangi, G.K. (1984). Mafuta. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

-------------- (1995). Walenisi. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mohamed, S.A. (1976). Nyota ya Rehema. Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S.A. (1995). Amezidi. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Mulokozi, M.M. (2003). *Utafiti wa Fasihi Simulizi*, katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya waandishi wa Kiswhaili III: Fasihi. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Msokile, M. (1992). Kunga za Fasihi na Lugha. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors.

Mutegi, M.J.N. (1985). *Uhakiki wa tamthilia tano za Kiswahili za Ebrahim Hussein.* Nairobi: Tasnifu ya Uzamili (MA). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Nazareth, P. (1972). Literature and Society in modern Africa. Nairobi: East African Literature Bureau.

Ngara, E.A. (1980). Art and Ideology in the African Novel. London: Heinemann Educational Books.

Njogu, K. na (1999). Chimerah, R. Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. (1988). Mwongozo wa Kilio cha Haki. Nairobi: Heinemann Kenya.

------------ (1997). Uhakiki wa Riwaya za Visiwani. Nairobi: University of Nairobi Press.

Ogoti, B.A. (1969). Zamani, A Survey of East African History. Nairobi: Longman Kenya Limited.

Okpewho, I. (1983). Myth in Africa. London: Cambridge University Press.

Owen, C. (1971). Social Stratification. London: Routledge and Kegan Paul Ltd.

Ousmane, S.C. (1976). God's Bits of Wood. London: Heinemann African Writer Series.

Raban, J. (1968). The Techniques of Modern Fiction. London: Edward Arnold.

Rice, P. and (1989). Waugh, P (editors) Modern Literary Theory 2nd Ed. London: Edward Arnold.

Robert, S. (1946). Kufikirika. Nairobi: Nelson.

------------ (1951). Kusadikika. Nairobi: Nelson.

-------------(1952). Adili na Nduguze. London and Basingstoke. Macmillan Publishers Ltd.

Senkoro, F.E.M.K (1982). Fasihi. Dar-es-Salaam: Press and Publicity Centre.

----------------------(1987). Fasihi na Jamii. Dar-es-Salaam: Press and Publicity Centre.

Thomson, D. (1962) 2nd Edition. Europe since Napoleon. London: Longman, Green and Company Ltd.

Vasquez, A.S. (1973). Art and Society London: Merlin Press.

Walter, R. (1989). How Europe Underdeveloped Africa. Nairobi: East African Educational Publishers.

Wamitila, K.W. (2002). Uhakiki wa Fasihi. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

----------------- (2003a). Kichocheo cha Fasihi. Nairobi: Focus Publication Ltd.

------------------ (2003). Mwongozo wa Walenisi. Nairobi: Sasa Sema Publication Ltd.

------------------ (1998) Towards unlocking Katama Mkangi's Walenisi. *A case of Parabolic Narrative?* Katika Kiswahili Juzuu 61, 1998. Jarida la TUKI Chuo Kikuu Dar-es-Salaam.

Wa Thiong'o, (1977). Petals of Blood. London: Heinemann

-----------------(1986). Decolonizing the Mind. Nairobi: Heinemann Educational Books Inc.

------------------- (1987). Matigari. London: Heinemann.

------------------- (1994). Writers in Politics. Nairobi: East African Educational Publishers.


KENYAT... LIBRARY